# Nipashe

Jumatano Oktoba 2, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580038

www.ippmedia.com

...om/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Wafa kwa kupigwa na radi wakinywa pombe kilabuni

UKURASA 12



Democratic waungana kumchunguza Trump

siasa

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Rwanda inavyojijengea heshima kupitia wahamiaji toka Libya

Umakini muhimu tamu, chungu mitandao ya kijamii katika siasa

Marekani na kigugumizi kupigwa visima vya mafuta Saudi Arabia

Kwa nini CIA haikugundua shambulio la Septemba 11? Ukurasa 19

UKURASA 13

# Mambo 7 pasua kichwa Mkurugenzi mpya NEC

UKURASA 2



Wafanyakazi tisa wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi. **Habari Uk. 2. PICHA: MIRAJI MSALA**

## Miradi ya bil. 1.9/- mikononi mwa Takukuru

UKURASA 3

## Hakimu, mwanasheria wa Tanapa wamwangukia DPP

• **Yumo** pia wakili wa serikali, Kabendera naye ndani, raia wa kigeni nao wataka yaishe... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **ZAHERA, MATOLA SASA WALIAMSHA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mambo saba pasua kichwa Mkurugenzi mpya wa NEC

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Magufuli juzi alifanya uteuzi wa nafasi mbalimbali ikiwamo ya Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), huku Dk. Wilson Mahera akiteuliwa kushika wadhifa huo.

Dk. Mahera anachukua nafasi ya Dk. Athumani Kihamia aliyeshika nafasi hiyo kwa miezi 15 tangu alipoteuliwa.

Wakati Dk. Mahera anaingia katika taasisi hiyo nyeti ya kusimamia uchaguzi, anatarajiwa kukutana na mambo saba ambayo ni changamoto katika utekelezaji wake wa majukumu ikiwamo uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

**UCHAGUZI MKUU**

Kwa sasa imebaki miezi 12 kufikia uchaguzi mkuu ambao utafanyika kukiwa na daftari jipya lililoboreshwa. Jana jioni, Rais Magufuli, alimwapisha Dk. Mahera kushika nafasi hiyo.

Kwa mujibu wa NEC, uchaguzi huo ambao utafanyika Oktoba 25, mwakani, kwa mwaka 2015 Tanzania Bara kulikuwa na vituo vya kupigia kura 36,549 na mwakani vinatarajia kuwa 37,407, huku 6,208 vikibadilishwa majina. Kwa upande wa Tanzania Visiwani vimeongezeka kutoka 380 hadi 407.

Iwapo mkurugenzi huyo atadumu kwenye nafasi hiyo bila kutumbuliwa, atakuwa na wajibu wa kusimamia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Uchaguzi huo unafanyika wakati Rais Magufuli, akiingia katika kipindi cha pili na iwapo atachaguliwa atakuwa Rais kwa awamu nyingine ya miaka mitano kwa mujibu wa katiba.

Kipindi cha uchaguzi, NEC itakuwa na wajibu wa kuhakikisha mchakato huo unafanyika vizuri kwa maana ya kusambaza vifaa vya kupigia kura kwa wakati, kukusanya masanduku ya kura na kuhesabu. Baada ya hapo, itakuwa na kazi ya kuhesabu kura na kutangaza matokeo kwa wakati.

**DAFTARI LA WAPIGAKURA**

Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ulioanza Julai 18, mwaka huu, kwenye mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, ni moja ya changamoto ambazo anapaswa kuzifanyia kazi na huenda kikawa kigingi kikubwa katika utekelezaji wa majukumu yake. Uboreshaji wa daftari hilo unatarajiwa kukamilika Machi, mwakani.

Kwa sasa kinachofanyika kwenye daftari hilo ni kuondoa majina ya waliofariki dunia,

INAENDELEA UK 26



Kaimu Balozi wa Marekani hapa nchini, Dk. Inmi Patterson (kulia), akikabidhi ruzuku kwa mwanzilishi mwenza wa Asasi ya Tanzania Data Lab, Mahadia Tunga, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Ukimwi Tanzania kupitia Mfuko wa Balozi wa kupambana na VVU/UKIMWI. Zaidi ya Sh. milioni 574 zimetolewa kwa asasi za kiraia 11 zilizosajiliwa, zisizojiendesha kibiashara na za kidini kutoka maeneo mbalimbali nchini. Kushoto ni Meneja Fedha na Utawala wa asasi hiyo, Nguza Kinonda. **PICHA: JOHN BADI**

# Hakimu, mwanasheria wa Tanapa wamwangukia DPP

**Na Waandishi Wetu**

WATUHUMIWA watano wa kesi ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi wakiwamo Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Bernad Nganga na Mwanasheria wa Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Maneno Mbunda, wamemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuomba wakiri makosa na kusamehewa.

Sambamba na wawili hao, wengine ni Mwanasheria wa Serikali, Fortunatus Mhalila, Nelson Kangero na Tumaini Mdee ambao kwa pamoja wanakabiliwa na mshtaka tisa.

Licha ya vigogo hao, Kangero ambaye anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ya meno ya tembo pia ameandika barua ya kuomba kukiri mashtaka yake na kuomba msamaha.

Mapema katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Wakili wa Utetezi, Upendo Msuya, akisaidiwa na Fridolin Bwemelo, aliileza mahakama hiyo mbele ya Hakimu Rose Ngoka kwamba wateja wake wameandika barua ya kukiri na kuomba msamaha kutokana na agizo la Rais John Magufuli na kwamba mpaka sasa hawajapata maelekezo yoyote kutoka ofisi ya DPP.

Kutokana na sababu hizo, Wakili Msuya aliiomba mahakama kuwapangia tarehe ya karibu wateja wake ili majibu ya DPP yakitoka wafike mahakamani hapo kwa ajili ya utekelezaji.

Awali, Wakili wa Jamhuri Elianinenyi Njiro, alidai mahakamani kuwa shauri hilo limekuja kwa ajili ya kutajwa kwa kuwa upelelezi wa shauri hilo ulishakamilika lakini jalada lilipelekwa kwa DDP.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo Mei 6, mwaka huu, na kusomewa mashtaka 11 na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Javelin Rugahuruza, yakiwamo ya kujihusisha na rushwa, kughushi na kujipatia mali kwa njia ya rushwa kati ya Juni Mosi, 2018 na Aprili 15, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali.

Mashtaka mengine waliyosomewa ni kuchukua rushwa ya Sh. milioni 31.5 toka kwa Kangero, utakasaji fedha ya Sh. milioni 31.5, kughushi nyaraka za uwongo za nyara ya serikali za kilo 15 za meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 9.8.

Kangero pia anakabiliwa na shtaka la uhujumu uchumi kwa kukutwa na vipande 15 vya meno ya tembo vya thamani ya dola za Kimarekani milioni 15,000 sawa na Sh. milioni 108 bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

**WENGINE WATAKA YAISHE**

Raia 10 wa kigeni waliokuwa wanafanya kazi katika kampuni ya Uwindaji ya Oterlo

INAENDELEA UK 26

# Vigogo NSSF kortini tuhuma za utakatishaji

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO tisa wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), akiwamo Kaimu Mkurugenzi wa Fedha, Jamila Vulu, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kughushi, wizi na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Washtakiwa hao walisomewa jana mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Kelvin Mhina katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni mwandishi wa hundi, Abdul Njozi; Meneja Uhakiki, Amir Kapera; Mhasibu James Oigo, Mhasibu Mkuu, Hellen Peter na Mhasibu Mwandamizi anayeshughulikia matumizi, Ivonne Kimaro.

Wengine ni Kaimu Meneja Rasilimali Watu, Tikyeba Alphonce na Mhasibu Dominic Mbwete.

Simon alidai kuwa katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Julai Mosi, 2016 na Septemba 4, 2017 walikula njama ya kutenda makosa ya kughushi na kutakatisha fedha.

Katika shtaka la pili, mshtakiwa Njozi na Akiri wanadaiwa katika kipindi hicho, wakiwa watumishi wa umma, kwenye ofisi za makao makuu ya NSSF, walighushi hundi 47 za Benki ya CRDB kwa akaunti namba 01J1028249500 yenye jina la NSSF zenye jumla ya Sh. 2,130,211,437.35.

Katika shtaka la tatu, washtakiwa wote wanadaiwa katika kipindi hicho, wakiwa Makao Makuu ya shirika, waliiba fedha hizo.

Washtakiwa hao pia wanashtakiwa kwa tuhuma za kusababisha hasara ya Sh. 2,130,211,437.35 kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao wakiwa watumishi wa umma.

Shtaka la mwisho, washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha kiasi hicho cha fedha, huku wakijua fedha hizo zimetokana na mazalia ya fedha za kughushi.

Hakimu Mhina alisema mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi, hivyo washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote mpaka pale upelelezi utakapokamilika na kesi kuhamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa, maarufu kama Mahakama ya Mafisadi.

Alisema kesi itatajwa Oktoba 15, mwaka huu na kuamuru washtakiwa wapelekwe mahabusu kwa kuwa mashtaka ya kutakatisha fedha hayana dhamana.

## HABARI KITAIFA

# Takukuru yachunguza miradi ya bil. 1.9/-

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Dodoma, imeanza kufanya uchunguzi katika miradi minne yenye thamani ya Sh. bilioni 1.9 kutokana na kuwapo kwa viashiria vya rushwa.

Miradi hiyo ni pamoja na mitatu ya elimu ya lipa kulingana na matokeo (P4R) iliyopo wilaya za Kongwa na Bahi na Hospitali ya Wilayani Chamwino.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Taasisi hiyo mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, alipokuwa akitoa taarifa ya robo ya mwaka kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Alifafanua kuwa taasisi hiyo ilifuatilia miradi 39 ambayo ni ya sekta ya ujenzi wa miundombinu, elimu, maji, afya na kilimo yenye thamani ya Sh. bilioni 46.9, ambapo wamebaini miradi minne kuwa na viashiria vya rushwa.

"Takukuru imeanza uchunguzi katika miradi hiyo, lengo ni kuona inatekelezwa ipasavyo ili kuinua maendeleo ya wananchi wa eneo husika na Taifa kwa ujumla," alisema Kibwengo.

Katika hatua nyingine, alisema Takukuru imeingilia kati utekelezaji wa mkataba wa uundwaji wa kampuni kati ya halmashauri moja na taasisi binafsi kwa ajili ya kununua maeneo,kuyapima,na kuuza viwanja.

"Mkataba huu ungeweza kuisababishia halmashauri ya Jiji la Dodoma hasara ya zaidi ya Sh. milioni 700 kutokana na baadhi ya taratibu hazikufuatwa hivyo tumeelekeza kabla ya kuendelea na mchakato huo taratibu zifuatwe,"alisema.

Kibwengo alisema kwa kipindi hicho, Takukuru imepokea tuhuma 155 za rushwa kwenye sekta mbalimbali huku kata,mitaa na vijijini zikiongoza kwa asilimia 39.4.

Aidha, alisema sekta ya ardhi tuhuma za rushwa ni asilimia 13.5, elimu asilimia 12.3, Mahakama asilimia 7.7,Wizara asilimia 5.8,Polisi asilimia 5.2,sekta binafsi 5.2, na Maji 4.5.

Kadhalika, alisema Taasisi hiyo imekamilisha majalada 15 ya uchunguzi ikiwemo kufungua mashauri nane ambayo washtakiwa wake ni watu binafsi, watumishi wa sekta mbalimbali ikiwamo elimu na kilimo. Pia wamo watumishi wa Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), Wakala wa Barabara (Tanroads), watendaji wa kata, vijiji, na askari wa jeshi la akiba.




Baadhi ya wazee wa Mkoa wa Dodoma, wakishiriki maandamano kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani, katika barabara ya Nyerere, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watatu wauawa Dar tuhuma za ujambazi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewaua watuhumiwa wa ujambazi watatu akiwamo aliyeuawa nje ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alisema jana kuwa katika tukio la kwanza, Jeshi la Polisi limemuua mtuhumiwa Emmanuel Peter ambaye alikuwa anasakwa kwa muda mrefu.

Alisema mauaji hayo yalitokea juzi eneo la Ilala Boma majira ya mchana, ambapo polisi ilipata taarifa kutoka kwa msiri kuwa mtuhumiwa huyo yupo na wenzake wanne.

"Msiri wetu alituambia Peter maarufu kama Mark Silengo, akiwa na wenzake wanne wanapanga mipango ya kwenda kufanya uhalifu," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema kikosi kazi kilifika eneo hilo la tukio na kumkuta mtuhumiwa huyo na ghafla alishtukia amezungukwa na askari, ndipo alipotoa silaha kwa nia ya kuwafyatua risasi polisi.

"Polisi waliokuwa eneo la tukio walimuwahi na kumjeruhi mtuhumiwa huyo, na kumnyang'anya bastola ikiwa na risasi mbili, na risasi moja ikiwa chemba imepakiwa tayari kwa kufyatuliwa," alisema. Alisema mtuhumiwa huyo alipelekwa hospitali, lakini na kufariki dunia, na mwili wake umehifadhiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Katika tukio la pili, Mambosasa alisema Alhamisi iliyopita mchana eneo la Mbezi Msakuzi njia panda ya Mpiji Magoe.

"Tulipata taarifa kuna watuhumiwa wa ujambazi ambao wamejipanga kwenda kuvamia Vyama vya Akiba na Mikopo (Saccos) ya Msakuzi. Tuliweka mtego na ilipofika saa sita mchana zilifika pikipiki mbili aina ya Boxer ambazo hazikusomeka namba zake zikiwa na watu wanne, mmoja akiwa na bastola," alisema.

Alisema watu hao walipogundua wanafuatiliwa, walikimbia ndipo askari walipofyatua risasi kwa nia ya kuwasimamisha, lakini nao walijibu mapigo.

Alisema katika majibizano ya risasi, polisi iliwajeruhi watuhumiwa wawili ambao walifariki dunia baadaye na wengine walikimbia.

Alisema majeruhi hao walikutwa na bastola moja na risasi tatu ndani ya magazine na makanda mawili ya risasi.

Wakati huo huo, Jeshi hilo limekamata magari 50 yakiwamo 19 ya serikali ambayo yalikutwa yakipita kwenye barabara ya mwendokasi.

"Ninaendelea kutoa onyo kwa madereva wa serikali na watu binafsi waache mara moja kupita kwenye barabara ya mwendokasi," alisema.

## Wazee Chadema wafunguka mazito

**Na Enock Charles**

BARAZA la Wazee la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), limeitaka serikali kurejea ahadi yake ya kumalizia mchakato wa katiba mpya iliyoitoa mwaka 2015 wakati wa uchaguzi mkuu.

Wazee hao wamedai kuwa mchakato huo bado una umuhimu mkubwa kwa Watanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hashim Juma Issa, alidai kushangazwa na ukimya wa serikali kuhusu mchakato huo ambao uligharimu fedha nyingi za Watanzania.

Wazee hao wanadai kusitishwa kwa mchakato huo ni hasara kubwa kwa Taifa kwa kuwa mchakato huo ulishaanza na umegharimu fedha nyingi, hivyo kutaka uendelezwe kwa maslahi ya Taifa.

Katika hatua nyingine, wazee hao wamelalamikia kuingiliwa kwa mikutano ya wabunge wa chama hicho na Jeshi la Polisi, wakidai kitendo hiko ni ukiukwaji wa misingi ya demokrasia nchini na kounya kuwa vitendo hivyo vinaweza kupelekea uvunjifu wa amani.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, wameapa kulinda kura kwa madai ya kuchoka kuibiwa kura kila uchaguzi unapofika, na kulionya Jeshi la Polisi kuwa waangalifu katika uchaguzi huo ili kuepusha uvunjifu wa amani.

"Safari hii hatukubali tena tunaanzia kwenye uandikishaji... mambo ya kusema sijui wewe hujatimiza vigezo, wewe sijui haujakamilika sifa, hatukubali," alisema.

MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA

SHAURI LA MADAI NAMBA 27 YA MWAKA 2019

ACCESSBANK TANZANIA LIMITED.................. .............................. MDAI

DHIDI YA

1. GRATION G. KYARUZI

2. ADVELLA M. NDYETABURA..........................................................WADAIWA

KWA: WADAIWA WOTE

POPOTE MLIPO

Mahakama hii inawafahamisha kwamba Mdai amefungua madai dhidi yenu nakala yake inapatikana katika Mahakama hii

Shauri dhidi yenu limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 17/10/2019 saa 2.30 asubuhi na mnatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wenu dhidi ya madai haya

Zingatia kwamba kutokufika kwenu tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya ninyi kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.

Imetolewa kwa Mkono Wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20/09/2019

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI

MWANZA

215440302

# Z'bar yapata suluhisho la uhaba wa mafuta

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**



SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imezindua meli mpya ya mafuta Mv Mkombozi namba mbili, huku ikielezwa kuwa tasaidia kuondoa tatizo la uhaba wa mafuta katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Akizindua meli hiyo katika bandari ya Malindi Mjini Zanzibar, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, alisema baada ya uzinduzi wa meli hiyo hatarajii kuona uhaba wa mafuta unajitokeza tena visiwani Zanzibar.

"Sitaki kuona hamkani (tafrani) foleni mtindo mmoja katika vituo vya kuuzia mafuta sababu mafuta hamna... meli ndio hiyo hapa," alisema Dk. Shein.

Rais aliwataka viongozi kuhakikisha wanawalipa wafanyakazi wa meli hiyo mishahara inayostahili kwani wana kazi kubwa.

Alieleza kuwa kazi wanayoifanya ya kusafiri na meli muda mrefu sio kazi rahisi, hivyo ni vyema kuwajali wafanyakazi hao na kuwapatia mafunzo mbalimbali ili kufanyakazi zao kwa ufanisi.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa meli hiyo kuhakikisha wanajua kanuni, taratibu na sheria za nchi za kitaifa na kimataifa.

Alieleza bila ya kufuata kanuni, nidhamu, uadilifu na uwajibikaji wa kazi utendaji wa kazi utadorora.

Dk. Shein alisema serikali yake imeamua kuliimarisha na kulifanyia mabadiliko shirika la meli ili liwe la kisasa na kujiendesha kibiashara.

"Ulimwengu huu ni wa kibiashara kwa maendeleo ya nchi, hivyo serikali ya Zanzibar haiogopi kufanya biashara," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Mustafa Aboud Jumbe, alisema meli hiyo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 za mafuta itaimarisha uchumi wa Zanzibar.

Alisema meli hiyo ina uwezo wa kubeba tani hizo za mafuta kwa wakati mmoja.

Alieleza serikali imetumia Sh. bilioni 36 kununua meli hiyo, na kuwa fedha zote imeshalipwa.






# Bilioni 65/- zatengwa kujenga minara

**Na Prisca Ulomi, MWANZA**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 65 kwa ajili ya kujenga minara ya mawasiliano kwenye maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa lengo la kukuza uchumi na kufanikisha utoaji wa huduma za serikali kwa wananchi na kurahisisha uendeshaji wa shughui za kijamii.

Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema hayo wakati akikagua upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwenye kata ya Nyampande iliyopo wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Malaga kilichopo kwenye Kata ya Nyampande, Mathayo Thobias, aliishukuru serikali kwa huduma ya mawasiliano wanayoipata na kuwa chanzo cha mapato kutokana na serikali ya kijiji kupata Sh. milioni 3.6 ambazo inalipwa na kampuni ya Vodacom inayomiliki mnara huo.

Nditiye alisema, tayari serikali imetenga Sh. bilioni 65 za kujenga minara ya mawasiliano ipatayo 1,222 kwenye kata 521 sehemu mbalimbali nchini kwa kuupa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ruzuku ya kuzipa kampuni za simu za mkononi fedha hizo kupitia utaratibu uliowekwa, kwa kuzingatia vigezo na masharti ya zabuni baada ya UCSAF kutangaza zabuni ya kujenga minara hiyo.

Alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa sekta ya mawasiliano inaongeza mchango wake kwenye pato la taifa kwa kuongeza kiwango cha uchangiaji kutoka asilimia 13.1 kwa mwaka 2017/2018 kwa kushika nafasi ya tatu.

"Hapa tulipo wote tuna simu za mkononi na hakuna atakayekaa zaidi ya nusu saa bila kushika simu yake ya mkononi," alisema Nditiye.

Amesema lengo la Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa ya mfano na tayari nchi nyingi za Afrika zinajifunza kutoka Tanzania katika Sekta ya Mawasiliano na dhamira ya serikali ni kuendeleza hekta hiyo ili kwenda sambamba na nchi zilizoendelea duniani.

Tanzania iko vizuri kati ya nchi chache za Afrika kama Afrika Kusini na Mauritius kwa upande wa mawasiliano.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amemweleza Nditiye kuwa mkoani kwake usikivu wa mawasiliano uko vizuri, mawasiliano yanasikika kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

"Zamani hata likitokea tukio inachukua wiki kufahamu ila sasa ni saa chache tu tunapata taarifa na kushughulikia," alisema Mongella.



# Serikali yaahidi makubwa kwa wazee

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kuwalinda wazee dhidi ya vitendo vya ukatili, kwa kuwawekea miundombinu na mazingira bora katika kutumia vyombo vya usafiri na kuweka utaratibu na vigezo vitakavyowawezesha kulipwa pensheni.

Pia ameyataka mashirika ya wazee yaelekeze rasilimali wanazozipata kutoa huduma za msingi kwa wazee na waepuke kutumia fedha nyingi kwenye mikutano, warsha na makongamano ambayo hayawafaidishi moja kwa moja wazee wenye uhitaji.

Alisema hayo jana wakati akihutubia wananchi katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee Duniani, yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja Nangwanda Sijaona, Manispaa ya Mtwara.

Alisema utoaji wa huduma kwa wazee ni moja ya vipaumbele vya serikali na kwamba itaendelea kuchukua hatua za kuboresha hali na maisha ya wazee nchini.

Alisema miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na serikali katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya wazee ni pamoja na kuanzishwa kwa mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wa kunusuru kaya maskini uliolenga kuyasaidia makundi mbalimbali ya jamii yanayoishi katika umasikini uliokithiri likiwamo kundi la wazee.

"Hadi kufikia Septemba 2019 jumla ya wazee 680,056 kutoka kaya 1,118,747 wananufaika na mpango wa Tasaf kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Mpango huu, umesaidia wazee kujikimu na kumudu majukumu ya kulea wajukuu ambao wazazi wao wamepoteza maisha kwa sababu mbalimbali ikiwamo ugonjwa wa Ukimwi."

Alisema serikali pia inaendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007 ambayo inatambua kuwa wazee ni kundi maalumu linalohitaji kupewa kipaumbele katika kupata huduma bora za afya, inaweka mkazo kuwa wazee wote wenye umri wa miaka 60 na kuendelea na wasiokuwa na uwezo watibiwe bila malipo.

Aliziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zoezi la kuwatambua na kuwapatia vitambulisho wazee wasiokuwa na uwezo linakuwa endelevu ili waweze kunufaika na huduma ya matibabu bila malipo wanapougua.

Kadhalika, Waziri Mkuu amevitaka vituo vyote vya kutoa huduma za afya vya umma kutoa huduma bora na za haraka kwa wazee wenye vitambulisho hivyo na watenge dirisha maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wazee ili wasikae kwenye foleni muda mrefu.

Awali, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala mbalimbali ya wazee ikiwa ni pamoja na kutafakari fursa za changamoto zinazowakabili wazee na namna ya kuzitatua.

Alisema taarifa kutoka Ofisi ya Rais-Tamisemi hadi Desemba 2018 jumla ya wazee 1,837,162 wametambuliwa na kati yao 684,383 wamepatiwa vitambulisho vinavyowawezesha kupata huduma za matibabu bila ya malipo.

TANGAZO


ULIPO
TUPO
Thamini kesho
yako na yake
ATM
Simbanking
www.crdbbank.co.tz
*150*03#
CRDB
BANK
Tunakusikiliza

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuwaepushe wazee na tiba za waganga

KUZUIA maradhi na kuhakikisha wazee wanakuwa na afya bora ni suala ambalo linastahili kuwa la kipaumbele wakati huu serikali na jamii inapoadhimisha Siku ya Wazee Duniani.

Ndiyo maana tunaweza kusema uzee bila tiba ni kama uzee uliodharauliwa kwa sababu unapokuwa na umri huo ndipo milango ya maradhi na kudhoofika kiafya inapofunguka.

Taifa lipowakumbuka wazee leo, hebu tutizame hali zao na jinsi walivyo na mchango mkubwa kwa taifa letu.

Itakumbukwa kuwa wazee hawa wanashambuliwa na magonjwa na wengi huendelea kujitibu kwa mitidawa na huduma nyingine za tiba asilia.

Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wa taifa hili wanahitaji huduma na utaratibu ambao utafanya maisha yao kuwa mepesi hasa kwenye kupata tiba.

Ndiyo maana tunaona kuwa tunapoadhimisha Siku ya Wazee wetu, tutafakari jinsi ya kuwaondoa kwenye giza la tiba za asilia na hata wakati mwingine kukimbilia kwa waganga wa ramli.

Wazee hawa wake kwa waume, mara nyingi tunawashuhudia, ambavyo wamekuwa wakisota iwe kwenye zahanati, hospitali za wilaya, mikoa na hata za rufani bila kupata huduma licha ya kuwa na kadi za wazee.

Mara kwa mara wale ambao watoto wao au jamaa zao hawakuwaingiza kwenye mfumo rasmi wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), tumewashuhudia wakihangaika mno kusaka tiba.

Wazee hao ambao mara nyingi inakuwa vigumu kupata vipimo vikubwa hata pale wanapotumia kadi za Mfuko wa Huduma ya Afya ya Jamii Ulioboreshwa, wanahitaji kufikiriwa upya sasa kuhusu matibabu.

Ndiyo maana tunaona kuwa pengine ni wakati wa kufikiria namna bora ya kuwa na Mfuko wa Bima ya Afya Wazee kama ambavyo kuna toto afya kadi ya watoto wadogo na walio chini ya miaka 18.

Tunasema hivyo kwa sababu ni vigumu wazee hawa waliolitumikia taifa kwa miongo kadhaa kuwa na uwezo wa kujigharamia matibabu kwa jinsi ya hali halisi ilivyo sasa.

Licha ya huduma ya toto afya kuondoa baadhi ya tiba muhimu kama X-ray ya MRI, kipimo cha CT Scan, kusafisha damu, tiba ya saratani, tiba ya moyo, kutibu na kupandikizwa figo tunaona kwa wazee ndiyo mambo wanayoyahitaji.

Ni kwa sababu wazee hawa wanahitaji kufanyiwa vipimo kama vya MRI, CT Scan na hata kupewa dawa za saratani kwa kuwa maradhi hayo huambatana pia na umri wa uzee.

Ni vyema serikali ikakubaliana nasi kuwa iwapo taifa litaamua kuwa na kadi ya matibabu ya wazee ni muhimu ikaandaliwa kwa kutumia mfuko wa NHIF kama ilivyo ya watoto.

Ni muhimu kuangalia upya matibabu ya wazee hawa kwa sababu kama tulivyotangulia kusema tiba ni suala linalowaumiza wazee wengi mno hapa nchini.

Ni ukweli kuwa hata kama utafiti ungefanyika leo wazee wengi wangebainika kuwa na udhaifu kutokana na kudhoofishwa na magonjwa.

Licha ya kwamba chakula na umaskini ni suala linalowakabili wazee wa Tanzania, tiba ni jambo muhimu kwa ajili ya ustawi wa kundi hili.

Ndiyo maana umefika wakati wa kuanza utaratibu wa kuwatibu pengine hata kwa awamu. Serikali kuanzia sasa ianze mikakati ya kuandaa mfuko wa bima ya wazee kwa ajili ya ustawi wao.

Kuna mambo mengi yanayofanyika na yanagharamiwa na serikali ikiwamo mfuko wa barabara, mfuko wa mahakama na maeneo mengine kama hayo, hivyo ni wakati wa kuwakumbuka na kuwasaidia wazee.

Shime serikali iwakumbuke wazee hawa na kuwaondolea mzigo wa kikimbilia kwa waganga wa kienyeji na kula tiba za asilia ambazo mara nyingi haziwaponyeshi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# TCRA mko wapi wakati tunaibiwa?

**KATIKA** kikao cha Bunge la Bajeti, Mbunge wa Mwanga, Profesa Jumanne Maghembe, aliwasilisha kilio chake dhidi ya kampuni za simu kuwaibia wateja wake vifurushi na muda wa maongezi na alijibiwa kuwa hatua zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

Mbunge huyo ambaye amewahi kuwa waziri katika serikali ya awamu ya nne na tano, alisema kampuni hizo pia zinadanganya watu kwa kununua vifurushi.

Si ajabu pale mtu kwa mfano ana dakika 200, lakini anapokuwa ametumia dakika 45 kwa kufuatilia anaambiwa kuwa dakika zake zimekaribia kwisha!

Kilio cha Mbunge huyo ndiyo kilio cha watumiaji wengi wa simu nchini kwa kuwa kila siku wanayavumilia mengi yanayotendwa na kampuni za simu dhidi yao.

Mathalani, ipo kampuni moja ya simu wasione una salio kwenye mtandao ni lazima wakuonyeshe kuwa umeishiwa kifurushi na muda wa maongezi.

Ukiwauliza jibu lao siku zote ni rahisi sana kwamba muda wa maongezi au bando kwisha hutegemea na matumizi yako, hivyo unapoona imekuwa hivyo ujue matumizi yako ni makubwa.

Unaponunua muda wa maongezi kutoka kwa kampuni hizo unaokwenda sambamba na bando, ikitokea bando limekwisha basi muda wa maongezi nao umekwisha, na wakati mwingine bando likiisha na muda wa maongezi nao umekwisha.

Aidha, kampuni hizi zimeanzisha utaratibu wa kumwezesha mteja kununua muda wa maongezi moja kwa moja kutoka kwenye salio lake la simu, lakini kuna nyakati hawezi kufanya hivyo kwa kuwa wanataka ahamishe fedha hiyo kwenda kuwa muda wa maongezi ili akatwe kodi kwanza.

Mathalani, unanunua muda wa maongezi wa Sh. 5,000 kodi yake ni Sh. 762.71 maana yake unapaswa kununua zaidi ili kufidia gharama hizo zinazobwebwa na mtumiaji wa simu na kuwa maumivu kwake.

Wakati mwingine unapokuwa na salio kwenye simu yako ni lazima uzime data, ukinunua salio huku data inafanya kazi unajikuta salio lote limeisha ndani ya sekunde chache na ni kawaida kuchukua saa kadhaa kujiunga kupata vifurushi.

Kama haitoshi kuna wakati mtandao unagoma kubadilisha kifurushi, unaweza kununua zaidi ya mara nne na hupati ujumbe wa kubadilisha kwenda kwenye kifurushi na ukijaribu kupiga simu, unachukuliwa fedha yote iliyomo kwenye simu yako.

Unapojaribu kuwapigia huduma kwa wateja hupati majibu ya kuridhisha na matokeo yake watumiaji wa simu wanaendelea kuumia kila siku.

Miezi miwili iliyopita, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, alizionya kampuni za simu zilizokuwa zinatoza zaidi ya bei elekezi ya Sh. 10.40.

Aidha, kuna kampuni zinazojinadi gharama ya mtandao wowote ni Sh. moja kwa sekunde ambayo ni sawa na Sh. 60 bei ambayo inazidi mara tano ya gharama ambayo ni elekezi.

Alisema bei elekezi imepungua kutoka Sh.15.60 hadi Sh. 10.40, huku malengo ya serikali ni kuwa ifikapo 2021 kampuni zitoze Sh. 2 kwa dakika kwa mtandao wowote wa simu.

Aliiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuchukua hatua dhidi ya wahusika na kuhakikisha wateja wanarudishiwa fedha zao walizoibiwa kwa muda mrefu.

Licha ya serikali kutoa onyo na Bunge kulalamikia suala hilo na kuelekeza hatua kuchukuliwa, lakini bado wateja wanaendelea kuumia na kukosa pa kupeleka kilio chao.

Kwa ujumla watumiaji wa simu kila mmoja kwa nyakati zake ana kilio dhidi ya kampuni hizo, lakini cha kushangaza hatuoni hatua zinazochukuliwa au ahueni kwa watumiaji wa simu.

Wizi wa bando na dakika ni tatizo kubwa kwa mitandao ya sasa kiasi cha kujiona wanyonge, na wakati mwingine hakuna la kufanya kwa kuwa ni lazima mtu awasiliane kupitia simu.

Muungwana anaona kwamba ni vyema basi kwa msimamizi wa kampuni hizo ambaye ni TCRA akachukua hatua dhidi ya kampuni hizi, kuliko watu kuendelea kuumia kimya kimya.

**Ukiwauliza jibu lao siku zote ni rahisi sana kwamba muda wa maongezi au bando kwisha hutegemea na matumizi yako, hivyo unapoona imekuwa hivyo ujue matumizi yako ni makubwa.**

# Tani 40,000 za korosho zasafirishwa nje ya nchi

**Na Mary Geofrey**

TANI 40,050 za korosho zimesafirishwa kutoka mikoa ya Lindi na Mtwara kupitia Bandari ya Mtwara kuelekea nchi mbalimbali duniani hadi kufika Septemba 23, mwaka huu.

Hayo yalielezwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Joseph Buchweishaija, kupitia taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari, katika ziara aliyofanya ya kufuatilia ubanguaji wa korosho kwenye viwanda vilivyopo kwenye mikoa hiyo.

Alisema meli tatu zilizokuwa zimebeba kontena 1,015 sawa na tani 23,328 zimeondoka na kazi hiyo itakamilika kwa siku mbili na kwamba nyingine zipo njiani kwenda katika bandari hiyo kupakia.

"Serikali imeweza kusafirisha tani 40,050 za korosho kwenda nje ya nchi. Na hivi sasa ninavyozungumza tayari meli mbili zimepakia korosho na kuondoka, meli ya tatu imeanza kupakiwa na itabeba kontena 1,015 ambazo sawa na tani 23,328.

Kazi nzima itakamilika kwa siku mbili ikizingatiwa kuwa kuna meli nyingine mbili zipo majini na zitatia nanga na kuanza zoezi la kupakia korosho kwenda nje ya nchi," Prof. Buchweishaija alisema.

Kuhusu ubanguaji wa korosho zilizonunuliwa na serikali, alisema zimetoa ajira wakiwamo wanawake kwa asilimia 92.

"Tumefanikiwa vizuri na kuonyesha dalili kuwa Tanzania inaweza hasa tunapozungumzia nchi ya viwanda maana tukiuza korosho ghafi tunahamisha ajira na kutoa wito kwa viwanda kuendelea kuongeza uzalishaji ili ikiwezekana korosho zote zinazozalishwa Tanzania zibanguliwe nchini," Prof. Buchweishaija alisema.

Katika kutekeleza mpango wa ubanguaji, serikali kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), iliingia mikataba na viwanda vikubwa pamoja Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) kwa niaba ya viwanda na wabanguaji wadogo ili kubangua korosho.

Alisema viwanda vidogo vimefanikiwa kubangua korosho tani 607.75 kuwezesha wabanguaji wadogo 1,000 kupata ajira.

Kadhalika alisema, viwanda vikubwa vilibangua korosho tani 3,309.64 na kutoa ajira kwa watu 2,511 ambao kwa asilimia kubwa ni wanawake.

Alivipongeza viwanda vya ndani kwa kuwa na uwezo wa kuongeza thamani ya korosho ya Tanzania tangu Rais John Magufuli alipotangaza uamuzi wa serikali kununua zao hilo Novemba 12, mwaka jana.

"Nimejionea mwenyewe korosho zetu zilivyo na ubora unaostahiki, zinabanguliwa kwa utaalamu na zimefungashwa kwa kutumia vifungashio vizuri, katika madaraja yote hususani daraja la WS320 linalopendwa na wanunuaji wengi kutoka nje ya nchi. Hakika viwanda vyetu vinafanya kazi nzuri," Prof. Buchweishaija alisema.

Prof. Buchweishaija aliendelea kusema kuwa, ubanguaji wa korosho uligawanyika kwa viwanda vya aina mbili, viwanda vidogo vinavyosimamiwa na Sido pamoja na viwanda vikubwa.

# Wadau pamba waomba mfumo wa kidigitali

**Na Mwandishi wetu, MWANZA**

WADAU wa pamba wameomba kuwekwa mfumo wa kidigitali utakaosaidia kutatua changamoto zinazowakabili wakulima.

Ushauri huo ulitolewa wakati wakizungumza katika Mkutano wa 16 wa wadau wa pamba ambao ulihudhuriwa na ujumbe wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

Walisema mfumo huo utasaidia mambo mbalimbali ikiwamo wakulima kutambulika na kusajiliwa kidigitali.

Akitoa tathmini ya hali ya zao hilo, Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba, Marco Mtunga, alisema mfumo huo unahitajika ili kuwasajili wakulima na pia katika ukopaji, uuzaji na urejeshaji wa mikopo vikarabatiwe kupitia mfumo huo.

"Tunashauri pia uhakika wa kurejesha madeni na bima ya mazao vitahamasisha vyombo vya fedha kufanya kazi na AMCOs," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema mkutano huo unalenga kuweka mikakati na kujadili fursa mbalimbali na kutatua changamoto za namna ya kuinua uchumi kupitia zao la pamba.

"Moja ya mikakati ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo, ni kuleta mapinduzi katika kilimo kwa kuwekeza katika mnyororo wa thamani ya mazao mbalimbali ikiwamo pamba, hivyo katika majukwaa ya wadau wa pamba nchini ni tija ya kufikisha malengo ya kuinua thamani ya zao hilo," alisema. Aidha, alifafanua kuwa mfumo wa dhamana kwa wakulima wadogo lengo lake ni kuona wakulima wa zao la pamba wanawezeshwa na kuendelea kumiliki thamani ya zao la pamba, si kulima tu na kuziuza, bali kuweza kuwa na viwanda na kumiliki masoko.

"TADB ina mikakati ya kutumia 'Mfumo Jumuishi' ambao ulitumika kusajili wakulima wa zao la kahawa na matokeo yake ni chanya, hivyo kuna mpango kuwaingiza wakulima wa zao la pamba katika mfumo huo ili nao wanufaike na ubunifu wa kidigitali katika kufanya miamala mbalimbali ikiwamo, kupokea malipo, mikopo na uwekezaji," alisema.

Naye Naibu Waziri Bashe alisema mikakati ya benki hiyo kwa zao la pamba, ni kuleta mabadiliko na kumfikia mkulima mmoja mmoja wa pamba pamoja na vyama vya ushirika kwa kuwajengea uwezo wa kibiashara na kuhakikisha wakulima wananufaika na zao hilo.

"Kutokana na ukuaji wa kasi katika uzalishaji wa pamba nchini kwa 2018/2019 unakadiriwa kuwa tani 400,000 na lengo ni kuzalisha tani 1,000,000 kwa mwaka 2020/21 kwani uwezo tunao, hivyo tunatakiwa kuzifufua AMCOS na kuzihimiza kutumia fursa mbalimbali ikiwamo ya mikopo katika Benki ya Maendeleo ya kilimo," alisema.

Alisema serikali inatambua changamoto kubwa ni ya maghala na inalifanyia kazi.

"Kwa awamu ijayo, tunajipanga na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa kupitia mfuko wa dhamana mbao TADB inashirikiana na benki nyingine za biashara kuwafikia wakulima wengi wa pamba, hivyo tuna lengo la kuwekeza Sh. bilioni 200 hadi Sh. 400 katika hilo," alisema.

**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD**

Property Management, General Auction Services, Debt Collection, Court Broker, Advertising & Commission Agency.

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na **EFC TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD, MAKAO MAKUU – DAR ES SALAAM,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapa chini walipe madeni wanayodaiwa.

Kushindwa kulipa kwa muda huo, tutalazimika kuuza dhamana (mali) zao kwa mnada wa hadhara.

| No | Jina la Mteja | Maelezo ya Dhamana |
|---|---|---|
| 1 | Farida Lutura | Mortgage Residential Licence No.TMK024013, Parcel No. TMK/MBGL/KNY28/106 MBAGALA,KWANYOKA Occupied by Abdallah Said Luongo |
| 2 | Flora Andrea Dachi | Mortgage Residential Licence No. KND029295, Parcel No. KND/KWE/KMZ39/173, Occupied by Flora Andrew Dachi |
| 3 | Tumaini Leoni Msele | Mortgage Residential Licence No. ILA024762, Parcel No. ILA/KPW/KPN16/6A Occupied by Tumaini Leon Mselle. |
| 4 | Salum O Amir | Transfer Of Ownership House Located at Upembani, Mwandege-Mkuranga Owned by Salum Omari Amiri. |
| 5 | Bahati Abdul Mnyanga | Mortgage Residential Licence No. ILA029878, Parcel No. ILA/BUG/MYN3/53A, Located at Buguruni, Occupied by Bahati Abdallah Mnyanga. |
| 6 | Patrick Ndaro | Transfer Ownership of House located at Kivule Street, Kivule Ward in Ilala Municipality Owned By Patrick Peter Ndalu |
| 7 | Charles Yusuph Puka | Transfer Of Ownership House Located at Mji Mpya, Majohe- Ilala Municipality, Owned by Charles Yusuph Puka. |
| | | Transfer Of Ownership House Located at Mji Mpya, Majohe- Ilala Municipality, Owned by Charles Yusuph Puka. |
| 8 | Lucia Ndalo Kambona | Transfer Ownership House Located at Kitunda- Mzinga, Occupied by Lucia Kambona. |
| 9 | Paulo J Muhiri | Legal Mortgage Over Residential Licence No. ILA029742, Parcel No. ILA/KTD/KPNB18/88 Located at KITUNDA, KIPUNGUNI B, ILALA In the name of PAUL JULIAS WANGUBO. |
| 10 | SK Twins Park Hotel | Legal Mortgage over Certificate of Title No. 160894. L.O No 725426, Located on Plot No. 36 Block B, Mangesani Bagamoyo Urban in the name of Kiswigu Mpyanga Bernard. |
| 11 | Mansour Ramadhan Hamdun | Legal Mortgage Over Residential Licence No. KND 030587, Parcel No. KND/SNZ/SINE11/36 Located at SINZA E in the name of Mansour Ramadhan Hamdun |
| | | Motor Vehicle Scania with registration no T784 BHQ in the name of Ramadhan Hamdun Mansour |
| | | Motor Vehicle Toyata Land Cruiser with registration no T993 ARL in the name of Mwanarafa Hadji Konde |
| | | Motor Vehicle Trailer with registration no T763 AZR in the name of Ramadhan Hamdun Mansour |
| 12 | Chacha Nyamuhanga Chacha | Residetial License No ILA 0022, Parcel No. ILA / KTD/KTK49/45 located at Kitunda Kati in the name of Chacha Nyamuhanga Chacha. |
| 13 | Thomas Evarist Batulaki | Residetial License No KND 014671, Parcel No. KND/MBB/MBO17/91 located at Mabibo in the name of Thomas Evarist Batulaki. |
| 14 | Joseph Magarya Buranga | Residetial License No ILA 027834, Parcel No. ILA/KTD/KPNB10/52 located at Kipunguni B in the name of Joseph Buranga Wangi. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji
NUTMEG Auctioneers
Mkwepu Street Road,
Ami Buliding, 3rd Floor.
P.O. BOX 6201
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 -754 497396/0752000695

AU

Mkurugezi Mtendaji
EFC Microfinance Bank
Tanzanite Park,
38 New Bagamoyo
P.O. BOX 11735
DAR ES SALAAM
Tel: +255-22 276021 1/12

215440302

# M'biashara adaiwa kujeruhi kwa risasi

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

POLISI mkoani Arusha, imemtia mbaroni mmiliki wa Kampuni ya Ulinzi ya Bonds Security ya Jiji Arusha, Frank Kessy, kwa tuhuma za kumpiga risasi ya paja Meneja wa Operesheni ya Kampuni ya Ulinzi ya Max Security ya jijini Arusha, Andrew Lubambe.

Imeelezwa kuwa tukio hilo lilitokea Septemba 24, mwaka huu. Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Koka Moita, alisema Kessy baada ya kutenda kosa hilo, alitoweka kusikojulikana na polisi ilikuwa ikimsaka na kufanikiwa kukamatwa Septemba 30, mwaka huu, saa 10 jioni, akiwa mafichoni Usa River nje kidogo ya Jiji la Arusha.

Kamanda Moita alisema mtuhumiwa alifanya kosa hilo Septemba 24, mwaka huu, majira ya saa 6 mchana katika nyumba ya kulala wageni ya Ahadi, iliyopo Elikiuriel wilayani Arumeru, baada ya kugombea lindo na kampuni ya ulinzi ya Max.

Alisema Lubambe alipigwa risasi paja la mguu wa kulia na Kessy na alipelekwa katika hospitali ya Rufani ya Mount Meru kwa matibabu na hali yake kwa sasa inaendelea vizuri, baada ya kuruhusiwa kwenda nyumbani kwake kwake Sakina.

Kamanda Koka alisema hakuna mtu wala kampuni iliyo juu ya sheria na hakuna mtu aliyelishika Jeshi la Polisi mkoani Arusha, na kuwa jeshi hilo halitamvumilia mtu ambaye anavunja sheria.

Alisema polisi itachunguza matukio mengine ya matumizi mabaya ya silaha aliyoyafanya Kessy siku za nyuma, na kama ikibainika kuwa ana matukio mengi, hatua za kisheria zipo na zitafanya kazi.

"Mtu huwezi kumzuia kusema na kama amesema kuwa polisi Arusha imeiweka mfukoni, mimi sijasikia ila polisi iko kwa ajili ya kulinda raia na mali zao, ukivunja sheria hatua kali zinachukuliwa na sio vinginevyo," alisema Moita.

Akizungumzia tukio hilo Mkurugenzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Maxwell, Stanislaus Chaila, alisema kuwa ana imani na Jeshi la Polisi,kwani linafanya kazi yake kwa weledi mkubwa na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote waliohusika katika tukio hilo.

## Mwanga kutatua kero ya maji Arusha waonekana

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (AUWSA), Ruth Koya, amesema tatizo la upungufu wa maji katika Jiji la Arusha na viunga vyake litamalizika ndani ya miezi miwili baada ya kukamilika kwa mradi wa Sh. bilioni 520.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, mkurugenzi huyo alisema mbali na kuwezesha upatikanaji wa majisafi kwa asilimia 100, pia changamoto kubwa ya wananchi kutumia fedha nyingi kunyonya majitaka inaenda kupatiwa ufumbuzi kupitia mradi huo.

Alisema maboresho hayo yote yametokana na Rais John Magufuli kutoa fedha hizo ili warekebishe miundombinu ya maji na kuwezesha wananchi wa mkoa huo wa kitalii kupata majisafi kufikia mwakani.

Koya alisema fedha hizo zimewezesha kuchimbwa kwa visima 56 na kujengwa kwa matangi zaidi ya 10 yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita zaidi ya milioni 10.

Alisema fedha hizo pia zimetumika magari matano ya kisasa ambayo ni maalum kwa ajili ya kusaidia wananchi kuondoa majitaka kwa gharama nafuu kwenye makazi yao.

Alisema mradi huo umeleta mafanikio na mabadiliko makubwa kwa jiji hilo kwa kuwa utawezesha kusambazwa kwa mfumo wa majitaka na kufikia asilimia 30 ya watakaopata huduma hiyo toka asilimia saba za sasa.

Mkurugenzi huyo alisema uboreshaji wa mfumo huo utawezesha wananchi wa mkoa huo kunufaika na upanuzi wa mtandao wa majitaka.

"Lakini wale ambao hawatafikiwa na mtandao huo, watanufaika kwa kutumia magari haya ya kisasa ya kunyonya majitaka ambayo yamenunuliwa kupitia mradi huu na watahudumiwa kwa gharama nafuu, tofauti na wanavyotozwa sasa," alisema.

Alibainisha kuwa kukamilika kwa mradi huo kutawezesha wananchi wa mkoa huo kupata maji lita milioni 200, kiwango ambacho ni zaidi ya mara mbili ya mahitaji yao ya sasa.

Mwenyekiti wa Bodi ya AUWSA, Richard Masika, alisema mradi huo unatekelezwa chini ya ufadhili wa serikali kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na unatarajiwa kukamilika Juni mwakani.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi zaidi ya 827,000 na mradi utakuwa na uwezo wa kutoa maji lita milioni 200 kwa saa.



Mfanyakazi wa mradi wa Nano, Christina Akunay, akichuja maji kwa chujio la Nano lililotokana na utafiti wa Dk. Askwari Hilonga wa Chuo cha Nelson Mandela, kwa ajili ya kuwauzia wateja majisafi na salama katikati ya Jiji la Arusha jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## Fluoride yatesa maelfu Arusha

**Allan Isack, ARUSHA**

ZAIDI ya wakazi 50,000 wa Kata za Oldonyosambu, Oldonyowasi na Engikareti katika Halmashauri za Arusha na Arumeru wanakabiliwa na changamoto ya kutumia maji yenye kiwango kikubwa cha fluoride.

Akizungumza na Nipashe, Diwani wa Kata ya Oldonyosambu, Raymond Larumbe, alisema kwa kipindi kirefu wananchi wa maeneo hayo wameathirika kwa kutumia maji yenye kiwango kikubwa cha madini hayo.

Alisema matumizi ya maji yenye kiwango kikubwa cha fluoride yamekuwa yakisababisha madhara makubwa ikiwa ni pamoja na watoto kupinda miguu, kuoza meno, watoto kuwa na vichwa vikubwa na kupinda mgongo.

Kiongozi huyo alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuzindua mradi mkubwa wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha, ambao aliweka jiwe la msingi Desemba 2, mwaka jana.

Alisema mradi huo ukikamilika utatatua changamoto hiyo kwa wananchi kupata majisafi na salama, akibainisha kuwa hadi sasa wataalamu wa mradi huo wanaendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

"Nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kuokoa uhai wa wananchi wa Lemanda na kwa hili serikali imeonyesha njia ya kuwajali watu wake ambao tangu uhuru wameteseka kwa kutumia maji yenye kiwango kikubwa cha madini ya floride na baadhi yao wameathirika kwa namna tofauti kama kupinda miguu na migongo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Wilson Mahera, alisema katika mikakati yao ya kukabiliana na changamoto hiyo, Januari 4, mwaka huu, waliwasha mtambo maalum uliotolewa na wataalamu kutoka China.

Mtambo huo una uwezo mkubwa wa kupunguza kiwango cha fluoride kilichozidi kwenye maji.

"Mtambo huu niliwasha katika Kijiji cha Lemanda, Kata ya Oldonyosambu ili kusaidia wananchi waondokane na madhara wanayopata na kuwa na ongezeko la watu wenye ulemavu sababu ya kunywa maji haya," alisema.

Alibainisha kuwa mtambo huo una uwezo wa kuchuja maji na kupunguza kiwango cha fluoride kutoka miligramu 18.7 kwa lita moja hadi kufikia miligramu 0.37 kwa lita.

Alisema eneo hilo linakadiriwa kuwa na madini ya fluoride yenye kiwango cha miligramu 19 hadi 20 kwa lita moja ya maji, kiasi ambacho ni kikubwa na kinasababisha madhara kwa watumiaji wa maji hayo.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linabainisha kuwa kiwango kizuri cha fluoride kwenye maji hakipaswi kuzidi miligramu 0.5 kwa lita.

HABARI KITAIFA

# Mtazamo hasi kikwazo wanawake kuwania uongozi

**Na Mwandishi Wetu**

JAMII bado ina mtazamo hasi kuhusu wanawake kushiriki katika kugombea nafasi za uongozi na kuwa viongozi wa kisiasa katika ngazi mbalimbali kuanzia shehia, wadi, jimbo hadi taifa.

Changamoto kadhaa zimeibuliwa katika mikutano ya kijamii iliyofanywa na Chama cha Wanahabari wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) kwa kushirikiana na wanaume wa mabadiliko katika shehia 31, ambapo 19 shehia za Unguja na 12 za Pemba.

Kaimu Mkurugenzi wa Tamwa-Zanzibar, Asha Abdi Makame, amesema katika mikutano ya uhamasishaji iliyofanywa na kikosi kazi cha wanaume wa mabadiliko katika wilaya zote 11 za Unguja na Pemba, wanawake wamekuwa wakijitokeza kwa wingi katika mikutano hiyo na kuelezea mambo yanayowakwaza katika kuzifikia ngazi za uongozi au kuwa viongozi katika jamii zao.

Pamoja na mambo mengine, imani za kishirikina zinachukua nafasi kubwa katika kuwavunja moyo wanawake wengi wasijitokeze kugombea nafasi za uongozi.

Mwandiwe Makame wa Kaskazini 'A' Unguja alisema alijaribu kugombea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na akatishwa na mgombea mwenziwe ambaye alimwambia kama hajipendi aendelee na uamuzi wake wa kugombea nafasi ya uongozi katika jimbo.

"Kama vile vitisho havitoshi, walinijia wakubwa wa jimbo na kunishauri kuwa nijitoe... mimi niliendelea na mipango yangu ya kugombea, lakini niliangushwa katika hatua za awali na hata hivyo, sikusalimika kwani hali yangu ya afya mpaka leo ni tete, miguu yangu imeathirika, siwezi kutembea, tatizo halijulikani, hospitali hawaoni ugonjwa," alisema.

Mwanamke mwingine aliyewahi kujitokeza kugombea nafasi ya uongozi katika ngazi ya wilaya, anasema jambo jingine linalowakwaza ni rushwa.

"Wagombea wenzetu wengi huwa na uwezo wa kiuchumi, hivyo kugawa fedha kwa wapigakura kuanzia kura za ndani ya chama, sasa sisi wengine ambao kipato chetu ni kidogo huwa ni vigumu kupita," alisema Bahati Suleiman, mkazi wa Wilaya ya Kati Unguja.

Abdi anasema hata hivyo, yapo matumaini yaliyopatikana kutokana na mpango huo wa mwaka mmoja wa kuihamasisha jamii kubadili mitazamo na kumwona mwanamke kama mgombea halali na kumpa nafasi ya kugombea na kushinda. Alisema wanawake wenyewe wameona wakati umefika wa kupeana moyo, kusaidiana na kupigiana kura pale mmoja wao atakaposimama kugombea nafasi yoyote ya uongozi na wafanye hivyo bila kujali chama alichogombea.

Huzaima Ali Hamdani, kutoka Chadema anasema "Tumegundua ipo haja ya kuwaunga mkono wanawake wenzetu watakaposimama kwa sababu ni wazi kuwa ajenda ya maendeleo haina chama na wanawake wana uwezo mkubwa na utashi wa kuisukuma ajenda hiyo mbele."

Naye Maryam Saleh kutoka Chauma Wilaya ya Chakechake, alizungumzia suala la gharama kubwa za kuchukua fomu ya kugombea jambo ambalo linawarudisha nyuma kwani wao vitega uchumi vyao ni vidogo hivyo inakua kikwazo kumiliki pesa hizo.

Katika uchaguzi uliopita kwa baadhi ya vyama fomu za kugombea zilifikia hadi Sh. 200,000. Abdi anasema vyama vya siasa navyo vina mchango mkubwa katika kukwamisha wanawake kushika nafasi za uongozi hasa pale vinapoona kuwa kumsimamisha mwanamke kugombea wakati vyama vingine vimesimamisha wanaume ni sawa na kupanga kulipoteza jimbo, ingawa ipo mifano ya wanawake waliogombea majimboni na wakashinda.

Tamwa inaishauri jamii na vyama vya siasa kubadili mitazamo hasi dhidi ya wanawake katika kugombea nafasi za uongozi kwa sababu uhalisia unaonyesha kuwa wanawake wanapopata nafasi za uongozi hufanya kazi vizuri zaidi kuliko wanaume na husimamia amani na utulivu.



Wakili Hamza Jabir (kulia), akiongea na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampeni ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambayo imeratibiwa na kampuni ya mawakili ya Avis Legal. Kushoto ni Wakili Henry Mwinuka na Miss Land Scape Anita Mlay. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waililia serikali kituo cha afya

**Na Ibrahim Yassin, MBEYA**

WANANCHI wa kata za Tembela na Mwasanga katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameiomba serikali kuangalia namna ya kuwajengea kituo cha afya ili kuwaondolea kero ya kusafiri umbali mrefu wa kilometa 10 kufuata huduma za matibabu Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Kata za Tembela na Mwasanga zenye zaidi ya wakazi elfu 600 zipo pembezoni mwa mji wa Jiji la Mbeya ambao wanakabiliwa na changamoto lukuki ikiwamo ukosefu wa vituo vya kutolea tiba, hivyo kuwalazimu kutembea kilometa 10 kusaka huduma hiyo Mbeya Mjini.

Faida Mkola, mkazi wa kata ya Tembele, alisema toka Tanzania ipate Uhuru hawajawahi kuwa na kituo cha kutolea tiba hivyo wanaiomba serikali kupitia idara ya afya kuona namna ya kuweka vituo vya kutolea tiba ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Happy Sanga, mkazi wa kata ya Mwasanga, alisema kwa muda mrefu kulianzishwa ujenzi wa kituo cha kutolea tiba, lakini ujenzi huo umekuwa ukisuasua hali ambayo inawafanya kupata shida ya matibabu huku mama wajawazito wengi wao wakijifungulia njiani wakati wakielekea katika vituo vilivyopo Mbeya Mjini.

Bertha Mpogole, mkazi wa Tembela, alisema wanaomba serikali iwasaidie kukamilisha ujenzi huo kwani asimilia kubwa wanaopata shida ya matibabu ni watoto, wanawake na wazee na kwamba endapo ujenzi utakamilika wataondokana na kadhia hiyo ya kutembea umbali mrefu kusaka tiba.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alifanya ziara katika kata hiyo na kutoa maagizo ya serikali katika kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo na kwamba ni aibu na dhambi kubwa wananchi kukosa huduma za afya.

**Faida Mkola, mkazi wa kata ya Tembele, alisema toka Tanzania ipate Uhuru hawajawahi kuwa na kituo cha kutolea tiba hivyo wanaiomba serikali kupitia idara ya afya kuona namna ya kuweka vituo vya kutolea tiba ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.**

# Wakumbushwa mikopo ya NMB

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

BENKI ya NMB imewataka wafanyabiashara nchini kuendelea kulipa mikopo yao kwa benki hiyo pamoja na kuwa mabalozi wake kwa kuwaleta wateja wengine.

Rai hiyo imetolewa na Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola, wakati wa kongamano la NMB Business Club Iringa kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo (MSMEs) lililofanyika mjini hapa.

Alisema wafanyabiashara wanatakiwa kujenga nidhamu ya fedha kwenye biashara zao pamoja na kuendelea kulipa mikopo ili benki iendelee kutoa huduma mbalimabli ikiwamo mikopo kwa wengine.

NMB Kanda ya Nyanda za Juu inajumuisha matawi 30 kwenye mikoa sita ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

Chilongola alisema NMB Business Clubs, zina malengo ya kuwafikia jamii ya wafanyabiashara wadogo na wakati (MSMEs), ambao kwa sasa inajumuisha wafanyabiashara zaidi ya 200,000 wakiwa wateja wa NMB nchi nzima.

Alisema mikopo yao inafikia thamani ya Sh. bilioni 600 na kuongeza kuwa NMB Business Club ni mahali mwafaka pa kuelimisha wafanyabiashara juu ya masuala mbalimbali kuhusu biashara zao.

Aidha, alisema NMB ina business Clubs 36 nchi nzima, katika hizo kwenye kanda zipo saba yaani Mpanda, Sumbawanga, Tunduma, Mbeya, Njombe, Mafinga na Iringa.

"Kila moja ikiwa na wanachama kati ya 150 mpaka 300 wamekuwa wakifaidika na mafunzo mbalimbali kutoka NMB yanayohusu bidhaa zinazotolewa kwao na benki kama vile jinsi ya kutunza vitabu vya mahesabu, elimu ya masoko na pia elimu ya mlipa kodi," alisema Chilongola.

Alisema benki hiyo ni miongoni mwa benki inayoongoza kwa wigo wa huduma za kibenki kwa kuwa wana matawi zaidi ya 229 nchi nzima, mawakala zaidi ya 6,800 na mashine za ATM zaidi ya 800.

Mmoja wa wanachama wa NMB Business Club Iringa, Jesca Msambatavangu, alishukuru benki hiyo kwa kuanzisha business clubs ambapo kupitia clubs hizo wanapata mafunzo ya ujasiriamali.

Alisema kuwa ili kuhakikisha mtiririko wa fedha kwenye biashara, ni lazima wafanyabiasha wajenge nidhamu ya fedha kwenye biashara. "Unahitaji kuweka malengo ya biashara yenye uhalisia kufuatilia maendeleo ya biashara yako, changanua changamoto zinazotokea na kuzifanyia kazi kwa usahihi," alisema Msambatavangu.

Alisema kuwa kimsingi nidhamu ya fedha ni lazima kuhakikisha unatengezea faida zaidi na kupunguza matumizi yasio na ulazima pamoja na kuweka akiba.

# Msako watoa rushwa hadi nyumba za ibada

**Na Moshi Lusonzo**

TAASISI ya Kuzia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema itawakamata watu watakaotumia nyumba za ibada kutoa rushwa kwa waumini kwa lengo la kushawishi kupata kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba.

Akizungumza katika mkutano mkuu wa 50 wa Jumuiya ya Kiislam ya Ahmadia jijini Dare s Salaam jana, Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Ilala, Christopher Myuva, alisema taasisi hiyo imejiandaa kupambana na watu wanaotumia nyumba za ibada kuendesha kampeni zinazoambatana na vitendo vya rushwa na kuwaonya endapo watabainika, watakamatwa mara moja.

Mkutano huo wa siku tatu umewajumuisha waumini zaidi ya 6,000 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani pamoja na nchi zingine kutoka Kenya, Uganda, Msumbuji na Pakistani.

Myuva ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, alisema wameshazungumza na viongozi wa dini zote, na wamekubaliana kuhakikisha hakuna watu watakaotumia nyumba hizo vibaya wakati wa uchaguzi.

"Takukuru ina uhusiano mzuri na taasisi za dini, tumewaambia wenzetu watusaidie kuwaelimisha waumini wao kwa sababu hatutakubali watumie nyumba za ibada kushawishi watu kwa kutoa rushwa," alisema Myuva.

Alisema katika muda wote wa kampeni na uchaguzi, kila Mtanzania hanabudi kuhakikisha anachagua kiongozi kutokana na uadilifu wake na si vinginevyo.

"Vitabu vyote vya dini vinapinga suala la rushwa kwa sababu humwondolea mtu ubinadamu wake, naamini kwa kutumia hadhara hii ujumbe huu utafika haraka ili kila mtu afahamu," aliongeza.

Naye Katibu Mkuu wa Ahmadia, Seif Hassan Nakuchima, alisema anakubaliana na hatua inayochukuliwa na Takukuru kwa sababu viongozi bora wanachaguliwa kwa uwezo wa Mungu na kupitia kura halali.

"Waumini wa Kiislamu tunaamini rushwa ni jambo la dhambi na lenye kumkasirisha Mungu, tutaungana na Takukuru kuhakikisha kila muumini anapata haki yake ya kuchagua au kuchaguliwa bila ushawishi wowote wa mali," alisema Nakuchima.

Aliyekuwa Amir wa Jumuiya hiyo, Sheikh Muzaffar Ahmad Durann, alisema mkutano huo una madhumuni ya kuwaweka pamoja waumini kwa ajili ya kutafakari maneno ya Mungu.



Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye (mbele), akitoka kukagua mnara wa kijiji cha Mlaga, Kata ya Nyampande katika ziara ya kukagua upatikanaji wa huduma za mawasiliano, wilayani Sengerema mkoani Mwanza jana. **PICHA: WUUM**

# Uchaguzi mitaa kuwapeleka mikoani vigogo wa CUF

**Na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI wakuu wa kitaifa wa Chama cha Wananchi (CUF), watafanya ziara za mikoani kwa lengo la maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa.

Serikali imeshatangaza kwamba uchaguzi huo utafanyika Novemba 24, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Habari wa Chama hicho, Abdul Kambaya, alipozungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam juzi.

Kambaya alisema kwamba Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahimu Lipumba, anatarajia kuanza ziara leo katika mikoa ya Tabora, Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Geita, Kagera, Mara na Kigoma.

Kambaya alisema Makamu Mwenyekiti Bara wa chama hicho, Maftaha Nachuma, naye atakuwa akifanya ziara katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma wakati Naibu Katibu Mkuu, Manfalena Sakaya, atakuwa akifanya ziara katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Manyara na Singida.

Katika hatua nyingine, CUF) imemshangaa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola kuhusiana na kauli yake aliyoitoa hivi karibuni kwamba hajawahi kupata malalamiko kutoka kwa chama chochote cha siasa kuhusiana na kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara.

Kambaya alisema kauli ya Lugola inashangaza kwa sababu ni kipindi kirefu sasa tangu vyama hivyo vianze kulipigia kelele suala ya kuzuiwa kufanya mikutano.

"Ni muda mrefu sasa tangu tuanze kupigia kelele juu ya hili zuio la vyama vya siasa kufanya mikutano na utekelezaji wa zuio hili unasimamiwa na Jeshi la Polisi nchi nzima, halafu tena jeshi hilo hilo ndilo linadai halijawahi kupata malalamiko. Hapa panatia shaka juu ya utendaji baina ya Waziri na Jeshi la Polisi lililo chini yake," alisema Kambaya.

"Hivi karibuni tumemsikia Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, akirudia tena kutamka kwamba hajawahi kupata malalamiko rasmi kutoka kwenye chama chochote juu ya kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara. Yapo matukio mengi ya wazi ya vyama vya upinzani kulalamika juu ya kuzuiwa na Jeshi la Polisi kufanya mikutano hiyo kwa madai ya kuwapo kwa zuio la serikali."

Mbali na hilo, katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, chama hicho kililitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha linaimarisha ulinzi kwa kuzingatia usawa.

Pia kiliiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuondoa hitajio la nambari ya simu katika kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpigakura kwa kuwa si wapigakura wote wenye sifa ya kumiliki nambari hiyo.

## NBC yahamasisha uwekaji wa akiba

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC imezindua kampeni yake maalum inayofahamika kwa jina la 'Ibuka Kidedea na NBC', ikilenga kuhamasisha na kushawishi wateja wake na jamii kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba kupitia Akaunti ya Malengo ya benki hiyo, ili kufanikisha malengo yao ya muda mfupi na muda mrefu.

Kampeni hiyo ya miezi sita imetajwa kuwa inalenga kuwafikia maelfu ya Watanzania ambao bado hawajafikiwa na huduma za kibenki kwa kuwa inahusisha namna rahisi zaidi ya kufungua akaunti hizo.

Akizungumza wakati wa warsha fupi ya uzinduzi jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi wateja wa Rejareja wa benki hiyo, Benjamin Nkaka, alisema kampeni hiyo inalenga kuleta mabadiliko kwenye mtazamo wa uhifadhi wa akiba miongoni mwa Watanzania kutoka kuhifadhi pesa majumbani na badala yake wazihifadhi kupitia benki hiyo, huku wakifurahia faida.

"Ni wakati mwafaka kwa Watanzania mmoja mmoja au vikundi kuacha kuhifadhi fedha zao kwenye vibubu au namna nyingine yoyote ile majumbani mwao kwa kuwa njia hizo si salama kwao na kiuchumi. Badala yake wanaweza kuhifadhi pesa zao kupitia akaunti ya Malengo ya NBC ambayo inawahakikishia usalama wa fedha zao huku pia wakifurahia faida zinazotolewa na benki," alisema.

Alizitaja faida zitokanazo na akaunti hiyo ambazo mbali na kuokoa pesa za mteja, pia inaweza kubadilika kuwa amana kulingana na mapato ya mteja. Pia inatoa fursa kwa mteja kuweka akiba hiyo kupitia mashine za kuwekea fedha (ATM) za benki hiyo zinazopatikana kote nchini, kwenye matawi na kupitia mawakala wa huduma za benki hiyo.

"Habari njema zaidi ni kuwa hakutakuwa na makato ya mwezi, huku pia mteja akipata riba ya hadi kufikia asilimia 7 kwa mwezi," aliongeza.

Aidha, Nkaka alibainisha kuwa kampeni hiyo, inawalenga wateja wote wapya wa benki hiyo pamoja na wale ambao tayari wanamiliki akaunti ya malengo ya benki hiyo, huku akisisitiza kuwa walengwa ni mtu mmoja mmoja na si kampuni au taasisi.

Kwa upande wa zawadi kuu, alisema wateja ambao watakuwa na ongezeko la akiba la Sh.1,000,000 katika kipindi cha kampeni hiyo watapata tiketi ya kuingia kwenye droo itayowapa nafasi ya kushinda pikipiki ya kubebea mizigo ya magurudumu matatu kwa washindi watatu.

"Kadri mteja anavyozidi kujiwekea akiba ndivyo anavyojiongezea nafasi ya kushinda kiasi cha Sh. 500,000 na kupata uwezekano mara tano zaidi wa yeye kushinda dhidi ya atakayejiwekea akiba ya Sh. 100,000 tu.

HABARI KITAIFA

# Aagizwa elimu kichaa mbwa

Na Shaban Njia, KAHAMA

WANANCHI wilayani Kahama, wamemtaka Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Emmanuel Nangay, kutoa elimu ya kinga ya kichaa cha mbwa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kutokana na wao kuwa karibu na mbwa hao.

Waliyabainisha hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya chanjo ya mbwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa (RABIES) yaliyofanyika katika viwanja wa magereza na kusema, asilimia kubwa ya wanaocheza na mbwa ni watoto wadogo ambao ni wanafunzi.

Mmoja wa wananchi hao, Abdallah Jafari, alisema endapo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari watapatiwa elimu ya chanjo ya mbwa dhidi ya kichaa, wataweza kuwa mabalozi kwa kuwasisitiza wazazi kuwapatia chanzo cha mbwa na paka.

Naye Fatuma Issa, alisema mbwa anapokuwa na kicha mtoto mdogo hawezi kutambua na anaweza akamsogelea na kumng'ata na akashindwa kutoa taarifa na ikasababisha kuumwa kwa kichaa cha mbwa na kupoteza maisha yake.

Kwa upande wake, Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Emmanuel Nangay, ni kweli elimu ya kinga dhidi ya kichaa cha mbwa inatakiwa kutolewa shuleni na hii ni kutokana na asilimia kubwa ya wanaokuwa karibu na mbwa ni watoto ambao ni wanafunzi.

Alisema kuwa, ugonjwa wa kichaa cha mbwa hauna tiba ila unakinga na unaua kwa muda wa siku saba endapo mtu aliyeumwa na mbwa akishindwa kupatia kinga hiyo, na kuwataka wananchi kutoa taarifa pindi watakapombaini mtu aliyeumwa na mbwa.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la kutetea hasa na ustawi wa wanyama Tanzania (TAPO), Yohana Kashililah, alisema wananchi walioko pembezoni mwa mji hawana elimu ya utambuzi wa kchaa cha mbwa ukilinganisha na wanaoishi mjini.

# Mashinji ahamasisha watakaotaka kugombea

Na Ahmed Makongo, BUNDA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimewataka wanachama wake kujitokeza kwa wingi na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mbali na kujitokeza, wametakiwa kuchagua viongozi wanaokubalika ndani ya jamii na wale ambao watakijenga na kukilinda chama hicho.

Hayo yalielezwa jana na Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, kwenye mkutano wa kuchagua viongozi mbalimbali, wa chama hicho ngazi ya mkoa wa Mara.

Dk. Mashinji aliwataka wanachama kujitokeza kwa wingi na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu, pamoja na uchaguzi mkuu mwakani.

Alisema Chadema ni chama imara ambacho kinajali demokrasia, hivyo wanachama wake wote wenye sifa za kuwa viongozi wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali.

Aidha, Dk. Mashinji aliwapatia salamu za Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, kwamba anawatakia uchaguzi mwema wa mkoa huo na kwamba yuko pamoja nao, ambapo anawataka waendelee kukijenga chama hicho.

"Wanachama wenzangu jitokezeni kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi unaokuja wa serikali za mitaa pia katika uchaguzi mkuu...Chadema ni chama imara na ni chama kilichoanzishwa na watu makini, wala msibabaishwe na mtu yeyote," alisema Mashinji na kuongeza kuwa wachague viongozi wanaokwenda na kasi ya Chadema.

Aidha, alisema uchaguzi wa chama hicho ngazi ya taifa utafanyika D esemba mwaka huu na kwamba kuelekea katika uchaguzi huo kuna mambo manne ya msingi. La kwanza ni chama hicho kubaki imara, la pili ni kupata wagombea, la tatu kuwa na ajenda za msingi na la mwisho kuwa na fedha, ambapo chama hicho kuelekea uchaguzi huo kitahakikisha kinajipanga ipasavyo na kitahakikisha uchaguzi huo unafanyika.

Mwenyekiti wa Kanda ya Serengeti ambaye pia ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, alisema chama hicho kina mkakati mkubwa, ambapo kikipata fursa ya kuchukua dola mwaka 2020, kitainua uchumi wa wananchi kwani kwa sasa maisha yamekuwa magumu kwa kila mwananchi.

"Ebu tujiulize tangu CCM imeingia madarakani ni wananchi wangapi wameondokana na umaskini...pamba ya wakulima wameichukua bila kuwalipa, kuna watu wanakula mlo mmoja kwa siku, tuna ajenda nyingi za kuishambulia serikali ya CCM katika uchaguzi wa serikali za mitaa na katika uchaguzi mkuu wa 2020," alisema Heche.

Aidha, alisema wanaokihama chama hicho ni sawa na kuuza utu wao na kusema chama hicho bado kiko imara na kitahakikisha kinachukua dola mwaka 2020, kwamba wanachama wote washikamane ili azima hiyo iweze kutimia.

Katika uchaguzi huo wa ngazi ya Mkoa wa Mara, wajumbe walimchagua, Lucas Ngoto, kuwa mwenyekiti wa chama hicho mkoa wa Mara, baada ya kupata kura 52 dhidi ya mpinzani wake Kinga Haile, aliyepata kura 48, ambapo Katibu wa chama hicho mkoani Mara, amechaguliwa ni Daniel Ayot, aliyepata kura 61, baada ya kumshinda, Fikiri Malenge aliyeambulia kura 36.

Wakati huo huo, baadhi ya wanachama wa chama hicho akiwamo Mbunge wa Bunda Mjini Bulaya, wamekabidhiwa vyeti vya utambuzi wa ujasiri wao kwani pamoja na kukamatwa na kupelekwa mahabusu bado wanakitumikia chama hicho bila kurudi nyuma.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Mafia, Mbaraka Dau, katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mafia, alipoanza ziara yake ya siku mbili wilayani humo mkoani Pwani jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Shaib Nnenduma. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wavuvi sasa wanufaika na mikopo

Na Neema Emmanuel, MWANZA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, amesema wizara hiyo imeweka mkakati kufikia Novemba mwaka huu, baadhi ya vyama vya ushirika wa wavuvi ambavyo vitakuwa tayari vimeisha jiunga vitapatiwa mkopo.

Ulega alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa ili wavuvi waweze kunufaika na sera ya serikali ya vyama vya ushirika, wizara hiyo itaanza kuvipatia mikopo vyama vya ushirika wa wavuvi ambavyo vitakuwa tayari vimeanzishwa na kusajiliwa.

"Mvuvi mmoja mmoja hakopesheki ingawa wapo baadhi wanaokopesheka ila walio wengi hawakopesheki kwa sababu ya kutokuwa na dhamana itakayomfanya aaminike ikiwamo hati ya mali isiyo hamishika, hivyo wakiunda ushirika ndio unakuwa mdhamini, mkakati wetu siye wizara ifikapo Novemba mwaka huu ni kuvipa mkopo baadhi ya vyama vya ushirika vitakavyokuwa tayari vimeanzishwa na kusajiliwa," alisema Ulega.

Aidha alisema, hivi juzi ametoka kuhamasisha na aliwasisitiza maofisa uvuvi wote kuwa mwelekeo kwa sasa ni vyama vya ushirika kuvipa nguvu kwa kuvihamasisha, hivyo hata hao wavuvi wa mwalo wa Butuja kama wapo tayari waende kuwapa elimu na kuanzisha.

Mwenyekiti wa Utunzaji wa Viumbe Hai ndani ya mita 60 mwambao mwa ziwa (BMU) ya Mwalo wa Butuja, Dickson Maila, alisema, wavuvi wa ndoano bado wanachangamoto kubwa ya mitaji hivyo kwa kulitambua hilo wameanzisha umoja wao ambao wanatarajia kufikia mwezi ujao watakuwa wamekamilisha kiasi cha Sh. milioni 5 kwa ajili ya kuanzisha na kuweza kusajili ushirika wao wa wavuvi Butuja.

Mmoja wa wavuvi kutoka mwalo wa Butuja, Cleoper Magessa, alisema wanaomba maofisa uvuvi kuwatembelea katika mwalo wao na kuwaelimisha kuhusu faida ya ushirika, changamoto na hasara, kwani anaimani wakielewa wataweza kuanzisha na kusajiliwa ushirika wao hivyo kuwa wametekeleza kwa vitendo sera ya serikali.

# Wafa kwa kupigwa radi wakinywa pombe kilabuni

**Na Gurian Adolf, NKASI**

WATU wanne wamekufa papo hapo baada ya kupigwa na radi wakiwa kilabuni wanakunywa pombe na wengine saba kujeruhiwa katika kitongoji cha Nkata kijiji cha Kate, Nkasi mkoani Rukwa.

Mwenyekiti wa kijiji cha Kate, Wilbroad Feluzi, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12:30 jioni kijijini hapo.

Alisema watu hao wakiwa wanaendelea kunywa pombe katika kilabu hicho, ghafla ilipiga radi katika eneo hilo hali iliyosababisha watu wengi kuanguka na kupoteza fahamu.

Baada ya kuwafanyia uchunguzi watu waliokuwa katika kilabu hicho, alisema ilibainika wanne kati yao wamefariki dunia papo hapo na wengine kujeruhiwa na kupelekwa kwenye zahanati ya Kanisa Katoliki iliyoko kijijini hapo. Baada ya kufikisha hapo kwa huduma, wengine walizinduka na kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Mwenyekiti huyo aliwataja waliofariki dunia kuwa ni John Sumuni (31), Akleo Feluzi (45), Boniface Fundililwa (38) na Anastazia Njali (48) wote wakazi wa kijiji hicho. Mganga Mfawidhi wa zahanati ya Kate Mission, Elly Joseph, alikiri kuwapokea majeruhi zaidi ya 10 na baada ya kuwapatia huduma ya kwanza, wengi wao waliruhusiwa kurudi nyumbani na wanne waliokuwa mahututi walibaki na wanaendelea na matibabu.

Alisema kati ya majeruhi hao waliobaki, watatu wanaendelea vizuri isipokuwa mmoja ambaye akipata kidonda mguuni, hivyo hali yake si nzuri. Alisema wagonjwa wengine wanaoendelea vizuri, wanaweza kuruhusiwa wakati wowote iwapo hali zao zitaendelea kuimarika.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kuthibitisha kuwa watu wanne ndio waliopoteza maisha na kuwa wako kwenye kikao baada ya hapo yeye na viongozi wenzake watakwenda katika kijiji hicho kuwajulia hali majeruhi na kushiriki mazishi ya watu waliopoteza maisha.

Alisema kuwa baada ya hapo, kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, atatoa ripoti zaidi juu ya tukio hilo.



Mafundi wa kampuni ya CCECC wakiwa wameifunga barabara ya kwenda Tandale Sokoni katika Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam wikiendi, kwa ajili ya kukarabati sehemu ya barabara hiyo kwa kiwango cha lami. **PICHA: JOHN BADI**

# Wahukumiwa kulipa mil. 101/- kukiri kosa utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA Magdalena Uhwello na Halima Nsubuga, wamehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 101 au kwenda jela miaka 21 baada ya kukiri makosa ya kuendesha biashara ya upatu isivyo halali na kutakatisha fedha.

Kadhalika mahakama hiyo imesema Dola za Marekani 388,000 zilizopo katika akaunti za washtakiwa Equit benki Tanzania Ltd na Uganda, kuwa mali ya serikali.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo, jana.

Awali, washtakiwa walisomewa mashtaka yao kwamba Aprili Mosi, 2017 na Juni 30, 2017 na kudaiwa kukusanya fedha za upatu kutoka kwa watu mbalimbali ambazo walikuwa wakichangia kwa kuwaahidi kuwapatia faida watakayopata.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa siku na tarehe ya tukio la kwanza washtakiwa walitakatisha fedha hizo huku wakijua ni zao la upatu. Washtakiwa walikiri makosa hayo.

Hakimu alisema kwa kuwa washtakiwa wamekiri makosa yao wenyewe mahakama yake inawatia hatiani.

Wankyo alidai kuwa upande wa Jamhuri unaiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa washtakiwa.

Pia alidai kuwa Jamhuri inaomba mahakama kutoa amri ya kutaifisha Dola za Marekani zilizopo kwenye akaunti za washtakiwa kuwa mali ya serikali.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Agostine Shio, aliiomba mahakama iwaonee huruma washtakiwa ni wanawake wenye familia wanategemewa na watoto wao.

Aliiomba mahakama izingatie washtakiwa kukiri makosa yao wameipunguzia gharama na ni wakosaji wa mara ya kwanza. "Mheshimiwa hakimu tunaiomba mahakama itoe adhabu nafuu kwa washtakiwa ikiwamo kulipa faini kwa makosa yote, pia hawana pingamizi kuhusu serikali kutaifisha fedha zilizopo kwenye akaunti zao," alidai Shio.

Pia alisema utetezi unaiomba mahakama adhabu itakayotolewa iwe ndani ya uwezo wao.

Akisoma adhabu hiyo, Hakimu Mwaikambo alisema kwa kosa la kwanza washtakiwa watalipa faini ya Sh. milioni moja au kwenda jela mwaka mmoja.

"Washtakiwa mtalipa faini ya Sh. milioni 100 kwa kosa la pili au mkishindwa mtakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 20 kwa kosa la kutakatisha fedha," alisema Hakimu Mwaikambo.

# Afya ya Kabendera yaimarika

**Na Hellen Mwango**

MWANDISHI wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera, anayebakiliwa kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kutakatisha fedha wa zaidi ya Sh. milioni 100, ameiambia mahakama kuwa anaendelea vizuri na matibabu na kwamba ameanza kutumia dawa.

Kabendera alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustine Rwizile, aliyemhoji kuhusu maendeleo ya afya yake kwa sasa.

Mshtakiwa alidai ameanza kutumia dawa kwa hiyo matibabu yanaendelea.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado unaendelea.

Wakili wa utetezi, Jebra Kambole, alidai kuwa mshtakiwa yuko mahabusu miezi miwili sasa na kwamba afya yake bado haijaimarika, hivyo waharakishe upelelezi huo.

Kutokana na ombi la Wakili Kambole, Wankyo alidai kuwa upande wa utetezi wawe na uvumilivu na kwamba hoja zao zinafanyiwa kazi.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba 11, mwaka huu, na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019 katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Pia anadaiwa bila kuwa na sababu za msingi kisheria alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173, 247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Katika shtaka la tatu anadaiwa mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 173.2 wakati akijua kuwa fedha hizo ni za kutakatisha na zao la makosa tangulizi ya kukwepa kodi na kujihusisha na genge la uhalifu.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

**Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019 katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.**



Ukurasa 14

**Kwa somo hili, Jafo hataki yajirudie ya mwaka 2014**

Democratic waungana kumchunguza Trump




Ukurasa 20



Ukurasa 18

**Rwanda inavyojijengea heshima kupitia wahamiaji toka Libya**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 2, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 15

**Marekani na kigugumizi kupigwa visima vya mafuta Saudi Arabia**

# Umakini muhimu tamu, chungu mitandao ya kijamii katika siasa

• Hususani wakati tukielekea katika uchaguzi ujao

**Na Fransisko Mpangala**

MWISHONI mwa mwaka jana simu yangu ya 'smartphone' ilizima ghafla na kushindwa kuwaka tena.

Kwa kuwa ilitokea ghafla sana, ilinichukua miezi miwili kujipanga upya ili kununua nyingine.

Kitendo cha kukosa simu hiyo kwa miezi miwili kilikuwa pigo kubwa kwangu kwani, matumizi ya simu ya kawaida (tochi) ambayo hayana huduma ya intaneti yalininyima fursa ya kupata habari na mijadala mingi ya kisiasa kupitia mitandao ya kijamii kama nilivyozoea.

Hakika nimekuja kuithamini sana mitandao ya kijamii, hasa kipindi kile cha miezi miwili niliyoshindwa kuipata huduma yake (wanasema ukose kitu ndio ujue umuhimu wake).

Kushindwa kuitumia mitandao hii kulinifanya kuitazama

INAENDELEA UK.16



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi, Isack Kamwelwe. **PICHA: MTANDAO**

**Kwa nini CIA haikugundua shambulio la Septemba 11?** Ukurasa 19

# Kwa somo hili, Jafo hataki yajirudie ya mwaka 2014

• Ni katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

NOVEMBA 24, mwaka huu, Watanzania wanatarajia kwenda kwenye vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa ikiwa ni miaka mitano tangu kufanyika kwa ule wa mwaka 2014.

Uchaguzi huo kwa kawaida huwa unahusisha nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo ya mwenyekiti na wajumbe sita wa serikali ya mitaa, huku kukiwa pia na nafasi ya viti maalumu kwa upande wa wanawake. Kwa upande wa vijiji, ni kwamba nafasi zitakazowaniwa ni ya mwenyekiti wa kijiji, wenyeviti wa vitongoji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na wajumbe wa viti maalumu wanawake.

Wakati nchi ikielekea kwenye uchaguzi huo, serikali inawaonya wakurugenzi wa halmashauri na kuwataka wajiandae kusimamia kikamilifu uchaguzi huo ili usikumbwe na hujuma za aina yoyote.

Uchaguzi huo utakaotumia zaidi ya Sh. bilioni 82, na inaonekana serikali haitaki kurudia makosa yaliyojitokeza katika uchaguzi wa mwaka 2014, ambayo yalidaiwa kufanywa na baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri.

Katika uchaguzi ujao, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, anawataka wakurugenzi wa halmashauri kutohujumu mchakato mzima wa uchaguzi huo.

> Ni muhimu kufanya hivyo kwa kuzingatia kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaweka wazi kuwa kila mtu ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

**UCHAGUZI WA 2014**

Baada ya uchaguzi huo, serikali ilichukua hatua kali kwa wakurugenzi 17 wa halmashauri mbalimbali nchini, huku sita kati yao uteuzi wao ukitenguliwa, watano kusimamishwa kazi, watatu kupewa onyo kali na watatu kupewa onyo.

Wote hao walipewa adhabu hiyo kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wao katika kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji uliofanyika Desemba mwaka 2014.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wa wakati huo, Hawa Ghasia ndiye aliyetangaza hayo jijini Dar es Salaam akiwatuhumu wakurugenzi hao.

Kwamba serikali ilichukua uamuzi huo kutokana na wakurugenzi hao kusababisha kutokea kwa kasoro na kuvurugika kwa uchaguzi huo hadi kuahirishwa katika baadhi ya maeneo.

Ghasia aliuambia umma wa Watanzania kuwa ofisi yake ilitimiza wajibu wa kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa ukamilifu kwa kutoa miongozo na mafunzo kwa watendaji wa halmashauri.

Mbali na hayo, akabainisha kuwa ofisi yake ilitimiza wajibu ukiwamo kuwezesha kwa fedha mikoa na halmashauri ili kugharamia maandalizi muhimu, ikiwa ni pamoja na kuandaa vifaa na karatasi za kupigia kura.

Ghasia alikaririwa wakati huo akisema: "Kimsingi kama maelekezo, miongozo na mafunzo yaliyotolewa yangezingatiwa na kila mmoja, uchaguzi ungefanyika vizuri nchini kote...wakurugenzi walikuwa wanawajibika kutambua nafasi zao kama wasimamizi wakuu katika kufanikisha uchaguzi huo."

Kwamba kutokana na ripoti walizopokea kuhusu masuala yaliyojitokeza katika uchaguzi huo, ni dhahiri wakurugenzi wa halmashauri zenye dosari, walionyesha udhaifu mkubwa katika kutekeleza jukumu la usimamizi wa uchaguzi, ambalo ni moja ya majukumu ya ukurugenzi. Alisema, walitenda makosa yaliyowaondolea sifa za kuwa wakurugenzi, ikiwamo kuchelewa kuandaa vifaa vya kupigia kura na kukosa umakini katika kuandaa vifaa, hasa karatasi za kupigia kura na hivyo kuwa na makosa.

Makosa mengine yaliyotajwa na Ghasia yalikuwa ni kuchelewa kupeleka vifaa kwenye vituo vya kupigia kura, uzembe katika kutekeleza majukumu yao na kutoa taarifa za kupotosha kuhusu maandalizi ya uchaguzi kuwa yamekamilika huku wakijua si kweli.

"Wapo waliodiriki kumsingizia mpiga chapa mkuu wa serikali kuwa alipelekewa nyaraka kwa ajili ya kuzichapa, lakini akazikosea, wakati siyo kweli kwa sababu zilipelekwa kwa watoa huduma binafsi," anasema.

**UCHAGUZI WA 2019**

Jafo anasema, Rais John Magufuli anatamani wakurugenzi waende kutekeleza demokrasia vizuri kwenye uchaguzi huo na ndiyo maana ametoa uwezeshaji kwa kila eneo, hivyo hatarajii kusikia hujuma.

"Naomba niwaambie huu uchaguzi ni mgumu sana lengo letu demokrasia itamalaki. Sisi tuliopewa dhamana ni jukumu letu kubwa kuhakikisha hiyo demokrasia kwenda kufanya kazi yake, kila mmoja wetu aende akatimize wajibu wake," anasema Jafo.

Ndivyo Jafo anavyokaririwa na vyombo vya habari akisema mwishoni mwa wiki iliyopita, jijini Dodoma, akifungua kikao kazi cha makatibu tawala wa mikoa, wakurugenzi wa halmashauri na wasimamizi wa uchaguzi huo.

Anasema, uchaguzi huo unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 82, na kwamba mkurugenzi yeyote atakayebainika kukwamisha au kuhujumu uchaguzi huo hataonewa huruma bali atawajibishwa.

"Sasa wewe mkurugenzi wa halmashauri ukafanye jambo lingine lolote kuhujumu mchakato mzima wa uchaguzi. Fedha hizo ni kwa ajili ya uchaguzi si vinginevyo, watakaothubutu kuzifuja 'watazitema'," anasema.

Anasema, wasimamizi wa uchaguzi wana jukumu na mzigo mkubwa na kwamba jambo la kwanza ni kuhakikisha uchaguzi unakuwa mzuri zaidi, kwa sababu kila msimamizi wa uchaguzi ana kanuni.

"Kanuni inasema waziri kwa wakati wowote anaweza kutoa miongozo. Katibu pia anaweza akatoa mwongozo, natamani sana mlioteuliwa mwende vizuri mpaka mmalize vizuri kwa mujibu wa kanuni zetu," anasema.

**KUSHIRIKI UCHAGUZI**

Wakati serikali ikijipanga kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa ufanisi, wananchi nao hawana budi kujiandaa kushiriki katika kuchagua viongozi wao au kuwania nafasi za uongozi.

Ni muhimu kufanya hivyo kwa kuzingatia kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaweka wazi kuwa kila mtu ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Haitapendeza iwapo serikali inatumia gharama kiasi hicho halafu Watanzania wasijitokeze kwa wingi kuchagua viongozi, bali watumie haki yao ya kidemokrasia ya kuwapata wawakilishi kwenye ngazi za maamuzi.

Kwa sasa elimu ya mpigakura imekuwa ikitolewa maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kumwezesha kila Mtanzania kushiriki katika uchaguzi, hivyo ni muhimu kuzingatia elimu na kuitumia.

Kimsingi uchaguzi ni jambo la hiyari na kidemokrasia, ambalo mtu anaweza kuamua kushiriki au kutoshiriki, lakini ili kutimiza demokrasia vizuri, ni muhimu kushiriki kuchagua viongozi.

Vilevile ikumbukwe kuwa kutoshiriki katika uchaguzi na hata kutowania uongozi ni sawa na kuruhusu kuwapo kwa viongozi wasiofaa na ikitokea hali kama hiyo aliyekacha uchaguzi asilalamikie uwepo wa viongozi wabovu.

# Marekani na kigugumizi kupigwa visima vya mafuta Saudi Arabia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Donald Trump wa Marekani amesema kuwa anafanya kila awezalo kujizuia kuhusu nini cha kufanya baada ya shambulio kubwa dhidi ya medani kuu ya mafuta nchini Saudi Arabia.

Wasiwasi ulitanda katika masoko ya mafuta ghafi duniani pamoja na masoko ya fedha baada ya shambulio la 'droni' zenye silaha dhidi ya medani kuu ya kuchimba na kuhifadhi mafuta upande wa Mashariki wa Saudia.

Shambulio hilo lilifanyika wakati wa kumbukumbu ya miaka 18 ya mashambulizi ya World Trade Centre (minara pacha ya biashara kimataifa) ambako walioteka ndege na kuzitumia kama silaha 19 miongoni mwao walitokea Saudia. Zaidi ya watu 2,500 walikufa.

Jambo la kushangaza ni kuwa shambulio hilo halikubadili kwa kina bei ya mafuta, ambayo ilipanda kwa ghafla halafu ikashuka baada ya siku chache, ikaanza tena kupanda kiasi tu.

Haikurudi katika viwango vya awali na Saudia inatazamia kurudisha uwezo wake wa kuzalisha mafuta kilipokuwa, ndani ya wiki kadhaa na si miezi.

Masoko ya hisa pia yalipata mshtuko halafu yakapungua, kiasi ambacho inaelekea wasiwasi mkubwa siyo shambulio hilo na athari zake katika soko la mafua, ila dhamira ya kujibu mashambulizi ipanuke kuwa vita halisi.

Hakuna shaka yoyote kuwa shambulio hilo linaendana na sera ya Iran ya kuzuia biashara ya mafuta katika eneo la Ghuba mradi yenyewe imewekewa vikwazo na Marekani, lakini imefanya kila juhudi kuonyesha kuwa chanzo cha shambulio hilo ni vita vya Yemen.

Maofisa wa ngazi za juu wa Jeshi la Saudia walijitahidi kuonyesha kwa waandishi wa habari na viongozi wa Saudia, mabalozi na wageni wengine kuwa makundi ya Wahuthi hayana uwezo wa shambulio kama hili, wakisema makombora na droni zilizotumika zilitokea Kaskazini. Yemen ni Kusini ya Saudia.

Mara baada ya shambulio hilo kufanyika, likaondoa nusu ya uwezo wa Saudia kuzalisha mafuta, hatua ya kwanza ilikuwa ni kuzuia bei ya mafuta isipande kwa nguvu hasa katika soko la kimataifa.

Wachambuzi walisema Saudia inatumia kiasi cha mapipa milioni nne kwa siku na kuuza nje mapipa milioni sita.

Ikitumia mapipa hayo milioni nne kwa siku inabakiwa na mapipa milioni moja tu ya kuuza nje na katika mazingira ambako Iran inauza mafuta kidogo tu na kuna wazalishaji wa kati kama Venezuela nao wako taabani, bei ya mafuta ingeweza kupanda haraka.

Tofauti ni kuwa kuna nchi kadhaa zenye hifadhi kubwa ya mafuta inayoweza kutumika katika hali kama hii, kwa mfano Rais Trump aliongelea uwezekano wa kupunguza hifadhi ya Marekani ya mafuta, wakati wahifadhi wengine wakubwa kama Russia, Japan na China walikuwa pia wanaangalia hali inavyokwenda.



Kiongozi wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei. **PICHA: MTANDAO**

> Baadhi ya wachambuzi waligusa pia uwezekano wa Marekani kuwa muuzaji mkubwa wa mafuta duniani endapo Saudia itachukua muda mrefu kidogo kujiimarisha katika eneo hilo.

Pia kulikuwa na uwezekano wa kuongeza uzalishaji wa mafuta kutoka kwenye miamba ya tope la mafuta (shale) hasa nchini Marekani, licha ya upinzani mkubwa wa wanamazingira. Kimsingi tatizo halikuwa katika mafuta ila hali ya kijeshi eneo hilo.

Wahuthi wanaofadhiliwa na Iran na wanaojigamba kufanya shambulio hilo wako vitani dhidi ya serikali ya Yemen inayolindwa kijeshi na ufalme wa Saudia na huku Iran ikiwa ngome ya Wahuthi.

Iran na Wahuthi inasema kuwa suala ni Saudia kuondoka katika vita ya Yemen, wakati Marekani na washirika wake wanasema tatizo ni Iran kuwasha moto kote Mashariki ya Kati, na sasa kufanya kila iwezalo kuzuia biashara ya mafuta, kwa kushambulia meli eneo la bahari kuu.

Ila kulikuwa na ugumu wa kitaaluma wa kuthibitisha droni na makombora hayo yalitupwa kutoka wapi na pia mivutano mikubwa nchini Marekani na kwingineko ambao si wengi wanataka pigo dhidi ya Iran, kwani utawala wa Saudia haupendwi maeneo mengi tu barani Ulaya au Marekani.

Rais Trump kwa mfano amekuwa mwangalifu kwa anachosema, hasemi kuwa shambulio la kujibu kilichotokea Saudia litafanywa, lakini alisisitiza katika mkutano na waandishi wa habari pamoja na mgeni wake, Waziri Mkuu Scott Morrison wa Australia kuwa ni rahisi sana kuingia Iran, kuipiga kwa muda mfupi, lakini matokeo yake ni makubwa sana.

Aliweka mkazo katika hatua nyingine za kuweka vikwazo dhidi ya Iran, kuwa Benki Kuu ya Iran imeongezwa katika vikwazo. Maana yake ni kuwa hakuna mtu anayefanya biashara na Marekani anayeruhusiwa kufanya biashara yoyote na Benki Kuu ya Iran; alisisitiza vikwazo vinafanya kazi vizuri sana.

Katika hatua ya awali, Rais Trump alionekana kuwa tayari kufanya shambulio la nguvu dhidi ya Iran, lakini azma hiyo ikaanza kupungua nguvu siku zilivyoenda.

Ingekuwa kuna utawala tofauti Saudia, siyo ajabu ingekuwa mwanzo wa vita kwani medani hiyo ya mafuta licha ya kuwa ni mali ya Saudia, lakini Marekani ndiye mshirika mkubwa kiteknolojia na kwa miaka mingi ilikuwa inamiliki hisa moja kwa moja katika Aramco (Arabian American Oil) ambayo baadaye inaitwa Saudi Aramco.

Alisema Marekani iko 'locked and loaded,' ikingojea Saudia iwaambie nani hasa alifanya shambulio hilo, baadaye akaacha suala liendelee kuangaliwa, kujadiliwa kati ya vyombo vya ulinzi na usalama Marekani na miongoni wa washirika wa Marekani Ulaya, n.k.

Suala jingine lililowashangaza baadhi ya wachambuzi ni jinsi Saudia inavyoonyesha udhaifu wa kutumia silaha lukuki inazoagiza kutoka Marekani na kulazimika kufunga bomba la mafuta kutokea eneo la Mashariki ya nchi hiyo kwenda Bahrain, moja ya falme za Ghuba, kurahisisha uuzaji nje.

Licha ya kuwa hakuna nchi inayoweza kulinda kila eneo la miundombinu muhimu kwao taifa, shambulio hilo litaleta kuulizwa maswali nchini Saudia kuhusu matumizi ya raslimali, kama ununuzi wa silaha umejenga uwezo wa kujilinda na kama ufalme wa Saudia una uwezo wa kuendelea na vita vya Yemen.

Licha ya kuwa utawala wa Trump unataka sana kutoa funzo kwa Iran kutokana na shambulio hilo, kisirisiri Marekani inataka pia mabadiliko Saudia, na bado haitaki kuingia vitani halisi na Iran kwani hali inaweza kufumua ukanda wote.

Baadhi ya wachambuzi waligusa pia uwezekano wa Marekani kuwa muuzaji mkubwa wa mafuta duniani endapo Saudia itachukua muda mrefu kidogo kujiimarisha katika eneo hilo.

Marekani ina utajiri mkubwa wa 'shale,' lakini uvunaji wake ni haribifu zaidi kwa mazingira kuliko mafuta ya kawaida.

Kutoa mafuta katika mazingira hayo siyo kuchimba na kuvuta juu ila kufanya ongezeko la thamani kama katika usafishaji wa dhahabu katika maji.

Baadhi nchini Marekani wanaona kuwa Marekani ina nafasi ya kuchukulia changamoto hiyo kibiashara kuwa inatokana na suala tata la vita ya Yemen, wakati ambapo kutokuwa tayari kwa nchi nyingine kuunga mkono au kushiriki mashambulio kutachangia Rais Trump kujizuia zaidi.

Ongezeko hafifu la bei ya mafuta nalo linaondoa uharaka wa kuzuia Iran isivuruge zaidi hali ya eneo hilo, huku Israel na Saudia wakijipanga kufanya shambulizi la nguvu dhidi ya Iran.

# Umakini muhimu tamu, chungu mitandao ya kijamii katika siasa



Rais John Magufuli (kushoto), William Ngeleja (kulia) na Januari Makamba, wanasiasa vijana ambao inaarifiwa walimwomba msamaha, kufuatia kuvuja kwa mazungumzo mtandaoni yakimsema Rais. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

mitandao ya kijamii kwa namna ya kipekee na lazima nikiri kuwa msukumo wa kuandika makala hii unatokana na shauku ya kuelezea umuhimu wa mitandao ya kijamii uliongezeka maradufu kipindi niliposhindwa kuipata huduma yake.

Mitandao ya kijamii inatafsiriwa kama nyenzo ya kuunganisha watu kwa kuwaleta pamoja na kujenga urafiki miongoni mwao ndani na nje ya nchi.

Pia inaunganisha watu wenye shauku ya aina moja, kwa maana mtumiaji anapaswa kujitambua mapema na kujiweka katika kundi analodhani linamfaa au lina manufaa zaidi kwake.

Binafsi ninapenda kufuatilia mambo ya siasa, kwa maana hii niliigeuza mitandao ya kijamii kama chombo cha habari kwa kupafanya mahala pa kujifunza, kuhabarika na kijiwe cha kujadili mambo ya siasa.

Ingawa zipo faida nyingi za mitandao ya kijamii, itakuwa ni ajabu sana nikijisaulisha kuwa hakuna changamoto zilizoletwa na mitandao ya kijamii.

Hivyo makala hii italenga kuchambua faida na hasara zilizoletwa na mitandao hiyo kwa upande wa siasa na wanasiasa kwa ujumla.

**TAMU ZA MITANDAO YA KIJAMII**

Mitandao ya kijamii inatoa fursa ya kupata habari nyingi za kisiasa ndani ya muda mfupi.

Katika moja ya makala ya mwandishi Christian Bwaya inayohusiana na mambo ya teknolojia anasema: "Mitandao hii hasa ya kijamii ni kama 'maporomoko' ya habari mpya kila sekunde yanaitwa 'streaming', 'TL' na majina mengine...kadri unavyofuatilia habari moja, ndivyo unaletewa 'mafuriko' ya zingine mpya...hukutani na ishara kuwa sasa umekaribia kufikia mwisho, kapumzike na matokeo yake unaweza kujikuta muda wote unaunganisha habari moja kwenda nyingine."

> Mtumiaji halazimiki kusubiria au kutegemea taarifa ya habari kwa kuwa ana uhakika wa kupata habari 'mithili ya mafuriko' muda wowote anaojisikia kiganjani.

Ingawa mwandishi huyu alikuwa anajaribu kuzungumzia changamoto za kutumia mitandao hii (nitayajadili mwishoni), lakini kwa upande mwingine maneno hayo yanaelezea faida kubwa iliyoletwa na mitandao ya kijamii kwa wadau wa siasa.

Mtumiaji ana uhakika wa kupata habari nyingi za kisiasa kadri muda na nafasi yake itakavyomruhusu.

Mtumiaji halazimiki kusubiria au kutegemea taarifa ya habari kwa kuwa ana uhakika wa kupata habari 'mithili ya mafuriko' muda wowote anaojisikia kiganjani.

Mitandao ya kijamii kwa upande mwingine imezidisha fursa kwa wadau wa siasa kutoa maoni yao kuhusiana na habari, mijadala au makala mbalimbali kwa njia ya ujumbe mfupi 'comments'.

Kwa maana hii, ushirikishwaji wa watu kutoa mawazo yao kuhusiana na mambo ya kisiasa umeongezeka maradufu.

Pia inatoa fursa kwa mtoa habari, mjadala au makala kujua maoni ya watu kuhusiana na taarifa husika.



Rais John Magufuli (kulia) akiwa na Nape Nnauye alipokwenda Ikulu kuomba msamaha kufuatia kuvuja kwa mazungumzo mtandaoni yaliyokuwa yakimsema Rais. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Faida nyingine inayotokana na mitandao ya kijamii ni kuibuka kwa kundi la watu wanaojiita 'wanaharakati'.

Kwa kujua na kutambua nguvu ya mitandao ya kijamii katika kufikisha ujumbe, 'wanaharakati wa mitandao ya kijamii' hufanya kila wawezalo kuitumia ipasavyo kufikisha sauti zao zisikike na hatimaye kuleta tofauti inayokusudiwa kwa nia njema.

Hii imesaidia kufikisha kero mbalimbali kwa serikali au viongozi wao ili kusaidia kuzipatia ufumbuzi.

Kwa maana hii, mtu akishindwa kufikisha kilio chake kupitia vyombo vya habari, bado anaweza kuwatumia 'wanaharakati wa mitandao ya kijamii' kufikisha kero zake kwa viongozi na wanasiasa kwa ajili ya ufumbuzi.

Isitoshe mitandao ya kijamii imewarahisishia wananchi kuona kazi mbalimbali zifanywazo na viongozi wao.

Kupitia ukurasa wa instagram wa Mbunge wa Segerea, Bonnah Kaluwa, napata fursa ya kuona kazi mbalimbali zinazofanywa na mbunge huyo katika jimbo lake.

Anaitumia pia kutoa taarifa mbalimbali kama ratiba ya mikutano kati yake na wananchi wa jimbo lake. Kwa maana hii mitandao ya kijamii imewasaidia wanasiasa kufikisha taarifa zao kwa urahisi na kuwaonyesha wapigakura kazi mbalimbali za kimaendeleo wazifanyazo kwenye maeneo yao.

Mitandao ya kijamii pia inatoa fursa kwa wananchi na wadau wa siasa kuona vikao na kampeni za kisiasa 'mubashara'.

Hii imewarahisishia wanasiasa kutangaza sera na kufikisha jumbe zao kwa urahisi. Nakumbuka mwaka 2016 nilifuatilia kwa karibu kampeni za Rais Donald Trump wa Marekani kupitia facebook 'mubashara'.

**CHANGAMOTO**

Hata hivyo, hakuna zuri lisilokosa na kasoro. Zipo changamoto zilizoletwa na mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa na wanasiasa.

Moja ya changamoto kubwa inayoikabili mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa (na kwa ujumla wake) ni kuwapo kwa habari nyingi feki na za kizushi.

Kwa kuwa mitandao ya kijamii haina uchujwaji wa habari (filtration) kama ilivyo kwa vyombo vya habari vya kitamaduni, mchanganyiko wa habari za ukweli, uongo au zilizozidishwa chumvi ni nyingi sana.

Shida inazidi kuwa kubwa kwa wapokeaji wa habari hizo ambao wanaupokea uongo uliotolewa kwa nia mbaya kama ulivyo.

Hii inatokana na watu wengi kuwa wavivu kuchambua kwa undani au kufuatilia ukweli wa taarifa mbalimbali.

Wapo watu kwenye mitandao ya kijamii ambao kwa nyakati nyingine huitumia vibaya kuwadhalilisha viongozi wenye heshima na hadhi kubwa kwenye jamii.

Ingawa yawezekana baadhi ya tuhuma zinazoanzia kwenye mitandao ya kijamii zikawa na ukweli, lakini lugha inayotumika kuziwasilisha zikawa si nzuri (matusi).

**CHUKI**

Wapo wenye chuki binafsi ambao huzusha kwa makusudi habari zilizojaa chuki kwa viongozi mbalimbali kwa lengo la kuwadhalilisha au kuwashushia hadhi yao.

Mara nyingi watu wa aina hii hung'ang'ania 'ishu' zisizo na msingi lakini zenye madhara kwa hadhi na heshima ya mwanasiasa husika katika jamii.

Hakika hili si jambo zuri kwani viongozi na wanasiasa hawa ilichukua muda mrefu kuitengeneza hadhi na heshima waliyonayo, hivyo kutokea mtu au kikundi cha watu kuja kumchafua kirahisi kwa sababu binafsi si jambo zuri.

Kwa sisi wadau wa kufuatilia mambo ya siasa huwa tunakutana na 'watumiaji wasumbufu' kwenye mitandao hii.

Hawa ni wasumbufu kwa maana ya watu wanaovuka mipaka katika kupishana hoja kistaarabu hadi kufikia kashfa, matusi na udhalilishaji.

> Mara nyingi watu wa aina hii hung'ang'ania 'ishu' zisizo na msingi lakini zenye madhara kwa hadhi na heshima ya mwanasiasa husika katika jamii.

**USHAURI**

Kutokana na mitandao ya kijamii kutengenezwa kwa mfumo wa kumvutia mtumiaji, wadau wanapaswa kuchukua tahadhari na kujidhibiti ili kuepuka kunogewa na kujikuta wanaitumia kila saa.

Wanapaswa kuepuka kugusagusa simu zao kuepuka 'mafuriko ya habari' za kisiasa zinazotoka kila saa, ambazo yawezekana nyingine mtumiaji hazihitaji.

Hii itasaidia wadau kuzidisha uzingativu wa shughuli wanazofanya kwenye maeneo yao ya kazi.

Lazima wadau wakumbuke kuwa mitandao ya kijamii ina mchanganyiko wa habari nyingi za ukweli na uongo na hivyo watumiaji wanapaswa kuwa makini na ikiwezekana kufuatilia habari iliyotolewa kwa kina ili kujua ukweli wa taarifa iliyotolewa.

Vipo vyanzo makini kwenye mitandao ya kijamii ambavyo vina hadhi (status) ya kutoa habari za ukweli ni vyema tukazitumia hivyo.

Kwa upande wa kumdhibiti mtumiaji msumbufu, njia pekee ya kukabiliana naye ni kumzuia kwa sababu jaribio lolote la kumwelimisha hata liwe la kistaarabu kiasi gani litaishia kuzua balaa zaidi.

***Kwa maoni zaidi mwandishi anapatikana kwa barua pepe fransiscompangala08@gmail.com***

## Robert Mugabe azikwa



Ibada ya mazishi ya Robert Mugabe ambaye ni Rais wa zamani wa Zimbabwe iliyofanyika kijijini kwake Kutama, Wilaya ya Zvimba kilomita 90, Magharibi mwa mji mkuu Harare. **PICHA: MTANDAO**

RAIS wa zamani wa Zimbabwe Robert Mugabe hatimaye amezikwa kijijini kwake Kutama.

Mugabe alifariki wiki tatu zilizopita nchini Singapore alikokuwa akipatiwa matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimsumbua.

Mwili wa Mugabe umepumzishwa kwenye ua wa nyumbani kwake katika kijiji cha Kutama, Wilaya ya Zvimba kilomita 90, Magharibi mwa Jiji la Harare.

Mamia ya waombolezaji walikusanyika kwenye tukio hilo ambalo awali lilitarajiwa kuwa ni la faragha na kuhusisha familia tu.

Wengi wao walikuwa wamevalia fulana nyeupe zilizokuwa na picha ya Mugabe na zilizoandikwa ujumbe "Baba wa taifa", "Mkombozi" na "Mbeba tochi."

Baadhi yao walikuwa wakiimba na kucheza na wengine walikuwa wamekaa kimya kwenye mahema meupe yaliyoandaliwa maalumu kwa shughuli hiyo.

Mkewe Grace Mugabe pamoja na watoto wao walisindikiza jeneza la Mugabe, lililokuwa limezungushiwa bendera ya Zimbabwe iliyokuwa na rangi ya kijani, njano, nyekundu na nyeusi. Padri aliyeongoza ibada ya mazishi alimwomba Mungu amuhurumie Mugabe, wakati familia ilipouaga mwili wake na kuongeza kwa kusema kuwa "mtu huyu ataishi milele."

Hakukuwa na ofisa yoyote mwandamizi wa serikali miongoni mwa waombolezaji.

Familia ya Mugabe iliamua kumzika mwasisi huyo wa taifa katika kijiji cha Kutama baada ya wiki za vuta ni kuvute kati ya familia na serikali iliyotaka mwili wake kupumzishwa kwenye makaburi ya kitaifa ya mashujaa jijini Harare.

Ulinzi uliimarishwa nchini humo wakati familia hiyo ilipokuwa ikiandaa mazishi yake.

Awali shughuli hiyo ilitarajiwa kuhudhuriwa na watu waliothibitishwa, tofauti na makubaliano ya awali ya familia na wazee wa kimila kwamba kila mtu angeruhusiwa kuhudhuria.

Msemaji wa chama tawala cha ZANU-PF, Simon Khaya Moyo ameyaita mazishi hayo ya faragha kuwa ni hatua ya "kusikitisha sana."

Mpiganaji huyo wa zamani wa msituni alichukua mamlaka baada ya uhuru kutoka kwa wakoloni mnamo mwaka 1980. **BBC**

# Rwanda inavyojijengea heshima kupitia wahamiaji toka Libya



Rais Paul Kagame wa Rwanda. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

NCHI ndogo isiyokuwa na bandari katika ukanda wa Afrika Mashariki, ikiwa na watu milioni 12 na eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 26,338, nikimaanisha Rwanda, imejitosa kuwachukua wahamiaji kutoka mataifa tofauti Afrika waliokwama nchini Libya.

Raia hao wanaotambulika kama wahamiaji haramu, walikuwa wanajaribu kwenda kwenye mataifa kadhaa ya Ulaya kupitia bahari ya Mediterranean, lakini wakashindwa kutokana na udhibiti unaofanywa katika nchi husika.

Idadi yao inakadiriwa kuwa zaidi ya 6,000 ambapo katika awamu ya kwanza, Rwanda imewachukua 66 wakiwamo wanawake na watoto. Wamehifadhiwa kwenye kambi iliyopo nje kidogo ya jiji la Kigali.

Wengi wa wahamiaji hao wanatoka katika nchi za Eritrea, Ethiopia, Somalia, Sudan na mataifa mengine hivyo waliobaki wanazuiliwa kwenye vituo vinavyoendeshwa na wanamgambo wa Libya wanaoshutumiwa kwa utesaji.

Msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Wakimbizi (UNHCR) katika Kanda ya Afrika, Charlie Yaxley, amekaririwa na Shirika la Habari za Uingereza (BBC) akiwa nchini Rwanda akisema, wahamiaji haramu hao watatafutiwa stakabadhi za kuomba hifadhi kwa watakaotaka kuishi Rwanda na pia kuwasaidia watakaoamua kurejea makwao.

> Nchi inaweza kuwapokea wahamiaji 30,000 kwa kipindi kirefu, lakini ikawatoa raia wake kwa maelfu zaidi kupata fursa za kuingia, kufanya kazi na hata kuishi kwenye mataifa mengine.

Kwa mujibu wa Yaxley, UNHCR itawagharamia wahamiaji hao nchini Rwanda kwa kuwapa mahitaji muhimu kama chakula, maji na malazi, huku wakihudumiwa na wataalamu tisa watakaowasaidia kuondokana na madhara hasa ya kisaikolojia yaliyotokana na mateso waliyoyapata walipokuwa Libya.

Mtaaluma wa masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Mathayo Sore, anasema hatua ya utawala wa Rwanda kuwachukua wahamiaji hao inaweza kutafsiriwa tofauti, miongoni mwa hizo ikiwa ni kujijengea heshima kuwa nchi yenye utulivu.

"Kwa muda mrefu sasa Rwanda imekuwa miongoni mwa nchi zilizo na historia ya machafuko, vurugu na mauaji, hivyo kusababisha kutoa wakimbizi, sasa kwa kuwapokea wahamiaji haramu hao inaweza kutaja kujijengea heshima kwamba sasa hivi kuna utulivu na amani nchini humo," anasema.

Naye mwanaharakati Fransisca Onesmo, anasema kitendo cha Rwanda kinaweza kutafsiriwa kama hatua itakayojenga imani kwa wadau wa maendeleo na uwekezaji, kwamba inafaa katika uendeshaji wa shughuli za uzalishaji, biashara na uchumi.

"Rwanda iliyokuwa ikisifika kwa machafuko yakiwamo mauaji ya kimbari ya mwaka 1994, inapoamua kuwapokea wahamiaji haramu na kuwahakikishia haki ya kuishi kama watapenda, inaweza kufanikiwa kubadilisha fikra na hisia hasi zilizokuwapo awali kuhusu taifa hilo," anasema Fransica.

Hoja hiyo inaungwa mkono na Sore anayeongeza kuwa licha ya Rwanda kutoa nafasi kwa wahamiaji hao, inaweza kuisaidia nchi hiyo kwa raia wake wanaotafuta fursa za kuishi na kufanya biashara ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Nchi inaweza kuwapokea wahamiaji 30,000 kwa kipindi kirefu, lakini ikawatoa raia wake kwa maelfu zaidi kupata fursa za kuingia, kufanya kazi na hata kuishi kwenye mataifa mengine," anasema.

Hata hivyo, Sore anasema katika ujumla wake, hatua iliyofikiwa itamwibua Rais Kagame kisiasa na kidiplomasia, kwa kuonekana kuwa kiongozi anayewajali Waafrika wenzake, hali ambayo ni tofauti na inavyotokea kwa mataifa mengine.

Anatoa mfano wa mashambulizi, kujeruhi, kupora na mauaji yaliyofanywa na baadhi ya raia wa Afrika dhidi ya wageni wanaoishi na kufanya biashara nchini humo, kwamba ni kinyume cha hatua iliyofikiwa Rwanda.

**MATESO WALIPOKUWA LIBYA**

Daniel anatambulishwa kama mmoja wa wahamiaji hao akiwa miongoni mwa waliowasili Rwanda, anasema makali waliyoyapitia, yaliwafanya kujihisi kama wanatengana na kifo baada ya kupata taarifa za kusafirishwa kwenda Rwanda.

"Tulipokuwa tunaweka sahihi ya kidole tuliona barua inayosema tunaondoka kuelekea Rwanda na tukajihisi ni kama tulikuwa tunatengana na kifo," Daniel akaiambia BBC.

Rwanda imekubali kuwachukua wahamiaji 500 kwa ushirikiano na UNHCR, na katika kufanikisha azma hiyo, Umoja wa Afrika (AU) 'ulitia mkono wake' kwa kuhakikisha usafiri wa kutoka Libya hadi Rwanda kwa waathirika hao wa kadhia ikiwamo ubakaji.

Haijafahamika wazi ni kwa muda gani wahamiaji hao watakuwa Rwanda na wana uhuru kwa kiwango gani kuondoka nchini humo. Katibu wa Kudumu katika Wizara ya Udhibiti wa Masuala ya Dharura na Wakimbizi ya Rwanda, Olivier Kayumba, amesema wahamiaji watakaotaka kuishi nchini humo, watapewa hadhi ya ukimbizi.

**KWA NINI RWANDA**

Imeripotiwa kuwa hatua ya kuwapeleka wahamiaji nchini humo imekuja baada ya jitihada za kuwadhibiti maelfu ya wahamiaji haramu wanaokimbilia Ulaya kupitia safari hatari ya bahari ya Mediterranean kushindikana.

Takwimu za UNHCR zinaonyesha kuwa zaidi ya watu 45,500 waliingia Ulaya kupitia bahari hiyo, kiwango hicho kikiwa kimepungua kwa asilimia 30 ikilinganishwa na mwaka 2018.

Pamoja na mafanikio ya Rwanda, Umoja wa Mataifa (UN) una kituo cha kuwaokoa wahamiaji kama hao kilichopo Niger, taifa jingine linalotumiwa kwa upande wa Kaskazini mwa Afrika kama njia ya kwenda Ulaya.

Hata hivyo, taarifa zinaeleza kuwa ni kiasi kidogo cha wahamiaji 2,900 waliookolewa huko Niger, walifanikiwa kupata usaidizi katika nchi za Ulaya na kwingineko.

Taarifa zinaeleza kuwa kituo cha UN kilichopo Niger na kile kilichopo jijini Tripoli, Libya vimefurika wahamiaji kupita uwezo wa kuwahifadhi.

Kwa upande wao, nchi kadhaa za Ulaya zimetumia njia mbalimbali za kuwadhibiti wahamiaji haramu hasa kutoka Afrika, ingawa kwa sehemu kubwa, udhibiti huo umekosolewa kwa kuwa na viashiria vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

**MKATABA**

Serikali ya Rais Paul Kagame imesaini mkataba na Umoja wa Afrika na UNHCR, mapema mwezi Septemba, kutoa hifadhi kwa wahamiaji haramu waliokwama nchini Libya.

Serikali hiyo imetangaza kuwa na uwezo wa kuwachukua wahamiaji 30,000, ikiwa ni kupitia mpango wa kuwapokea 500 kila baada ya muda ambao haukuwekwa wazi.

TUJIKUMBUSHE

# Kwa nini CIA haikugundua shambulio la Septemba 11?

KUFELI kwa Shirika la Ujasusi nchini Marekani (CIA) kugundua ishara na onyo la shambulio la Septemba 11, 2001, imekuwa moja ya masuala tata katika historia ya huduma hiyo ya ujasusi duniani.

Kumekuwa na tume, hakiki na uchunguzi wa ndani hadi sasa na kwa upande mmoja kuna wale wanaosema kwamba kweli CIA hawakuziona ishara za mapema.

Hata hivyo, kuna wale wanaosema kwamba ni vigumu sana kugundua vitisho mapema na kwamba kitengo hicho cha ujasusi kilitumia kila njia.

Kimsingi hapo ndipo penye utata!

Labda swali litakuwaje iwapo nitakuambia kwamba dosari kama hizi zimesambaa zaidi kwenye huduma za kijasusi na inaathiri maelfu ya mashirika, serikali na makundi hii leo?

Wakati uchunguzi mwingi bado unaangazia kile ambacho shirika hilo la CIA lilifanya ama kushindwa kufanya, kutokana na habari lilizokuwa nazo kabla ya shambulio la 9/11, baadhi ya watu wanarudi nyuma na kuchunguza jinsi shirika hilo lilivyoundwa na hususan sera yake ya kuajiri.

"Mitihani mikuu miwili waliokumbana nayo watu hawa ilikuwa ile inayolinganishwa na mtu anapojiunga na chuo kikuu ambayo inabaini intelijensia ya anayeomba kazi... mbali na wasifu wa kisaikolojia kuchunguza hali yake ya kiakili," anafafanua mfanyakazi wa zamani wa CIA na kuongeza: "Vipimo hivyo viliwaondoa watu ambao hawakuwa bora katika maeneo hayo yote mawili."

Mfanyakazi huyo wa zamani anabainisha kwamba katika mwaka aliowasilisha maombi yake ya kazi katika shirika hilo ni mwombaji mmoja kwa kila waombaji 20,000 aliyepata kazi, huku CIA ikisema iliajiri watu bora.

Anafafanua, wengi walioteuliwa hata hivyo walikuwa wakifanana na kwamba kwa upande wa wanaume walikuwa ni weupe, Wamarekani na waumini wa dini ya Kiprotestanti.

"Hili ni suala la kawaida katika kuajiri watu...kwamba huajiri watu wanaojiona kuwa wenyewe," anasema.

Katika utafiti wao, wataalamu wa kiintelijensia Milo Jones na Phillipe Silberzahn waliandika sifa ya utambulisho wa kitengo cha CIA na utamaduni wake kuanzia mwaka 1947 hadi 2001.

Kwamba sifa yake ilikuwa ni mchanganyiko wake wa wafanyakazi kutokana na rangi, jinsia, kabila na tabaka kihistoria. Utafiti uliofanywa na Jenerali mmoja kuhusu ajira ulibaini kwamba mwaka 1964, tawi la CIA na idara za takwimu za kitaifa hazikuwa kabisa na wataalamu weusi, Wayahudi, wanawake na kwamba ilikuwa na wafuasi wachache wa Kanisa Katoliki.

Kufikia mwaka 1967, kulingana na ripoti, kulikuwa na wafanyakazi 20 Wamarekani weusi kati ya wafanyakazi 20,000, huku idara hiyo ikiendelea na utamaduni wake wa kutoajiri watu wa kundi la walio wachache kutoka 1960 hadi 1980.

Na hadi mwaka 1975, jamii ya kiintelijensia ya Marekani, waziwazi ilipinga kuajiriwa kwa wapenzi wa jinsia moja.

Akizungumza kuhusu uzoefu wake na shirika hilo kwa mwaka 1980, mtu aliyekuwa na habari za ndani aliandika kwamba mchakato wa kuajiri ulisababisha kuonekana kuwa wale walioajiriwa wanafanana na wale waliokuwa tayari wameshaajiriwa, wakiwamo watu weupe, watu wa tabaka la katikati, matajiri na wale wanaotoka vyuo vikuu. Aidha, ofisa mmoja alinukuliwa akisema CIA ina maofisa wanaofanana kama mchele.



Osama Bin Laden. **PICHA: MTANDAO**

> “Bin Laden alivalia joho si kwa sababu alikuwa mtu aliyepitwa na wakati, asiye na fikra nzuri ama asiyejua teknolojia, bali kwa sababu alitaka kufanana na mtume Muhammad.

Na miezi kadhaa kabla ya shambulio la Septemba 11, jarida la kimataifa kuhusu intelijensia liliandika:

"Tangu kuanzishwa kwake, jamii ya ujasusi ilishirikisha watu weupe si kwamba ndio lililokuwa tabaka katika uongozi, bali kwa sababu walionekana kama wadhamini na walinzi wa maadili na thamani ya Wamarekani."

Lakini ni kwa nini suala hili la ajira katika kitengo hicho ni tatizo?

Unapounda kikosi cha wanariadha cha mbio za kupokezana vijiti, unatazama wanariadha wenye kasi.

Kwa nini ni muhimu iwapo wana rangi ya kufanana, jinsia ama hata tabaka?

Kwa sababu wakati kuna tatizo kuu, hakuna mtu aliye na majibu yote, kila mtu ana dosari yake.

Na iwapo mtu ataajiri kundi la watu wanaotoka katika eneo moja, kuna uwezekano mkubwa kwamba watatoa suluhu inayofanana wakati wa tatizo.

### OSAMA BIN LADEN

Osama Bin Laden alitangaza vita dhidi ya Marekani kutoka katika pango moja eneo la Tora Bora, mwezi Februari mwaka 1996.

Picha zilimwonyesha mtu aliyekuwa na ndevu zilizokuwa zimefika chini ya kifua chake.

Alikuwa amevalia joho ndani ya sare ya kijeshi aliyovaa. Hii leo, baada ya kujua kila kitu kilichofanyika, tamko lake linaonekana kuwa la kutisha. Lakini chanzo kutoka CIA kilisema kwamba hakiamini kama mtu huyo aliye na ndevu, anaweza kuwa tishio la Marekani.

Kwa upande mwingine, hakuna uchanganuzi wowote aliodhani kwamba Bin Laden, anaweza kuwa tishio. Chanzo kingine kutoka katika shirika hilo kilisema kuwa hawakuweza kufadhili uchunguzi wowote ili kujua zaidi kuhusu Bin Laden na Al Qaeda kwa kuwa mtu huyo alikuwa akiishi pangoni.

Kwao alikuwa mtu ambaye alipitwa na wakati.

Richard Holbroke, Ofisa Mwandamizi katika utawala wa Rais Clinton alihoji: "Inawezekanaje mtu anayeishi pangoni kuwashinda viongozi katika jamii ya habari? Sasa fikiria mtu kutoka jamii ya Waislamu ambavyo angezichukulia picha za Osama!"

Bin Laden alivalia joho si kwa sababu alikuwa mtu aliyepitwa na wakati, asiye na fikra nzuri ama asiyejua teknolojia, bali kwa sababu alitaka kufanana na mtume Muhammad. Alifunga siku kama zile ambazo mtume Muhammad alifunga. Mienendo yake ambayo ilionekana kama mtu aliyepitwa na wakati kwa jamii ya Magharibi, ilifanana na tamaduni za Kiislamu zilizotokana na mtume wao.

Kama Lawrence Wright anavyoeleza katika kitabu chake cha Septemba 11, ambacho kilimshindia tuzo la Pulitzer kwamba Bin Laden, alitekeleza operesheni zake akitoa picha ambazo zilikuwa na maana ya ndani kwa Waislamu wengi, lakini hazikueleweka miongoni mwa wale ambao hawakuwa Waislamu.

Sasa fikiria mtu anayeijua dini ya Kiislamu jinsi ambavyo angepokea picha hizo.

Kuhusu pango alilokuwa akijificha, lina maana ya undani zaidi.

Kama vile kila Muislamu anavyojua, Mtume Muhammad alitafuta hifadhi katika pango baada ya kuwatoroka waliokuwa wakimtafuta Mecca. Kwa Waislamu pango ni eneo takatifu. Na Bin Laden alitumia maficho yake huko Tora Bora kama Hijja yake akitumia pango hilo kama propaganda.

Kama msomi mmoja wa Kiislamu alivyosema: Bin Laden hakuwa mjinga, alikuwa mtu wa mkakati. Alijua jinsi ya kutumia Qur'an kuwashawishi wale ambao baadaye wangekuja kuwa mashahidi katika shambulio la Septemba 11.

Wachanganuzi pia walidanganywa kwamba Bin Laden alikuwa akitoa taarifa zake kupitia mashairi.

Kwa wazungu wenye tabaka la katikati, alionekana kama Mullah aliyepitwa na wakati kwa kuishi katika pango. Hata hivyo kwa Waislamu, ushairi una maana tofauti kwani ni njia nzuri ya kuwasilisha ujumbe na kundi kama vile Taliban limekuwa likitumia mbinu hiyo kuwasilisha ujumbe wake.

Hata hivyo, kitengo hicho cha Marekani kilikuwa kikichunguza matamshi ya Bin Laden kikitumia ulinganishaji.

Kufikia mwaka 2000, ufuasi wa Bin Laden ulikuwa umefikia watu 20,000, wengi wao wakiwa na elimu ya taasisi na kupendelea uhandisi. Yazid Sufaat ambaye alikuwa mtafiti mkuu wa kundi la Al Qaeda alikuwa na shahada katika somo la Kemia. Na wengi walikuwa tayari kuuawa kwa dini yao.

Wakati huohuo, Ofisa Mwandamizi Paul Pillar, hakufikiria kwamba kuna uwezekano wa shambulio kubwa la kigaidi kufanyika.

Na dosari nyingine ya CIA ilikuwa kuchelewa kwake kuamini kwamba Bin Laden ataanzisha mgogoro na Marekani.

"Kwa nini nianze vita ambavyo sitashinda?"

Wachanganuzi hawakuelewa kwamba watu wanaopigana vita vya Jihad, ushindi haufai kuhakikishwa duniani bali peponi.

Ukweli ni kwamba mpango huo wa Al-Qaeda uliitwa "Harusi kuu."

Na ni itikadi ya watu wanaojitoa muhanga, kwamba siku ya kifo cha muuaji pia ni siku ya harusi yake, wakati anapokelewa na mabikira mbinguni.

CIA ingeongeza ufadhili wake kulichunguza kundi la Al- Qaeda, ingejaribu kuingia ndani ya kundi hilo, lakini katika shirika hilo la kijasusi, hawakuona sababu muhimu ya kufanya hivyo kwa haraka.

Hawakuongeza ufadhili kwa sababu hawakuona tishio.

Ukosefu wa Waislamu katika shirika hilo la CIA ni mojawapo ya mifano ya jinsi ukosefu wa watu wa jamii tofauti, ulivyodhoofisha kitengo hicho cha ujasusi kinachoongoza duniani.

Na inatoa wazo la jinsi watu kutoka jamii tofauti wangeweza kutoa suluhu ya tishio kama hilo la al-Qaeda. Lakini tatizo sio CIA pekee kwa kuwa unapotazama mabaraza ya mawaziri, kampuni za mawakili, uongozi wa kijeshi, na maofisa waandamizi pamoja na maofisa watendaji katika kampuni za kiteknolojia, pia tatizo hilo linapatikana.

Waajiri huwapendelea watu wanaofanana nao hivyo basi tunashindwa kuona hatari kwa sababu hatujui dosari zetu.

Hata hivyo, Shirika la CIA limechukua hatua muhimu ya kuorodhesha watu kutoka maeneo tofauti miongoni mwa wafanyakazi wake tangu shambulio hilo la Septemba 11 kufanyika.

Hata hivyo, tatizo bado linaendelea kulikabili shirika hilo na ripoti ya ndani kwa ndani ya mwaka 2015, ilitoa ukosoaji mkubwa. **BBC**

# Democratic waungana dhidi ya Trump suala la Ukraine




Baadhi ya raia wa Marekani wakiwa na mabango yanayoshinikiza kumshtaki Rais Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi ambao kwa wingi wao ni wa chama cha Democratic hatimaye wamepata hoja ya kuwaunganisha kuingia katika hatua ya kumchunguza Rais Donald Trump.

Ni kuhusu amri au shinikizo alilotoa kwa serikali ya Ukraine kufanya uchunguzi kuhusu anachofanya au 'dili' kadhaa za Hunter Biden, mwanaye Joe Biden, aliyekuwa Makamu wa Rais wakati wa Barack Obama na sasa ndiye anaongoza safu ya wanachama wa Democratic wanaowania kupewa bendera mwakani kupambana na Trump, akiwa anatafuta muhula wa pili.

Uwezekano wa kushtakiwa Trump endapo Baraza la Wawakilishi litafikia uamuzi huo utakuwa ndiyo mwisho wa Trump, kwa vile itabidi ajiuzulu. Hashtakiwi akiwa bado kitini.

Baadhi ya taarifa zinasema kuwa Trump aliweka shinikizo la kuchunguzwa shughuli za kina Biden katika sekta ya gesi nchini Ukraine na kuwa suala hilo lina uhusiano na kuondolewa kwa misaada ya kijeshi ya Marekani kwa nchi hiyo.

Rais Trump mwenyewe alisema katika mahojiano na waandishi wa habari Ikulu hivi majuzi kuwa anataka nchi nyingine za Magharibi zitoe misaada ya kijeshi inayohitajiwa, akidai kuwa Marekani inalipa peke yake wakati ni suala la wote kuchangia.

Trump alitoa mifano ya maeneo mengine ambako Marekani ndiyo imekuwa ikitoa fedha kwa masuala ya ulinzi na wengine wanaitegea.

Sakata hilo lilianza wakati ofisa mmoja wa shirika la ujasusi nchini Marekani, CIA alipopeleka taarifa ya kina katika moja ya vyombo vya habari vyenye mwelekeo wa Democratic kuonyesha mazungumzo ya simu kati ya Rais Trump na Rais Volodymyr Zelensky kushinikiza uchunguzi huo.

> Trump amemwelezea 'mtonyaji' wa suala hilo au 'mlipua bomu,' kuwa ni kama mhaini, tafsiri ambayo haikubaliki popote nchini Marekani, iwe ni kwa chama cha Democrat au Republican.

Vyombo vya habari vya kiliberali (vyenye uhusiano wa karibu na Democrat) vimeunganisha moja kwa moja shinikizo la kufanyika uchunguzi huo na kuondolewa sehemu kubwa ya misaada ya kijeshi.

Trump alikataa dai hilo, akaamrisha itolewe hadharani nakala iliyosanifiwa ya mazungumzo na Zelensky, lakini moto haukupoa.

Baadhi ya wabunge wanasheria wakasema kuwa nakala ya mazungumzo hayo inatoa undani wa suala hilo ambalo ni baya zaidi kwa Trump kuliko walivyotazamia, lakini watetezi wa Trump wanasema kuwa kuondoa misaada hiyo ni sehemu ya sera ya 'Amerika Kwanza.'

Inatokana na mwelekeo wa kupunguza misaada ya Marekani katika maeneo yasiyojenga maslahi ya nchi hiyo na siyo kutokana na hitaji hilo la kumchunguza mwanaye Biden na kwa upande huo kumhusisha baba yake.

Baadhi ya wanasiasa nchini Ukraine akiwamo Waziri Mkuu wa zamani nchini humo (inaelekea ni mpinzani wa Zelensky) wanataka nchi hiyo ifanye uchunguzi wa shughuli za kampuni zinazohusiana na kina Biden, lakini walizuiliwa.

Kuna baadhi ya taarifa zinasema kuwa Biden aliwahi kutamba kuwa amezuia uchunguzi dhidi ya kampuni ya mwanaye wakati huo suala lililokuwa linaendelea dhidi ya Trump ni Russia kuingilia uchaguzi mkuu Marekani mwaka 2016.

Katika uchunguzi huo ambao umeendelea na kujadiliwa kwa nguvu bungeni na vyombo vya habari hadi miezi michache iliyopita, wabunge wa Democratic hawakupata nguvu ya kutosha kujiamini kuleta mashtaka dhidi ya Trump.

Hata ilipotolewa taarifa ya mchunguzi maalum aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa FBI (shirika la upelelezi wa jinai nchini humo) bado hawakupata mahali pa uhakika pa kushika. Ila sasa wanapata mwanya: Trump alitaka hujuma kutoka nje.

Trump amekuwa akielekeza mashambulio pande tofauti kulingana na kinachozungumzwa lakini siyo watu wengi wanaomsikiliza, hata miongoni mwa viongozi wa Republican katika Baraza la Wawakilishi, baadhi wakiwa wametangulia kutaka uchunguzi ufanyike.

Mbaya zaidi kwa Trump, hata viongozi waandamizi wa Republican katika Baraza la Senate (ambako Republican ndiyo wengi) wameeleza mashaka ya kina kuhusu dhamira ya Trump katika suala hilo. Trump amemwelezea 'mtonyaji' wa suala hilo au 'mlipua bomu,' kuwa ni kama mhaini, tafsiri ambayo haikubaliki popote nchini Marekani, iwe ni kwa chama cha Democrat au Republican.

Ila kilichopo sasa ni shauku ya kujua alifanya nini, hizo 'kwanini' ni baadaye.

Kwa upande mmoja unaweza kusema kuwa wabunge wa Democratic wamechangamkia suala hili kwa kutazamia kuwa wanaweza kumwondoa Trump madarakani endapo atakutwa na hatia, hivyo iwe rahisi kwao kupata ushindi uchaguzi mkuu mwakani.

Lakini baadhi wanakiri kuwa hatari ya kipindi cha kuchafuliwa, kushtakiwa Trump kushirikiana na Russia kuvuruga uchaguzi mkuu 2016 iko pale pale, kuwa mjadala huo unaparaganyisha jitihada za kujenga taswira ya Marekani mpya ya 'haki sawa kwa wote' ambayo watangaza nia wa Democratic, akiwamo Biden, wanajaribu kujenga.

Endapo mjadala huo utachukua muda mrefu na Trump ashinde, asipatikane na hatia ni kampeni ya Democratic itakayofifia.

Kwa upande mwingine Trump amekuwa akitoa mwito kwa Biden kueleza bayana ni 'madili' gani yeye na mwanaye walikuwa wanafanya nchini Ukraine.

Ila suala hilo linaonekana ni la muda mrefu na kilichopo mezani ni Trump kutaka serikali ya Ukraine ichunguze au iangalie tena kitu ambacho labda kilikuwa kimesahaulika.

Kwa maana hiyo wakinzani wa Trump hawasemi hapakuwa na tatizo lolote na kile mwanaye Biden alichokuwa akifanya Ukraine ila ni rai kutoka Ikulu ya Marekani kwa suala hilo, na siyo litokane na mlolongo wa kawaida wa kisheria nchini humo.

Ndipo baadhi wanaongeza misaada ilitegewa kufanyika uchunguzi kama huo, lakini madai hayo yanaelekea kupwaya, kuwa ni masuala tofauti kabisa.

Hata hivyo wajumbe wa Democratic katika Baraza la Wawakilishi wameshapulia suala hilo kwa sababu lina uwezo wa kumuumiza Trump, na kwa hali yoyote inabidi walifanyie kazi baada ya 'mlipua bomu' (au mpiga filimbi kwa lugha ya kisheria Marekani) kutaja kuwa Biden alitakiwa achunguzwe Ukraine.

Endapo wasingeshalipua, uhalali wa mwito huo na kama si kuvunja sheria na kutumia madaraka vibaya kwa upande wa Rais Trump, ingekuwa sasa wanafuatilia Biden alifanya nini au mwanaye, ambayo ni sawa na kumtosa kama mtangaza nia muhimu, na mgombea tarajiwa dhidi ya Trump mwakani.

Kwa maana hiyo Democratic waliungana juu ya suala hilo ili kurunzi isiendelee kumulika kwa Biden, ila kwa Trump.

Hata hivyo, kuna hatari kuwa kampeni hii ya kumshtaki Trump kwa kutaka kina Biden wachunguzwe nchini Ukraine itaishia kuumiza kampeni ya Biden, kwani suala hili halikuwa linafahamika hadi sasa, na siyo ajabu undani wake ukawa sumu kwa kampeni ya mtangaza nia huyo mtangulizi.

Kimsingi, mwanaye Biden, Hunter alijiunga na bodi ya kampuni moja ya gesi nchini Ukraine ambayo mmiliki wake ni waziri wa zamani wa Ukraine aliyekuwa akichunguzwa kwa tuhuma za utakatishaji fedha.

Wachunguzi wa habari wanasema alimpendekeza Hunter Biden ili kupendezesha taswira ya kampuni hiyo, kwani wakati huo utawala wa Obama, Biden akiwa Makamu wa Rais, ulikuwa ukiicharura Ukraine kwa rushwa.

Sasa, miaka mitano baadaye, wakati Joe Biden anakimbilia urais wa Marekani, kulipua suala hilo upya kutazua maswali kuhusu dhamira na uwezo halisi wa Biden katika kupambana na rushwa.

Iweje wakati akiwa Makamu wa Rais amruhusu mwanaye ajiunge na bodi ya kampuni ambayo si kwa viwango vya Marekani, lakini hata kwa sheria za Ukraine ni kampuni ya mafisadi sugu?

Mwanasheria wa Trump, Rudoph (Rudi) Giuliani ambaye aliwahi kuwa Gavana wa Jimbo la New York alitaka uchunguzi kuhusu kina cha uhusiano kati ya kina Biden na fisadi Mykloa Zlochevsky, mmiliki wa Burisma, licha ya kuwa Ukraine haina uchunguzi dhidi yake kwa sasa. Kutaka kujua kama walitakatisha fedha pamoja ni kosa?





# Atoa neno la kuhofia uchawi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAZAZI na walezi mkoani Mbeya wameaswa kuwaondolea vijana wao fikra potofu kuwa kila anayefanikiwa kibiashara anajihusisha na ushirikina.

Aidha, wameaswa kuwapa vijana moyo wa ujasiri na kuthubutu kwenye biashara badala ya kuwaaminisha kuwa kila aliyepata mafanikio kwenye shughuli hizo anatumia ndumba.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa anazungumza na wakazi wa kata ya Nsalala katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Chalamila yuko kwenye mwendelezo wa ziara zake za kutembelea kata mbalimbali na kusikiliza kero za wananchi.

Mkuu wa Mkoa alisema kumekuwapo na kasumba kwa wakazi wengi mkoani hapa kuamini kuwa kila mfanyabiashara mwenye mafanikio ni mshirikina.

Hatua aliyosema inawapa uoga vijana wazawa kutumia fursa zilizopo na matokeo yake kuwanufaisha wageni wenye uthubutu.

Aliwataka wakazi mkoa huo kubadilika na kutambua kuwa kuendelea kuwa na imani za kishirikina kunawachelewesha kimaendeleo na wasipoangalia huenda miaka kadhaa ijayo wakawa maskini.

Chalamila alionya kuwa ni aibu kuwa maskini ndani ya ardhi yao huku wageni wakiwa matajiri.

"Lini ulikwenda kwenye duka la huyo unayemwita mchawi ukanunua simenti baada ya kufika nyumbani ikageuka kuku?" Alihoji.

"Nani alinunua bati baada ya kufika kwenye kuezeka zikawa nyasi?" Alihoji tena Chalamila.

Aliwasihi wakazi mkoani hapa kushikilia imani ya matumizi sahihi ya pesa kwa kuhakikisha wanazingatia kuweka zaidi akiba ya kile wanachozalisha kuliko kuwa na matumizi makubwa na yasiyo ya msingi.

Baadhi ya wakazi wa mamlaka ya mji mdogo wa Mbalizi walilalamikia huduma ya upatikanaji wa maji kuwa mbovu, huku pia wakisema gharama wanazotozwa hazilingani na huduma wanayopata.

Mmoja wa wakazi hao Magdalena Makole, alisema mara nyingi maji yanatoka muda wa kulala yaani kuanzia saa 6:00 usiku hadi saa 11 alfajiri hatua ambayo imefanya wawe sawa na wachawi ambao muda wanapokuwa wenzao wamelala wao ndiyo wanaingia kazini.

# Mizani dawa kudhibiti wezi wa viazi mviringo

**Na Nebart Msokwa, BUSOKELO**

WAKULIMA wa viazi mviringo wa Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe katika mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kuwatafutia mifuko rasmi ya kuuzia mazao yao ili wasidhulumiwe.

Walitoa madai hayo wakieleza kuwa wafanyabiashara wanatumia mifuko yenye ukubwa tofauti kuwaibia na kuwadhulumu mazao yao.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mbunge wa Busokelo na kuwahusisha wakulima wa zao hilo pamoja na maofisa wa Wakala wa Vipimo.

Wakizungumza, wananchi hao walidai kuwa baada ya serikali kupiga marufuku lumbesa, wafanyabiashara wamebuni mbinu mpya za kuwaibia wakiibua mifuko waliyojiandalia wenyewe.

Mmoja wa wakulima hao, Nuru Sabala, alisema wafanyabiashara hao wanawaletea mifuko midogo iitwayo 'kipeto' na kwamba wanadai kuwa ikiwa miwili ni sawa na gunia la kilo 100.

Alisema mbinu hiyo inayotumiwa na wafanyabiashara hao ni mbaya kuliko hata ujazo wa lumbesa uliokuwa unatumika miaka ya nyuma kabla serikali haijauzuia na kuweka utaratibu wa kipimo cha kilo 100 kinachotambulika kisheria.

"Mwaka huu tumeumia sana, wananunua kwa bei ndogo ambayo haiendani na gharama za uzalishaji, halafu wanashona vile wanavyotaka mifuko wanayosema ikiwa miwili ni sawa na gunia moja ni uongo wanatuibia," alilalamika Nuru.

Alisema wanauza gunia moja kwa Sh. 28,000 lakini gharama za uzalishaji zipo juu na kwamba wanauza kwa bei hiyo baada ya kusafirisha na kufikisha eneo mnunuzi alipoegesha gari.

Mkulima Lucas Malamba, aliiomba serikali kuwaandalia mifuko maalumu ambayo itakuwa kwa ajili ya kuuzia viazi pamoja na kutoa maelekezo ya namna ya ushonaji ili iwe rahisi kuwadhibiti wafanyabiashara wanaonunua viazi hivyo.

Alisema mifuko hiyo itakapoandaliwa wataweza kuwakataa wanunuzi wanaowadhulumu tofauti na hali ilivyo sasa.

"Wakati mwingine huwa tunakata tamaa lakini, hatuwezi maana ndio ajira yetu, tunaomba serikali itusaidie kwa kuandaa mifuko ambayo itakuwa na nembo ya viazi na iwe maalumu kwa ajili ya viazi pekee na pia watuelekeze namna ya kufunga," alisema Malamba.

Mbunge wa Busokelo, Mwakibete alisema ili kuepuka wizi wa aina hiyo, ni lazima sasa wakulima wauze mazao yao kwa kutumia mizani badala ya kukadiria kwenye mifuko ambayo hata hivyo inaletwa na wafanyabiashara.

Vilevile aliwaasa wakulima wa viazi kuunda umoja ambao utawasaidia kudhibiti wizi na kuwa na sauti ya pamoja katika kupanga bei ya kuuzia zao hilo tofauti na sasa hivi ambapo bei zinapangwa na wafanyabiashara.

"Wenzetu wakulima wa kahawa, chai, kakao na mazao mengine ya biashara wananufaika na mazao yao kwa sababu wana umoja unaowaweka pamoja kuepuka dhuluma na sisi wakulima wa viazi tunatakiwa tuwe na umoja. Na ikiwezekana tuunde ushirika sasa," alisema Mwakibete.

Kwa upande wake ofisa wa Wakala wa Vipimo, Robert Makule alisema ofisi yake ilikuwa haijui kama kuna wizi wa aina hiyo unafanyika na akawahakikishia wakulima kushirikiana nao kudhibiti hali hiyo.

Alisema njia pekee ya kutumia kuuza mazao hayo ni mizani kwani baada ya serikali kupiga marufuku lumbesa mbadala ni mizani tu.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya vipimo endapo mfanyabiashara na mkulima watakamatwa wakifanya biashara kwa kutumia vipimo vinavyozidi uzito wa kilo 105 faini ni kuanzia Sh. 100,000 mpaka Sh. milioni 20 au kifungo gerezani.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga (mwenye koti jeusi), akionyeshwa na mmoja wa wananchi wa Mji wa Kasumulu wilayani Kyela jana, maeneo yao yaliyochukuliwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha pamoja cha Forodha kati ya Tanzania na Malawi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# MUHAS kuwa na tawi Mbalizi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MBUNGE wa Mbeya Vijijini (CCM), amewatangazia wananchi mkoani Mbeya, kuanza kujiandaa kupokea miradi mikubwa ya afya itakayojengwa kwenye mji mdogo wa Mbalizi.

Mbunge huyo, Orani Njeza, alisema kuwa serikali inakusudia kujenga tawi jipya la Chuo Kikuu cha Afya Mhimbili (MUHAS) na Hospitali ya Kisasa ya Rufani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema hatua hiyo, itasaidia kuimarisha huduma za kijamii katika mji huo.

Aidha, ujenzi wa chuo hicho utaambatana na kujenga kiwanda cha dawa za binadamu ambacho kitakuwa kikubwa kuliko vyote Afrika Mashariki na Kati.

Hayo yalisemwa na Mbunge huyo wa Mbeya Vijijini, alipokuwa anazungumza na wananchi wa Mamlaka ya Mji wa Mbalizi, kwenye mkutano uliofanyika katika ofisi za Chama Cha Mapinduzi mjini Mbalizi na kuwataka wananchi wa mji huo kujiandaa kunufaika na mradi huo.

Alisema utekelezaji wa mradi huo utainua vijana 2,000 kwa kuwapatia ajira na hivyo kupunguza tatizo la kukosa kazi.

"Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais wetu John Magufuli, imeamua kutuletea neema hii hapa kwetu, sasa ni jukumu letu kujiandaa kuipokea na kuitumia kwa ajili ya maendeleo yetu na taifa kwa ujumla, ni mradi wa aina yake katika nchi hii," alisema Njeza.

Vilevile alisema kuna ujenzi wa hospitali ya wilaya inayojengwa katika kata ya Inyala ambayo itasogeza huduma karibu na wananchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi - CCM, Wilaya ya Mbeya Vijijini, Akimu Mwalupindi, alisema serikali ya awamu ya tano imefanya mambo makubwa ambayo yanawavutia hata wapinzani na kuwafanya waanze kukimbia vyama vyao.

Alisema kwa sasa chama hicho kinaheshimika na kukubalika hata kimataifa hali ambayo alisema inasaidia chama hicho kuendelea kuimarika na kuwa na uwezekano mkubwa wa kuendelea kuwa madarakani.





## Waziri atoa somo kilimo cha mboga

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amewataka wakulima wa mboga kitumia majisafi na salama ili kulinda afya za walaji.

Kauli hiyo aliitoa wakati akizindua mradi wa mafunzo ya kuimarisha uwezo na ujuzi katika kilimo cha mboga unaotekelezwa na Baraza la Ufundi (Nacte) kwa ushirikiano na Serikali ya Uholanzi.

Alisema kilimo hicho wakati mwingine hakizingatii afya ya mlaji kwa kutumia viuatilifu vinavyohatarisha afya ya mtumiaji.

"Watu wanakosa mboga za uhakika kutokana na wakati mwingine maji yanayotumika kumwagilia mboga si safi na mwisho wa siku watu hawahamsiki kutumia kutokana na kuwa na wasiwasi zimelimwaje," alisema.

Alisema anaamini kupitia mradi huo watazingatia afya na usalama wa watumiaji wa mboga na matunda kwa kuwa ni muhimu kuzingatia katika mazao mbalimbali.

"Nitoe wito katika utekelezaji wa mafunzo haya tuzingatie afya za wateja, kutokana na matumizi haya ya viuatilifu wakati mwingine inawapa hofu watu kutumia mboga hizo," alisema.

Akizungumzia mafunzo hayo, alisema serikali hiyo imetoa ufadhili wa Sh. bilioni 2.5 kugharamia mafunzo ya kilimo hicho na matunda na itasaidia kuimarisha na kuchangia katika maendeleo.

Profesa Ndalichako alisema mafunzo ya ufundi stadi ni nyenzo muhimu ya kufikia uchumi wa viwanda kwa kuwa na wataalamu ambao wataweza kufanya kazi kwenye viwanda.

"Kilimo ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi lazima kiwe cha kisasa na kuondokana na dhana ya kumiliki heka nyingi na kukifanya kilimo kuwa hakina tija kwa kutumia nguvu zaidi kuliko maarifa," alisema.

Alieleza mradi huo utatekelezwa na Nacte kwa kushirikiana na chuo cha MSM cha Uholanzi na kimebobea katika sekta hiyo hivyo, Watanzania watumie fursa hiyo kupaisha kilimo hicho kwa kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa mradi.

"Tumeanza na vyuo vitatu lakini tunaweza kupeleka elimu hii kwa vyuo vingine, na pia wanafunzi watajifunza kwa vitendo maana tumezoea kuona mtu anasomea kilimo cha kahawa au korosho, lakini hajui hata mti unafafanaje, tunataka wajifunze kwa vitendo," alisema.

Pamoja hayo, alisema pamoja na kuimarishwa kwa kilimo hicho pia wasaidiwe kupata masoko ili kuchangia uchumi wa nchi kama ilivyo kwa Uholanzi.

"Na mimi nimeanzisha shamba la mboga nitakuwa mwanafunzi wenu, ni kweli tunafanya kilimo kama 'hobby' lakini wenzetu ni uchumi wanaongeza pato la taifa," alisema.

Katibu Mtendaji wa Nacte, Dk. Adolf Rutayuga, alisema hadi sasa vyuo 530 vya ufundi vimesajiliwa nchini na vinatoa wahitimu zaidi ya laki mbili.

Alisema mwaka 2013 nchi hiyo ilifadhili kwa kutoa Yuro milioni 1.6 kwa lengo la kuboresha elimu ya ufundi na ufadhili huo umeweza kuleta mafanikio makubwa.

# Bilioni 40/- zatengwa kujenga vyuo Veta

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 40 kujenga vyuo vya ufundi (Veta) katika halmashauri 25 nchini.

Fedha hizo zimetangwa katika mwaka huu wa fedha 2019/2020, na kuzitaka halmashauri zitakazo pata fedha hizo kuwatumia mafundi kutoka ndani ya Veta na kuacha tabia ya kuwatafuta wa mitaani. Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, wakati alipokuwa akihutubia katika hafla ya ufunguzi wa kiwanda cha kutengeneza samani kilichopo chini ya chuo cha Veta kanda ya kati.

Ndalichako alisema kuwa kiasi hicho cha fedha kilichotengwa na serikali ni kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo ili kuweza kuwasaidia vijana kupata ujuzi katika ufundi mbalimbali.

"Sh. bilioni 40 zimetengwa na serikali kwa ajili ya ujenzi huo katika halmashauri 25 nchini hivyo ni marufuku vyuo hivi kujengwa na mafundi kutoka mitaani jengeni wenyewe kwani rasilimali watu mnayo,"alisema Ndalichako.

Aliagiza halmashauri hizo kukamilisha ujenzi huo ifikapo Juni 30, mwakani.

Akizungumzia suala la ubadhirifu, alisema kuwa wizara yake haitakuwa tayari kuwafunga wezi wa fedha umma.

"Veta ilikuwa inafuga sana wezi hata ripoti ya Wizara ya Fedha ilionyesha kuwa Veta kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma sasa mimi sitakuwa tayari kuwafuga wezi bali nitawashughulikia na ninaendelea kumwomba kaka yangu Dk. Mpango kuendelea kuleta fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara ya Elimu,"alisema.

Prof. Ndalichako alisema kutumia wajenzi hao kutasaidia kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuliingizia taifa mapato.

"Nitoe wito kwa viongozi mbalimbali wa serikali, mashirika ya dini pamoja na taasisi binafsi kukitumia kiwanda hiki katika kutengeneza samani zenye ubora na gharama nafuu na kuacha tabia ya kuziagiza kutoka nje," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Veta Kanda ya Kati, Ramadhani Mataka, alisema ujenzi wa kiwanda hicho umegharimu zaidi ya Sh. bilioni tatu.

"Lakini fedha zote hizi ambazo zimetumika katika ujenzi wa kiwanda kwa asilimia 100, ni kutoka serikalini," alisema Mataka.



Wanafunzi wa Shule za Fountain Gate Academy (kulia), wakikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa mlezi wa watoto yatima katika Kituo cha Miyuji Cheshire Home, Mtawa Theresia Cosmas, wakati wa kuadhimisha siku ya kutoa inayoadhimishwa na shule hiyo kila mwaka, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jamii ijali yatima isingojee sikukuu

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

JAMII imetakiwa kujitolea mara kwa mara misaada kwa ajili ya watoto yatima na si kusubiri kipindi cha sikukuu ili wajione ni sehemu ya jamii.

Wito huo ulitolewa na Mlezi wa Kituo cha Jumba la Matumaini, Sister Aurea Vincent, alipokuwa akizungumza baada ya kupokea msaada wa vitu mbalimbali kutoka kwa wanafunzi wa shule za Fountain Gate za jijini Dodoma.

Wanafunzi hao walitoa misaada ya vitu mbalimbali kwa watoto wanaoishi kwenye vituo viwili ambavyo ni Jumba la Matumaini kinacholea yatima na Miyuji Cheshire Home kinacholea watoto wenye ulemavu wa akili.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Sister Aurea, alishukuru kwa wanafunzi hao kuwajali watoto hao kipindi hiki, huku akisema ni muhimu wakawa wanakumbukwa siku zote na si kipindi cha mwisho wa mwaka au sikukuu.

"Watu wengi huja kutuona katika kipindi cha mwisho wa mwaka hasa mwezi Desemba, hivyo ujio wenu kwa wakati huu umekuwa muhimu sana kwetu," alisema.

Aliwaambia kuwa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wanamahitaji sawa na wengine na wana haki ya kuishi katika mazingira bora na salama, hivyo jamii ione umuhimu wa kuwalinda watoto wasijiingize kwenye mazingira hatarishi.

Aidha, Sister Theresia Cosmas ambaye ni mlezi wa watoto katika Kituo cha Miyuji Cheshire Home, aliwashukuru kwa msaada wa mahitaji kwa watoto wao na kuomba jamii iige mfano wa shule hiyo.

Awali, akikabidhi msaada huo, Meneja wa Fountain Gate Foundation, Janeth Chijanga, alisema taasisi hiyo imetenga siku maalum ya kutoa msaada kwa wahitaji ambayo hufanyika kila mwaka.

"Hatua hii ni kurudisha sehemu ya kile tunachopata kwa jamii na pia tunawafundisha watoto matendo ya huruma," alisema.

Aliwaasa wanafunzi kujenga moyo wa kujitolea na kusaidia wenye mahitaji.



HABARI ZANZIBAR

# Ujenzi wa jengo la kihistoria waiva

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema taratibu za kuanza kwa ujenzi wa jengo la Beit-al-Jaib uko katika hatua za mwisho baada ya kupata kibali kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kujua maendeleo ya jengo hilo la kihistoria.

Alisema hatua zote muhimu zimekamilika ikiwamo fedha za ujenzi ambazo zimetolewa na Serikali ya Sultani wa Oman.

Talib alisema hatua zote zimefikiwa katika ujenzi wa jengo hilo ikiwamo kupata kibali kutoka Unesco, ambayo ndiyo inayoshughulikia ujenzi wa majengo ya kale.

Alisema jengo la Ngome Kongwe limo katika orodha ya urithi wa mambo ya kale ambalo linatambuliwa kimataifa.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba ujenzi wa jengo la Ngome Kongwe uko katika hatua za mwisho za kuanza, tayari tumepata kibali kutoka Unesco," alisema.

Aliyataja masharti yaliyowekwa na Unesco ambayo yanatakiwa kutekelezwa ni pamoja na ukarabati huo usibadilishe haiba na usanifu wa michoro ya jengo hilo.

"Tumepewa masharti katika ukarabati wa jengo la Beit-Al -Jaib ambao unatakiwa kuzingatia sifa na vigezo vya majengo ya kale bila kupoteza haiba yake ya asili," alisema.

Jengo la Beit-al-Jaib limebeba historia ya majengo ya kale yaliyoko katika Mji Mkongwe Zanzibar ambalo lilijengwa mwaka 1883 chini ya utawala wa mfalme wa pili wa Oman, Barghashi bin Said.

Oman imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa na kulirudisha jengo hilo katika hadhi yake na heshima ikiwa ndio utambulisho wa Mji Mkongwe na Zanzibar kwa ujumla.




Meneja Masoko wa Taasisi ya Emerson, Katia Wellving (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya tamasha la vyakula vya asili litakalofanyia Zanzibar hivi karibuni. Kushoto ni mmoja wa waandaaji wa tamasha hilo, Shabnam Salim. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wapongeza safari ya Shein Uarabuni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameipongeza ziara ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, katika nchi za Falme za Kiarabu ambayo imeleta neema kubwa kwa vijana na sekta ya afya.

Mwakilishi wa Chakechake, Suleiman Sarhani, alisema ziara ya Dk. Shein imeleta neema kubwa kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba kupata matumaini ya kujengwa kwa hospitali ya kisasa huko Wete, Pemba.

Alisema ukosefu wa hospitali ya kisasa ya rufani kwa wananchi wa Jimbo la Wete sasa umepata ufumbuzi wa kudumu kutokana na makubaliano ya kuanza kwa ujenzi huo.

"Tumefarajika sana na ziara ya Rais wa Zanzibar katika nchi za Kiarabu. Makubaliano yamefikiwa ya ujenzi wa hospitali ya kisasa huko Wete ambayo itakuwa na hadhi ya rufani," alisema.

Aidha, Sarhani alisema ujenzi wa hospitali ya kisasa ya Wete pamoja na upanuzi wake, itasaidia kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wa jimbo hilo.

Alisema kwa muda mrefu wananchi wa Wete wanapata matatizo ya kusafiri masafa kwenda mkoani Pemba kwa ajili ya kupata huduma za afya katika Hospitali ya Abdalla Mzee.

"Tunampongeza kwa dhati Rais Ali Mohamed Shein. Ziara yake katika nchi za Kiarabu imeleta faraja kubwa kwa wananchi wa Zanzibar katika sekta ya afya na kukuza vijana," alisema.

Naye Mwakilishi wa Wete, Harusi Said Suleiman, alisema ni faraja kubwa kwa wananchi wa Wete na maeneo mengine ya jirani juu ya kuwapo kwa taarifa za ujenzi wa hospitali ya Wete na upanuzi wake.

"Matunda ya ziara ya Rais Shein nchi za Kiarabu tumeyaona. Matarajio yetu makubwa tunasubiri kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo mkubwa," alisema. Waziri asiye na Wizara Maalumu, Juma Ali Khatib, alimpongeza Rais Shein na kusema ziara zake za nje zimekuwa zikilenga kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

"Tumefarajika na ziara ya Rais Shein katika nchi za Falme za Kiarabu. Tumepata fedha kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujiajiri pamoja na ujenzi wa hospitali ya Wete Pemba," alisema.

Katika ziara ya Rais Shein Umoja wa Falme za Kiarabu (UEA), kupitia Mfuko wa Khalifa, Zanzibar imepata Sh. bilioni 23 kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana kujiajiri.

## Ataka utoaji haki za utendaji kazini

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka watendaji wakuu wa wizara hiyo kuzitumia vyema dhamana walizopewa kwa wafanyakazi ili nao wafanye kazi kwa ufanisi.

Aliyasema hayo wakati alipofungua mafunzo elekezi juu ya upimaji utendaji kazi kwa mfanyakazi na upimaji wa wizara au taasisi juu ya kufikia malengo kwa watendaji wakuu wa wizara katika ukumbi wa wizara hiyo Mazizini, mjini Unguja.

Waziri huyo alisema dhamana walizopewa wakuu hao si kwa kuziendesha wanavyotaka wao, bali ni kwa kufuata sheria, kanuni na misingi ya haki na uwajibikaji.

Riziki alisema mafunzo hayo yatawasaidia wakuu hao katika kuwakumbusha wajibu wao juu ya kila mtendaji, kufahamu stahiki na haki kwa walio chini yake.

Alisema kuna umuhimu wa kupatiwa tena mafunzo hayo kwa watendaji hasa kwenye suala la namna ya upimaji wa wizara au taasisi katika kufikia malengo kwa kuwa kunaonekana kuwapo kwa uelewa mdogo juu ya suala hilo.

Pembe aliwataka kila mmoja kusimama vyema kwa kutimiza majukumu yake na kutenda haki kwa mfanyakazi bila kuwa na muhali, upendeleo katika kazi kwa kuwa inaweza kuwanyima wengine haki zao.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idrisa Muslim Hijja, alisema mafunzo hayo yamefanyika kwa lengo la kutekeleza agizo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar la kuitaka kila wizara kufanya mafunzo hayo pamoja na kuhakikisha kila mtendaji anawajibika kwa kupimwa utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Akiwasilisha mada juu ya upimaji wa wizara au taasisi katika kufikia malengo, Ofisa Mipango kutoka Tume ya Mipango, Omar Makame Juma, alisema kuwajibika kwa watendaji ni lazima kufuata kanuni na sheria zilizopo ili kufikia malengo yaliyowekwa na taasisi husika.

Alisema asilimia 75 ya taasisi duniani hazifikii malengo yake kutokana na kukosekana kwa maandalizi mazuri ya mipango mikakati juu taasisi zao.

Kwa upande wao washiriki wa mafunzo hayo waliwapongeza wawasilishaji wa mada na wameshauri kuwekwa utaratibu mzuri wakati wanapowasilisha maada zao ili kila mshiriki aweze kupata taaluma kama lengo la kufanyika mafunzo hayo lilivyokusudiwa.

# Wavuvi waibua kilio usalama ziwani

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

BAADHI ya wamiliki wa mitumbwi na wavuvi wa mwalo wa Butuja wilayani Ilemela mkoani Mwanza, wameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani kuimarisha ulinzi na usalama ziwani.

Hali hiyo imetokana na kuwapo kwa madai ya kuvamiwa, kuuawa na kunyang'anywa samaki kwa baadhi ya wavuvi wakiwamo wa mwalo huo ambao wanaofanya shughuli katika Ziwa Victoria na watu wanaosadikiwa kuwa majambazi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza, mfanyabiashara wa samaki mwalo wa Butuja, mmiliki wa mitumbwi ya Mv. Tunda Abel Kaitira, alisema mitubwi mingi na matajiri wameshatoa taarifa kwa ngazi za chini, lakini hakuna kilichofanyika.

"Tunazidi kuumia, watu wanakufa, mali zinateketea sisi tutakuwa katika mazingira ya aina gani?" Alihoji na kuendelea:

"Katika kukomesha vitendo hivyo Waziri wa Mambo ya Ndani anapaswa kutusaidia kuwabana baadhi ya askari wanaowanyang'a wavuvi samaki bila kufuata utaratibu, ikiwezekana serikali kupitia wizara hiyo iweke operesheni ya jeshi ambayo itasaidia kuimarisha ulinzi na usalama ziwani huku wavuvi wakivua kwa amani."

"Kuna tetesi kuwa wapo baadhi ya wavuvi ambao ni majambazi wanaingia majini na kufanya vitendo hivyo, tusaidiwe ili waweze kupatikana hata kama kuna matajiri wanahusika," alisema Kaitira.

Mwenyekiti wa Utunzaji wa Viumbe Hai ndani ya mita 60 mwambao mwa ziwa (BMU) mwalo wa Butuja, Dickson Maila, alisema ili kuimarisha ulinzi na usalama ziwani, aliiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuongeza doria kwani zilizopo ni chache, huku wavuvi wakipatiwa elimu ya kutambua mipaka ziwani inayotenganisha nchi moja na nyingine pamoja na matumizi ya dira ili kutambua mwelekeo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na Nipashe, alisema jambo la ulinzi na usalama ziwani ni mtambuka hasa kwa vyombo vya ulinzi na usalama, na anashukuru vyombo hivyo vinafanya kazi kubwa na nzuri, lakini wanaendelea katika kuhimizana na kufanya zaidi ili kuwasaidia Watanzania wanaokutana na madhira mbalimbali wawapo majini.

# Wauguzi na upimaji afya

**Happy Severine, BARIADI**

CHAMA cha wauguzi Tanzania kimetoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Simiyu kujitokeza kwa wingi kupima na kujua afya zao kwani huduma zote za vipimo muhimu zitatolewa bure kwa kipindi cha wiki nzima.

Wito huo ulitolewa jana na Rais wa chama hicho, Paul Magesa, wakati wa mkutano mkuu wa 47 wa chama hicho, unaoendelea kufanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Kusekwa Mjini Bariadi.

Magesa alisema katika Mkutano wao Mkuu wa 47 ambao kitaifa unafanyika mkoani Simiyu wameamua kutumia fursa hiyo kutoa elimu na huduma za upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi, maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) pamoja na magonjwa yasiyoambukizwa kwa wananchi ikiwa ni sehemu ya kutathmini utendaji kazi na changamoto zilizopo katika sekta ya afya.

Alisema ni wakati sahihi kwa wananchi wa Simiyu kujitokeza kwa wingi kupima afya zao, ili waweze kubaini maendeleo ya afya zao na kupatiwa matibabu sahihi kabla magonjwa hayo hayajawa sugu ndani ya miili yao.

Alisema kwa kipindi kifupi cha jana jumla ya wananchi 300 wamejitokeza kupima afya zao, huku akieleza kuwa idadi hiyo ni ndogo hivyo wananchi wengi wajitokeze zaidi ili waweze kupata huduma hiyo.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Festo John, alisema wauguzi wana jukumu kubwa katika afya ya mwanadamu, hivyo ni vema sasa wakajitafakari katika utendaji wao wa kazi ikiwa sambamba na serikali kuzidi kuboresha mazingira yao ya utendaji wao wa kazi.

Alisema ingawa takwimu za wauguzi mkoani Simiyu kuwa chini, lakini wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuwahudumia wagonjwa bila kuchoka.

Aliongeza kuwa kwa Mkoa wa Simiyu, idadi ya wauguzi ni ndogo kwani waliopo ni 617 tu, wakati mahitaji yanayohitajika ni wauguzi 1,500.

Dk. John aliongeza kuwa katika mkutano huo, wenye kauli mbiu ya wauguzi ni sauti inayoongoza, afya ni haki ya binadamu itasaidia kuboresha utendaji wa kazi uliotukuka.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa (wa pili kulia), akisalimiana na Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Kusini, Jeniffer Tondi, wakati alipotembelewa ofisini kwake kwa mazungumzo juu ya kampeni maalum ya uwezeshaji sekta ya kilimo inayoendeshwa na Benki ya CRDB. Wengine kutoka kulia ni Ofisa Mkuu wa Biashara wa Kanda ya Kusini, Leevan Maro, Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa benki hiyo, Kilo Mgaya na Ofisa Uhusiano, Emmanuel Tupeligwe wote kutoka Benki ya CRDB.

# KACU yafunga mjadala tumbaku ya ziada

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

CHAMA Kikuu cha Ushirika wilayani Kahama mkoani Shinyanga (KACU), kimesema hakutakuwapo na kikao chochote cha kujadili tumbaku ya ziada inayozalishwa nje ya mkataba katika msimu 2019/2020.

Kauli hiyo ilitolewa jana mjini Kahama na Mwenyekiti wa (KACU), Emanuel Charahani, wakati akizungumzia kuhusu namna wanavyokabiliana na tumbaku iliyozalishwa nje ya mkataba katika msimu wa mwaka jana.

Charahani aliwataka wakulima wa tumbaku kulima kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa, ambapo kwa Wilaya ya Kahama jumla ya kilo milioni 6.3 za tumbaku zinatarajiwa kuzalishwa ndani ya mkataba mwaka 2019/20120.

"Tayari uzalishaji wa kilo 41,000,000 zinahitajika kuzalishwa kwa ajili ya msimu ujao wa tumbaku na kwa hapa Kahama tuna kilo 6,000,000 ambazo zimegawiwa kwenye kila chama cha msingi na wakulima wameelekezwa namna ya kuzizalisha, hivyo mwaka huu hakuna vikao vya kujadili tumbaku iliyozalishwa nje ya mkataba," alisema Charahani.

Aliwataka viongozi wa vyama vya msingi wasimamie wakulima namna ya kuzalisha tumbaku yenye tija na si kuwaruhusu wakulima kulima zao hilo zaidi ya kile wameelekezwa na viongozi wao ili kuepuka kuwapo kwa tumbaku ambayo haitanunuliwa na kampuni za ununuzi zilizoingia mkataba na KACU.

Katika hatua nyingine Charahani alisema zaidi ya kilo milioni mbili za tumbaku zimebaki kwa wakulima kutokana na kuzalishwa nje ya mkataba katika msimu wa 2018/2019, ambapo wanatarajia kuanza ziara katika maeneo ya wakulima ili kutoa elimu ya kuzingatia kilimo cha mkataba.

Tumbaku ni miongoni mwa mazao ya kibiashara ambapo kwa Wilaya ya Kahama idadi kubwa ya wakulima inatoka katika Halmashauri ya Ushetu.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Trump azidi kuandamwa

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS Donald Trump wa Marekani amewashambulia wabunge wa chama cha Democratic akiwatuhumu kuchochea uchunguzi dhidi yake baada ya kutoa hati ya kumtaka wakili wake binafsi kutoa nyaraka za mawasiliano na Ukraine.

Wakati Trump akimshambulia vikali Mbunge wa chama cha Democratic, Adam Schiff na kusema anatakiwa kukamatwa kwa kile alichokitaja "uhaini", Australia nayo imethibitisha kwamba rais huyo hivi karibuni amewasiliana na serikali yake.

Ilieleza kuwa ameomba Waziri Mkuu wa nchi hiyo na viongozi wa mataifa mengine kumsaidia mwanasheria mkuu wa Marekani William Barr kupata taarifa zitakazomsaidia kuufanya uchunguzi wa mshauri maalumu Robert Muller kutiliwa shaka.

Robert Muller, aliongoza uchunguzi wa uingiliaji wa Urusi kwenye uchaguzi mkuu wa Marekani wa mwaka 2016.

**Ninapima njia mbadala. Nitakusanya ushahidi wangu wote pamoja na mawasiliano ya ujumbe. Sijui, ikiwa wataniruhusu nitumie video na mawasiliano niliyorekodi.**

Trump pia hakuacha kuwashambulia watoa siri ambao madai yao yalihusu mawasiliano yake ya simu na Rais wa Ukraine Volodymir Zelensky Julai, mwaka huu, yamesababisha kuanzishwa kwa uchunguzi wa bunge linalodhibitiwa na chama cha Democratic wa kumshtaki.

Mwanasheria wake binafsi, Rudy Giulini, anatajwa kuwa sehemu muhimu ya juhudi za kuiomba Ukraine kufanya uchunguzi dhidi ya familia ya mpinzani mkuu wa Trump kwenye uchaguzi ujao Joe Biden, ambayo haijatuhumiwa kwa kufanya kosa.

Hapo jana alipofanyiwa mahojiano na kituo cha utangazaji cha Fox, kuhusiana na hati hiyo ya bunge, Giuliani alisema anatafakari hatua atakazozichukua:

"Ninapima njia mbadala. Nitakusanya ushahidi wangu wote pamoja na mawasiliano ya ujumbe. Sijui, ikiwa wataniruhusu nitumie video na mawasiliano niliyorekodi. Nilikusanya ushahidi huu wote kabla ya uchunguzi wa Mueller kumalizika, kwa hivyo ilikuwa wazi kuwa jukumu langu kama Wakili wa Rais, mkutano wa mwisho ambao Waukraine waliuitisha, nililifanya wakati uchunguzi ulipomalizika."

Mwenyekiti wa kamati ya bunge ya masuala ya kijasusi, Adam Schiff, pamoja na wenyeviti wa kamati nyingine mbili zinazoongozwa na Wademocratic zimetoa hati hiyo kwa Giuliani na kumpa hadi Oktoba 15 kuwa amewasilisha nyaraka hizo.



Rais wa Marekani Donald Trump (kulia) na Waziri Mkuu wa Australia, Scott Morrison. **PICHA: AFP**

Huko Australia, msemaji wa serikali amethibitisha alipozungumza na kituo cha utangazaji cha ABC kwamba Trump aliwasiliana na Waziri Mkuu Scott Marrison kuomba kumsaidia mwanasheria mkuu Bill Barr kupata taarifa zinazohusiana na uchunguzi wa Muller.

Kulingana na gazeti la New York Times, lililowanukuu maofisa wawili wa Marekani ambao hawakutambulishwa, nakala ya maandishi ya mawasiliano hayo ilitolewa tu kwa kundi dogo la wasaidizi wa Trump ambao wanataka udhibiti mkali wa mawasiliano hayo. Australia imesema iko tayari wakati wote kusaidia juhudi za kufungua njia kwenye uchunguzi wa masuala kadhaa na Waziri Mkuu huyo pia alikubali kufanya hivyo.

Uchunguzi mpya wa maoni uliochapishwa jana umeonyesha kwamba Wamarekani wamegawika juu ya ama kuunga mkono mashtaka dhidi ya Trump ama kujiweka pembeni. **DW**

## 1,000 kurejea Burundi kesho

**BUJUMBURA,** Burundi

KUANZIA jana Jumanne serikali ya Burundi imekubali kuwa kundi la kwanza la wakimbizi wake walioko nchini Tanzania watarejea nyumbani Alhamisi wiki hii.

Hatua hiyo ni sehemu ya mpango wa serikali za nchi mbili kuwarudisha wakimbizi hao makwao. Kwa mujibu wa maofisa wa Burundi waliolieleza Shirika la Habari la Reuters.

Walisema jana Oktoba mosi, ndiyo tarehe iliyotolewa na serikali ya Tanzania kuwarudisha wakimbizi 2,000 wa Burundi nyumbani kutoka kwenye kambi za wakimbizi nchini Tanzania.

Takriba wakimbizi 1,000 wako katika kundi la kwanza litakalorejea nyumbani, alisema Meneja Mkuu wa shughuli ya kuwarejesha wakimbizi nchini Burundi Nestor Bimenyimana, akisema kuwa mchakato huo ni wa "hiyari".

Burundi na Tanzania zilikubaliana mwezi Agosti mwaka huu kwamba mchakato wa kuwarudisha nyumbani wakimbizi zaidi ya 2,000 wa Burundi waliopo nchini Tanzania utaanza Oktoba 1, jambo lililoibua hofu ya kulazimishwa kurudi nyumbani miongoni mwa wale waliovuka mpaka kuepuka ghasia.

Wakimbizi wamekuwa wakieleza hofu yao, huku utaratibu huo ukitarajiwa kuanza.

"Tunahofia wakati wowote watatushtukizia na kutulazimisha turudi Burundi." alisema Jean Bizimana, mkimbizi katika kambi ya Nduta iliyopo katika eneo la kaskazini magharibi ya Kigoma.

Mnamo Agosti, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Tanzania Kangi Lugola, alitangaza kuwa wakimbizi 2,000 watarudishwa Burundi kufikia Oktoba mosi mwaka huu ambayo ni jana.

Lugola alisema majadiliano hayo hayawahusu wakimbizi wenyewe moja kwa moja kwa sababu "hawakuja Tanzania kwa hiari yao".

"Tukisubiri urudi nchini kwako kwa hiari tutakuwa tunategemea hiari yako wewe binafsi, lakini sisi tunaangalia sababu iliyokufanya utoroke nchi yako ilikuwa hoja ya amani na usalama," alisema. **BBC**



Sehemu ya Kikosi cha Jeshi la China kilichoshiriki gwaride la kijeshi jana. **PICHA: REUTERS**

## China yatamba na uwezo kijeshi

**BEIJING,** China

MAMILIONI ya watu nchini China na maeneo mengine duniani jana yaliangalia mubashara kupitia televisheni za mtandaoni, gwaride la maadhimisho ya miaka 70 ya nchi hiyo.

Televisheni ya taifa ya China ya CCTV ilianza matangazo hayo ya maadhimisho ya miaka 70 kwa kauli mbiu ya kuwatakia maisha marefu raia wa taifa hilo.

Maadhimisho hayo ya aina yake yalipambwa na gwaride la kijeshi la askari 188.

Aidha, wanajeshi hao walitarajiwa pia kurusha ndege 150 jana na tayari nyingine zimeanza kupaa angani.

Wananchi wanaofuatilia kwa karibu maadhimisho hayo huku wakijipiga picha za ukumbusho wa siku hiyo muhimu katika historia ya nchi yao.

Silaha mpya za DF-41 ambazo wachambuzi wanasema kuwa zimelengwa kutumika sehemu yoyote duniani nazo zilionekana.

Wakati wote wa maadhimisho ulinzi mkali ulitawala muda wote wakati wa shughuli hizi zikiendelea katika mitaa mbalimbali nchini humo.

China ikiwa na sababu kubwa na ya msingi ya kusherehekea siku hiyo baada ya kupita hatua ya kuwa taifa maskini na sasa ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na uchumi mkubwa na maendeleo duniani. **BBC**

# Mambo saba pasua kichwa Mkurugenzi mpya wa NEC

INATOKA UK. 2

kuingiza majina ya watakaofikisha umri wa miaka 18 ifikapo Oktoba 25, mwakani, waliopoteza vitambulisho vya kupigia kura na waliohama maeneo.

Kwa mujibu wa utaratibu, baada ya kazi hiyo kukamilika, tume itakuwa na wajibu wa kuchapisha daftari la awali ambalo litabandikwa kwenye vituo kwa ajili ya wapigakura kuhakiki majina yao kabla ya kutengenezwa kwa daftari la mwisho.

**VIFAA KUPIGIA KURA**

Mwaka 2014, NEC ilieleza kupokea Sh. bilioni 290 za ununuzi wa vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya uchaguzi mkuu kwa mfumo wa Biometric Voter Registration (BVR).

Kwa mara ya kwanza Tanzania ilifanya uchaguzi kwa mfumo huo mwaka 2015 kutoka kwneye mfumo wa awali wa matumizi ya daftari la kudumu la wapigakura.

Katika uchaguzi wa mwaka 2015, BVR zilianza kutumika kwa mara ya kwanza, huku kukiwa na changamoto mbalimbali kama mashine kutokufanya kazi kwa wakati na kuwa na foleni ndefu.

Nyingine ilikuwa uchache wa mashine hizo na kusababisha wananchi kukaa muda mrefu kwenye vituo vya kupigia kura na wengine kukosa haki ya kupiga kura kutokana na misururu kirefu au muda wa kufunga kituo kufika.

Wakati wa uzinduzi wa daftari hilo mjini Moshi, NEC ilisema kutakuwa na vifaa vya BVR 3,000 vitakavyotumika kwenye mchakato huo.

**MALALAMIKO**

Kila wakati vyama vya upinzani vimeibua hoja ya kueleza kuwa Tume ya Uchaguzi si huru kwa kuwa mtendaji wake mkuu anateuliwa na Rais ambaye anatokana na Chama Cha Mapinduzi na yuko madarakani.

Hivi Karibuni, Kiongozi Mkuu wa chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, walisema uchaguzi hauwezi kuwa huru na haki iwapo NEC itaendelea kuwa ilivyo sasa.

Pia walisema kuna ulazima kufanya



Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera.

marekebisho ya katiba na kuwa na tume huru ambayo mtendaji mkuu, mwenyekiti wake na makamishna hawateuliwi na Rais.

Jambo hili liliibuka mwaka 2014 baada ya mkwamo wa katiba mpya kutokea kwa upinzani kupendekeza yafanyike marekebisho kwenye Katiba ya mwaka 1977 kwa kuhakikisha muundo wa tume unabadilishwa.

**MAPINGAMIZI**

Nyakati za uchaguzi vyama huruhusiwa kwa mujibu wa sheria kuwasilisha pingamizi la wagombea na mawakala. NEC inatakiwa kushughulikia hilo na kutoa majibu kwa wakati, ikiwamo rufani za wagombea wa udiwani, ubunge na urais.

**SAKATA LA MA-DED**

Mei 10, mwaka huu, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, ilitoa uamuzi kuwa wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa hawapaswi kusimamia usimamizi kwa vile hawako huru.

Uamuzi huo ulitokana na kesi namba 6 ya mwaka 2018, iliyofunguliwa na watetezi na wanaharakati wa haki za binadamu na demokrasia kwa kushirikiana na vyama vya siasa vilivyowakilishwa na mwanachama wa Chadema, Bob Wangwe, dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Kwa msingi huo, Nec itawajibika kuwa na wafanyakazi watakaosimamia uchaguzi huo kwenye maeneo mbalimbali tofauti na ilivyozoeleka kwa miaka miaka mingi ukisimamiwa na wakurugenzi hao.

**BAJETI FINYU**

Kutokana na uamuzi wa kuwaengua wakurugenzi wa halmashauri nchini kusimamia uchaguzi, Tume inalazimika kuajiri watu wa muda wa kufanya kazi hiyo kwenye maeneo mbalimbali, jambo ambalo huenda likaongeza bajeti itakayohitajika kwa ajili ya uchaguzi huo.

**UTEUZI NA UHAMISHO**

Juzi Rais Magufuli amefanya uteuzi wa wakurugenzi 10 watakaokwenda kwenye Halmashauri za Manispaa na wilaya mbalimbali na kuwahamisha wengine wawili kwenye vituo vyao vya kazi. Pia alimteua Mkuu mpya wa Itifaki.

Walioteuliwa na halmashauri zao mpya kwenye mabano ni Ndaki Muhuli (Siha-Kilimanjaro), Rehema Bwasi (Manispaa Morogoro), Sheillah Lukuba (Wilaya Morogoro) na Mohamed Mavura (Kibiti).

Wengine ni Ezekiel Magehema (Kyela), Diana Zacharia (Butiama), Hanji Godigodi (Mbozi), Saidi Magaro (Uyui), Hawa Mposi (Malinyi), Godwin Chacha (Rombo).

Waliohamishwa vituo ni John Magalula kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwenda Itigi mkoani Singida, Advera Ndabagoye, kutoka Kibiti Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Sambamba na wakurugenzi hao. Rais Magufuli alimteua Kanali Wilbert Ibuge kuwa Balozi na Mkuu wa Itifaki katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuchukua nafasi ya Balozi Grace Martin ambaye atapangiwa majukumu mengine ya kiubalozi.

***Imeandikwa na Salome Kitomari, Romana Mallya na Mary Geofrey***

## Mtoto huyu amepotea

**Na Mary Geofrey**

MTOTO Safiuna Chichiri Mruma (9), anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao tangu Septemba 26, mwaka huu.

Babu wa mtoto huyo, Hamidu Mruma, aliiambia Nipashe jana kuwa, mjukuu wake, alitoweka nyumbani kwao maeneo ya Ubungo Kibo, muda mfupi baada ya kutoka madrasa katika msikiti ulio jirani na wanapoishi.

"Ilikuwa siku ya Alhamisi alipotoka madrasa na wenzie hakufika nyumbani, tukamuulizia bila ya mafanikio, ilipofika saa 2:00 usiku tukatangaza msikitini ili kama yupo sehemu anacheza atarudi nyumbani," Mruma alisema.



Alisema walimtafuta hadi Shule ya Msingi Kimara Baruti ambako anasoma darasa la tatu bila ya mafanikio, mwalimu aliwaeleza kuwa walimuonya kutokana na tabia yake ya kutomaliza kazi.

Mruma alisema waliendelea kumtafuta kwa ndugu na jamaa wanapoishi ndugu zake bila ya mafanikio.

Alisema baada ya kukaa hadi Ijumaa bila ya mafanikio waliamua kwenda kuripoti Kituo cha Polisi Kimara na kupewa RB namba **KIM/RB/5164/2019**.

Aliomba mtu yeyote atakayemuona atoe taarifa katika Kituo cha Polisi kilicho karibu au kupiga simu namba **0713 414731**, **0653 304141** na **0686 371113**.

# Hakimu, mwanasheria wa Tanapa wamwangukia DPP

INATOKA UK. 2

Businness Coperation (OBC), wameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kuwakumbusha mashtaka yanayowakabili, ili waandike barua kwenda kwa DPP kukiri mashtaka yanayowakabili.

Waliowasilisha ombi hilo ni Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali.

Watu hao wanadaiwa kufanya kazi nchini bila vibali, huku Lesian Mollel (59) ambaye ni mkurugenzi wa OBC akikabiliwa na mshataka 37 ya kuajiri raia wa kigeni, bila kuwa na vibali kwa mujibu wa sheria za nchi za kutoa ajira kwa wageni.

Katika kesi hiyo Mollel ambaye ni mshtakiwa wa kwanza, alishindwa kufika mahakamani hapo kutokana na kutokuwapo kwa maombi ya kibali ya kumwondoa mahabusu katika Gereza la Kisongo kwenda mahakamani. Maombi hayo yaliwasilishwa mahakamani hapo jana na Wakili wa Utetezi Steven Mosha mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Rose Ngoka.

Baada ya maelezo hayo, Wakili wa Jamuhuri, Njiro, alieleza mahakama kuwa upelelezi wa shauri hilo unaendelea na kwamba hataweza kuwakumbusha watuhumiwa mashtaka yanayowakabili kwa kuwa jalada limepelekwa kwa DPP.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Ngoka aliuhoji upande wa utetezi kama una hoja dhidi ya maelezo yaliyotolewa na upande wa Jamhuri na kujibu kuwa hauna pingamizi.

Kutokana na majibu hayo, hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 16, mwaka huu, na kwamba watuhumiwa hao raia wa kigeni dhamana yao inaendelea.

**KABENDERA NAYE NDANI**

Siku moja baada ya Rais John Magufuli kuongeza siku saba kwa washtakiwa wa makosa ya uhujumu uchumi, ambao hawajawasilisha maombi yao, Mwandishi wa Habari Erick Kabendera, anayekabiliwa na kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, amejitokeza kuomba radhi.

Ombi hilo lilitolewa jana na Wakili Jebra Kambole kwa niaba ya Kabendera, baada ya mwandishi huyo kupandishwa tena kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kufuatia makosa matatu yanayomkabili.

Mwandishi wa habari huyo alipandishwa kizimbani kwa madai ya kuongoza kundi la uhalifu kwa lengo la kupata faida au manufaa mengine, kutokulipa kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya zaidi ya Sh. milioni 173.2 na utakatishaji wa fedha kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 173.24.

Wakili Jebra alidai Kabendera amemwomba radhi Rais Magufuli akieleza kwamba kama katika utekelezaji wa majukumu yake ya uanahabari kuna eneo alifanya makosa au aliteleza, amsamehe ili awe huru. Aidha, Wakili Jebra alisema Kabendera yuko tayari kufanya jambo lolote, ili kulinda uhuru na usalama wake.

Kabendera, mwandishi wa habari za uchunguzi ndani na nje ya nchi, alichukuliwa na Jeshi la Polisi nyumbani kwake Mbweni, jijini Dar es Salaam Julai 26, mwaka huu, kabla ya kufikishwa mahakamani.

Septemba 22, mwaka huu, Rais Magufuli alipokuwa akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua, alitangaza siku saba kwa watuhumiwa wa mashtaka ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha ambao watakuwa tayari kukiri makosa na kulipa fedha wanazodaiwa kuachiwa.

Siku saba ilikuwa kuanzia Septemba 23 hadi 28, 2019 na watuhumiwa hao walitakiwa kuwasilisha maombi yao kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Tanzania (DPP).

Juzi Rais Magufuli alipokea majina ya watuhumiwa uhujumu uchumi 467 ambao waliandika barua ya kuomba radhi na wanatarajiwa kuridisha Sh. bilioni 107.8 na kuongeza siku nyingine saba.

***Imeandikwa na Cynthia Mlolezi, Arusha na Mary Geofrey, Dar***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**WARDA S. AMOUR** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1599/0148** kilichotolewa na BAOBAB SEKONDARI mwaka 2016 pamoja na Result Slip. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi IV: **DAR/GOG/RB/302903/2019.** Taarifa ya polisi Result slip: **DAR/GOG/RB/302937/2019.**

6154440702


## KUPOTEA KWA CHETI



**Hajiri Seph Ramadhani** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4122-0014** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika Shule ya Sekondari Tumaini. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/URA/RB/342487/2019**

115440902

## KUPOTEA KWA CHETI




Valentino G. Mwalo anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1757-0569 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari Bendel Memorial.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: 99108101272224

115441602

## KUPOTEA KWA CHETI



**Monica Kuzilwa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0377/0098 kilichotolewa na Barza la Mithihani la Taifa mwaka 1990 katika Shule ya Sekondari Makongo.

Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/OST/RB/241463/2019

114525202

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

YUSUPH SINGANO MWANYANGE anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 252 AAC aina ya T BETTER rangi nyekundu.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi
MBE/MBE/RB/345192/2019.

115441402

## KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**ISAACK MICHAEL KABOGO** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zilizokuwa na namba za usajili T 411 BNU yenye chasis namba 04475890 na injini namba 6163632, T 843 AMD yenye chasis namba FRR22L23003863 na injini namba 6HH1232000 na T 239 DLA chasis namba LJRP13372F4009041.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:
**IR/TR/RB/2567/2019**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;187/2019

Ombi la SOPHIA RAMADHANI MBARAKA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ATHUMAN RAMADHANI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/09/2019.



115440602

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 226/2018**

**EVANCE JOHN MOSHA..............................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. PETER H. KAVISHE
2. ASIA AMIRI HANYA
3. HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA
4. TWINS AUCTION MART & CO. LTD……WAJIBU MAOMBI

### WITO KUITWA SHAURINI

Mjibu maombi wa pili hapo juu unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 8/10/2018 saa 2:30 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi. Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo name na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 25/9/2019.



115439902

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**REGINA GILBERT LIMBUMBA** Anatangaza kupotelewa na hati ya nyumba yenye namba 75 BLOCK D TUNGI Iliyoko ktk manispaa ya MOROGORO- TITTLE NO.48301.

Yeyote atakae iona hati hiyo ya nyumba anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi;

**MOR/MOR/RB/57867/2019.**

215440202


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# GUARDIOLA: MASHABIKI WANATAKA UBINGWA UEFA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini Manchester City inatakiwa kuwapa raha zaidi mashabiki wake kwa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

City jana Jumanne ilicheza dhidi ya vinara wa Kundi C kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya, Dinamo Zagreb.

Kikosi hicho cha Guardiola kilishinda mechi tano za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na safari hii wanajipanga kuhakikisha wanalitwaa taji hilo.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona, Guardiola ana matumaini kwamba, mtazamo wa mashabiki wa klabu hiyo utabadilika kama wakiweza kulitwaa taji hilo la Ulaya, baada ya kulibeba lile la Ligi Kuu ya England.

"Huo ndio ukweli wa klabu yetu. Utafanyaje? Wape raha na wanajua umuhimu wa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Guardiola.

"Nafikiri mwanzo, kizazi kilichopita hakikuwapo hapa, lakini jambo la msingi zaidi ni kuhakikisha tunashinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kule Liverpool na Manchester United wana uzoefu wa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, wamezoea kuwa pale.

"Tukiwa nyumbani, kwenye baa, tumekuwa tukiziangalia Liverpool na United. Si kwa miaka michache, lakini kwa miungo kadhaa. Na huo ndio utamaduni wa klabu.

"Nina hisia za kufuata hatua kama hizo. Nisingependa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa kwenye fainali na baadaye kupotea kwa miaka mitano. Hilo haliwezi kuwa sawa.

## VAR inapoteza utamu wa kushangilia - Aubameyang

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang anahisi matumizi ya teknolojia ya maamuzi ya usaidizi wa refa kwa njia ya video (VAR), kwenye Ligi Kuu ya England yanamaanisha kwamba mfungaji hutakiwi kusherehekea bao hadi teknolojia hiyo ithibitishe.

Aubameyang aliiwezesha Arsenal kupata sare ya 1-1 nyumbani kwa Manchester United Jumatatu, akifuta lile la kipindi cha kwanza lililofungwa na Scott McTominay.

Mchezaji huyo raia wa Gabon awali alionekana kama aliotea kabla ya kufunga akitumia vizuri pasi ya Bukayo Saka na kumfunga kiurahisi David de Gea.

Aubameyang hilo lilikuwa bao lake la saba la Ligi Kuu na kumfanya kuwa mchezaji wa kwanza wa Arsenal kufunga mabao mengi zaidi katika mechi saba za Ligi Kuu tangu Dennis Bergkamp alipofanya hivyo msimu wa 1997-98.

Lakini ilitakiwa hadi maamuzi ya VAR baada ya mwamuzi msaidizi wa pembeni kunyanyua kibendera, lakini VAR ilionyesha Harry Maguire alikuwa sambamba na Aubameyang kabla ya Axel Tuanzebe kubutua mpira.

"Bukayo alinipa pasi nzuri, nilikuwa na uhakika kwamba sikuwa nimeotea," alisema Aubameyang akiiambia Sky Sports.

"Nilishangazwa mwamuzi kukataa bao, lakini mara zote nilikuwa najaribu kutaka kufunga.





# 'Klopp ni bora kuliko Guardiola, Pochettino'

**LONDON,** England

CHRISTIAN Ziege anaamini kwamba, Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp anaweza kuchukuliwa kama ndiye kocha bora zaidi duniani kwa sasa.

Klopp aliiongoza Liverpool kushinda taji la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, wakati walipoifunga Tottenham mabao 2-0 kwenye fainali ya michuano hiyo jijini Madrid.

Mafanikio yao yalikuja baada ya kufungwa 3-1 kwenye fainali ya msimu wa 2017-18, huku kikosi hicho cha kocha, Klopp pia kilipitwa pointi moja tu kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England uliochukuliwa na Manchester City msimu uliopita.

Beki wa zamani wa Tottenham, Ziege pia amewataja Pep Guardiola na Mauricio Pochettino, pamoja na yule wa Bayern Munich, Niko Kovac, lakini kwake Klopp kwake ndiye namba moja.

"Nafikiri unatakiwa kuwa makini. Kumtaja kocha bora duniani unatakiwa kuwahesabu makocha wote, hata wale waliopo kwenye ligi za chini," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Bayern Munich na Liverpool, Ziege akiiambia Omnisport.

"Namba inakuwa hivi; Klopp, Guardiola, Pochettino au (kocha wa Bayern), Niko Kovac pia anakuwapo kwenye orodha hiyo.

"Kama ukiwaweka hao wote pamoja, bila shaka ni kwamba, Klopp anakuwa bora zaidi kushinda wote. "Na mimi ni shabiki mzuri zaidi wa Klopp, na kwa uhakika kabisa kwa sasa, yeye ndiye anabaki kuwa bora."

## HABARI MICHEZO

# De Gea: United lazima ishinde Old Trafford

**MANCHESTER,** England

DAVID de Gea amesisitiza kwamba, Manchester United lazima ishinde mechi za nyumbani badala ya kutoka sare kama ilivyokuwa dhidi ya wapinzani wao wa Ligi Kuu ya England, Arsenal juzi Jumatatu.

United imepata pointi tisa katika mechi zake saba za mwanzo kwa msimu wa 2019-20 chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer, na kuwafanya kuwa na mwanzo mbaya zaidi kwenye Ligi Kuu.

Bao la kwanza la Scott McTominay katika dimba la Old Trafford liliwaweka mbele 'Mashetani Wekundu' hao kabla ya mapumziko, lakini VAR ikawazawadia bao la kusawazisha Arsenal katika kipindi cha pili.

Makosa ya Axel Tuanzebe yaliigharimu United, mlinzi huyo alishindwa kucheza mpira na kumfanya Bukayo Saka kumtengenezea Pierre-Emerick Aubameyang kwa bao la kusawazisha.

De Gea, ambaye aliokoa vizuri mashuti ya Saka na Matteo Guendouzi, yalisaidia McTominay kwenda na mpira na kufunga bao hilo la uongozi.


"Ndio, lilikuwa kosa kubwa kwa upande wetu. Tuliruhusu bao muhimu zaidi," alisema De Gea akiiambia Sky Sports.

"Mchezo ulikuwa na uwiano sawa. Walikuwa na nafasi chache mno, lakini sisi ndio tulikuwa na nafasi kubwa.

"Tulikuwa na nafasi, bila shaka na wao walipata nafasi, lakini sisi tulipata nyingi zaidi na hatukuzitumia vizuri. Nafikiri sasa ni wakati wa kuangalia mbele na kuhakikisha tunashinda kila mchezo.

"Hii ni Manchester United, hivyo tunatakiwa kushinda mechi hizi muhimu. Kila mchezo wa nyumbani ni lazima tushinde ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi."

United imepata pointi 49 katika mechi 28 za Ligi Kuu ya England chini ya Solskjaer – ikiwa ni chache kwa mechi mbili alizopata Jose Mourinho mwishoni mwa msimu.





# EMERY AMTETEA XHAKA

**MANCHESTER,** England

UNAI Emery amemtetea nahodha wa Arsenal, Granit Xhaka, akimsifia kwa majukumu yake kwenye mchezo dhidi ya Manchester United wa Ligi Kuu ya England, juzi Jumatatu ambao ulimalizika kwa sare.

Xhaka, ambaye Emery alimthibitisha kuwa nahodha wiki hii, alishutumiwa mno kwenye mitandao ya kijamii baada ya United kupata bao la kwanza kwenye Uwanja wa Old Trafford, ambapo Arsenal ilitoka sare ya kufungana bao 1-1 na 'Mashetani Wekundu' hao.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Uswisi alionekana kushindwa kumzuia Scott McTominay aliyefunga bao kwa shuti kutoka umbali wa yadi 20, ingawa marudio ya picha ya video yalionyesha mpira ulimgonga kidogo kichwani kabla ya kutinga wavuni.

Kocha huyo wa Arsenal, Emery alimsifia Xhaka baada ya mchezo huo ambapo Pierre-Emerick Aubameyang alifunga bao lake la saba la Ligi Kuu msimu huu na kuweza kuwapa sare hiyo 'Washika Bunduki' hao wa jijini London.

"Alionyesha majukumu makubwa," alisema Emery akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikimbia kutoka nyuma. Alicheza vizuri, na sina tatizo kabisa na hilo," alisema.

Huku Alexandre Lacazette akiwa bado majeruhi, kinda Bukayo Saka alichukua nafasi na kung'ara kwa kumtengenezea pasi nzuri Aubameyang aliyesawazisha, ingawa mwanzo lilikataliwa kwa kuonekana kama ameotea, lakini teknolojia ya maamuzi ya usaidizi wa video, VAR ilionyesha hakuotea na iliruhusu bao hilo.

# *Piatek wa Milan sasa kumrithi Suarez Barca*

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inapanga maisha baada ya mshambuliaji wake wa kimataifa wa Uruguay, Luis Suarez.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alikuwa na wakati mzuri zaidi hapo kwenye dimba la Camp Nou, lakini kwa sasa anasumbuliwa na kushuka kiwango huku umri nao ukimtupa mkono.

Na sasa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Barca wanaangalia nani wa kuchukua nafasi yake.


Barcelona imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa AC Milan, Krzysztof Piatek kama ndiye mrithi wake wa muda mrefu Luis Suarez, kwa mujibu wa Calciomercato.it.

Suarez atatimiza umri wa miaka 33, Januari mwakani na mkongwe huyo wa Barca ameonyesha kushuka kiwango.

Barca wataangalia uwezekano wa kuleta sura mpya Januari, huku miamba hao wa soka la Hispania wakiwa wameshatenga kiasi cha euro milioni 50 kwa ajili ya kumsajili Piatek, huku Timo Werner wa RB Leipzig, mshambuliaji wa Getafe, Jaime Mata na mkongwe wa Juventus, Mario Mandzukic wakiwa wanahusishwa.



# DONDOO Z OKA MAGAZETI Y YA




# POGBA TATIZO UTOTO UNITED – SCHMEICHEL

## Sisemi kila anachokifanya ni kibaya, ninachanganyikiwa zaidi na namna kazi yake...

**MANCHESTER,** England

PETER Schmeichel anaamini Paul Pogba ni "tatizo la utoto" kwa Manchester United, kauli hiyo akiitoa wakati akihoji nafasi ya kiungo huyo nyota katika kikosi cha kwanza cha Ole Gunnar Solskjaer.

**Pogba alionyesha kiwango cha chini baada ya United kushikwa kwa sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu wakiwa nyumbani Old Trafford dhidi ya Arsenal juzi, Jumatatu usiku.**

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, ambaye alihusishwa na kujiunga na Real Madrid na Juventus wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto, alipona majeraha yake ya kifundo cha mguu na kuweza kuanza dhidi ya Arsenal hapo Manchester.

Hata hivyo, kipa wa zamani wa United, Schmeichel hakuwa na furaha kwa namna Pogba alivyocheza wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakiwa na mwanzo mbaya zaidi wa msimu kwenye Ligi Kuu kufuatia kufikisha pointi tisa tu katika mechi saba.

"Namna mpira ulivyokuwa ukisambazwa wakati Pogba akiwamo kikosini ni tofauti kabisa na kasi ya mpira ulivyokuwa ukisambazwa wakati akiwa hayupo kikosini," Schmeichel aliiambia Stadium Astro. "Hicho ni kitu nadhani wanapaswa kuendelea kukifanyia kazi. Kama Pogba anacheza ndani ya timu anapaswa kuongeza kasi ya mchezo. Aliupooza sana mchezo, katika dakika 25 za kwanza alikuwa akicheza tu mpira nyuma.

"Kwa mchezaji wa hadhi yake, hilo lilikatisha tamaa. Sitambui majukumu yake ni yapi katika timu hii. Hata Ole alipofanya mabadiliko na kumweka Pogba mbele zaidi, hakuna mengi yaliyotokea. Kulikuwa na pasi nzuri sana mbili kutoka kwa Pogba, lakini zilikuwa mbili, na si 15. Na ninaona hilo kama tatizo. Anachukua umakini sana. Ni aina ya kujisikia kama tatizo la utoto katika timu.

"Wakati unapokuwa na mtu ambaye anachukua umakini sasa, tunapaswa kutambua jukumu lake, nini atakwenda kukifanya kwa timu hii ya Manchester United? Nadhani wachezaji wanaoumzunguka ni wazuri wa kutosha.

"Alikuwa na aina ya kujificha kidogo katika kipindi cha kwanza, na zaidi kipindi cha kwanza. Kipindi cha pili alikuwa mzuri kidogo. Bila shaka wakati alipopanda mbele majukumu yake ya kukaba yalipungua kidogo, kisha alipata mpira kidogo zaidi. Kwa ukweli, hacheze kama alivyocheza msimu uliopita.

"Nadhani wanahitaji kujua jukumu lake ni nini, ni vipi Manchester United inapaswa kucheza naye kwenye timu. Halafu inapaswa kuwasiliana ili kila mtu [aelewe], [mashabiki] 75,000 hapa hawana furaha naye, kuwa sawa. Unasikia kila mahali, watu hawampendi Pogba sana kwa sababu yeye hafanyi mengi kwa timu, lakini tumeona kiwango bora cha dunia, tunampataje yeye kufanya hivyo katika timu hii ya Manchester United?

"Sisemi kila anachokifanya ni kibaya, ninachanganyikiwa zaidi na namna kazi yake ilivyo. Ni mchezaji wa kiwango cha juu duniani, unatarajia mtu kama yeye kuubeba mchezo, kuwaelekeza wachezaji makinda, kulikuwa na makinda saba leo [juzi] kuwa mtu wanayeweza kukutazama na kutafuta mwongozo wakati mambo yanapokuwa magumu."

## ZISIKUPITE

### DORTMUND YAMTOA SANCHO

MKURUGENZI wa Michezo wa Borussia Dortmund, amekiri hawezi kumuona mshambuliaji wa England, Jadon Sancho, 19, aliyehusishwa na Manchester United majira ya joto, akibaki katika klabu hiyo kwa muda mrefu. ***(Kicker, via Mail)***

### AMSUBIRI SOUTHGATE

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abraham, 21, anajiandaa kuikataa Nigeria na kuamua kuichezea England kama atapokea simu kutoka kwa Gareth Southgate kwa ajili ya kuitumikia kwenye michuano ijayo ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Jamhuri ya Czech na Bulgaria. ***(Telegraph)***

### VERTONGHEN AISIKILIZIA SPURS

BEKI wa Tottenham, Jan Vertonghen, 32, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu, amependekeza kuwa anaweza kutia saini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(London Evening Standard)***

### MANDZUKIC SASA AGEUKA LULU

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Mario Mandzukic, 33, anayewindwa na Manchester United, pia anatakiwa na timu ya Ligi Kuu Marekani (MLS), Los Angeles FC. ***(Calciomercato - in Italian)***

### KLOPP AMVUTA KOCHA PORTO

KOCHA wa Porto, Vitor Matos, amefikia katika mazungumzo mazuri na Jurgen Klopp anayemtaka kujiunga naye benchi la ufundi Liverpool. ***(Liverpool Echo)***

### WENGER KUMRITHI GIAMPAOLO

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger yupo katika orodha ya kupewa mikoba ya kocha wa AC Milan, Marco Giampaolo. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### TOBY AHUSISHWA NA UTD

MANCHESTER United imekuwa ikihusishwa na kwenda kumsajili nyota wa Tottenham, Mbelgiji Toby Alderweireld, 30, katika dirisha la Januari. ***(Tuttosport, via Inside Futbol)***

### PIQUE, RAIS BARCA KUTETA

BEKI wa Barcelona, Gerard Pique atafanya mazungumzo na Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu, wakati huu mvutano ukiongezeka kati ya wachezaji na bodi kwa mabingwa hao wa Hispania. ***(ESPN)***

### JUVE, INTER KWA RAKITIC

JUVENTUS na Inter Milan watakuwa wakijiandaa kuingia vitani katika dirisha la usajili la Januari kumwania kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 31. ***(Calciomercato, via Caught Offside)***

### ARSENAL KUMSOMA SZOBOSZLAI

ARSENAL imepanga kumtazama nyota wa kimataifa wa Hungary, Dominik Szoboszlai wakati akiichezea Red Bull Salzburg dhidi ya Liverpool kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya leo, wakati huu ikiwa inatarajia kutoa ofa kwa kinda huyo mwenye umri wa miaka 18 katika dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### TRAORE AWINDWA ROMA

ROMA inamfuatilia winga wa Wolves, Mhispania Adama Traore, 23. ***(Calciomercato)***

HABARI MICHEZO

# Simbu kufuata medali Qatar leo

**Na Shufaa Lyimo,** Arusha

MWANARIADHA wa Tanzania, Alphonce Simbu, leo jioni anatarajia kupanda pipa kuelekea mjini Doha, Qatar kushiriki mashindano ya Dunia yanayoendelea nchini humo.

Akizungumza na Nipashe jana, Simbu alisema amejiandaa kwa muda mrefu kuhakikisha anakwenda kuiwakilisha vema nchi, ambapo kwa upande wake atakimbia Jumamosi wiki hii.

"Nashukuru naendelea vizuri naomba Watanzania watuombee dua ili tuiwakilishe vema nchi yetu," alisema Alphonce.

Mwanariadha huyo aliongeza kuwa, mashindano hayo yatakuwa na ushindani mkubwa, kutokana na ukweli kwamba kila nchi itatoa washiriki watatu.

"Nimefanya mazoezi ya kutosha nikiwa chini ya makocha wangu, Antony Muingereza pamoja na Philipo Kandau, hivyo ninauhakika wa kufanya vizuri," alisema Simbu.

Mbali na Simbu, katika mashindano hayo washiriki wengine wa Tanzania ni Stephano Huche pamoja na Agustino Sule.




# Bondia Kakokere afariki Dunia Dar

**Na Sabato Kasika**

BONDIA wa zamani wa timu za Urafiki na Bora Shoes, Benedict Kakokere (62), amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana, ndugu wa marehemu, Francis Kakokere, alisema bondia huyo alifariki juzi katika Hospitali ya Mloganzila alikokuwa amelazwa.



Alisema bondia huyo alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa kiharusi, na kwamba anatarajiwa kuzikwa leo eneo la Pugu Kajiungeni jijini Dar es Salaam, na ameacha mke na mtoto mmoja wa kike.

"Enzi ya uhai wake alichezea timu za ngumi za Urafiki na Bora Shoes, lakini baadaye mwaka 1990 akastaafu na kufanya shughuli zake za ufundi wa vifaa vya umeme hadi umauti ulipomkuta," alisema Francis.

# BALINYA: KAZI NDIYO KWANZA IMEANZA KIMATAIFA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa Yanga wakiendelea kuugulia maumivu ya timu yao kushindwa kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mshambuliaji wa timu hiyo, Mganda Juma Balinya, amewataka kushusha presha kwa kuwa mpambano kimataifa bado unaendelea kwao kwa kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho.

Yanga ilitupwa nje na Zesco kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Jumamosi iliyopita kufuatia kukubali kipigo cha mabao 2-1 nchini Zambia ikiwa ni baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 katika mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, sasa Yanga imeangukia kucheza mechi moja ya mchujo nyumbani na ugenini dhidi ya timu mojawapo iliyovuka raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho, na ikipata matokeo ya jumla, itashiriki hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa inayoongoza kwa utajiri.

**Droo ya hatua hiyo inatarajiwa kufanyika Jumatano ijayo ambapo Yanga itajua timu itakayokutana nayo kuweza kuwania nafasi hiyo ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.**

Balinya alisema juzi kuwa mashabiki wa Yanga hawana budi kuwapuuza wote wanaowacheka kutokana na kufungwa na Zesco na kutolewa kwenye kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa kwani wao hawajapoteza kitu kwa kuwa bado wana nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Hakuna tulichopoteza kwenye mashindano ya kimataifa, tumeshuka daraja moja na sasa tunashiriki Kombe la Shirikisho Afrika, bado tupo na hatujakata tamaa, tutafanya kila kitu kuhakikisha tunamfunga kila atakayekuja mbele yetu," alisema Balinya.

Kwa sasa Yanga ambayo inaburuza mkia kwenye Ligi Kuu Bara baada ya kushuka dimbani mara moja na kupoteza mechi hiyo dhidi ya Ruvu Shooting, inajiandaa kuikaribisha Polisi Tanzania katika mchezo wa ligi hiyo utakaopigwa Uwanja wa Uhuru kesho.



Wachezaji wa timu ya Yanga ya Wanawake, Yanga Princess, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Ligi Kuu ya Wanawake itakayoanza baadaye mwezi huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *ZFF: Uzoefu umeiua Karume Boys Cecafa*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU wa Shirikisho la Soka Zanzibar ZFF Mohamed Ali Hilali, amesema licha timu ya vijana ya Karume Boys chini ya umri wa miaka 20 iliyoshiriki michuano ya Cecafa U-20 nchini Uganda kufanya vibaya, kwa ujumla wachezaji walijitahidi kulingana na umri wao huku akieleza kukosa uzoefu kuliwagharimu.

Alisema wachezaji hao kufanya vibaya kumetokana na uchanga wao wa kushiriki michuano hiyo ikilinganishwa na timu walizokuwa wakipambana nazo ambazo tayari baadhi ya wachezaji walikuwa na uzoefu.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema wachezaji wengi hawana uzoefu wa kushiriki michuano hiyo nje ya nchi, hivyo baadhi walikuwa na hofu tatizo lililochangia hata kutopata matokeo mazuri katika michuano hiyo inayoendelea nchini Uganda.

Alisema ZFF kupitia Kamati ya Maendeleo ya Soka la Vijana walichagua vijana ambao wataweza kuwaendeleza kulingana na umri wao ili wakipata nafasi ya kushiriki michuano mingine ya vijana tayari watakuwa na timu ambayo maandalizi yake hayatakuwa makubwa kutokana na kocha kujua mapema udhaifu wa wachezaji.

Karume Boys iliondolewa katika michuano hiyo katika hatua ya robo fainali baada ya kuchapwa mabao 5-1 dhidi ya Elitria, lakini ikiwa imeshinda mechi moja tu kati ya nne katika michuano hiyo ya Cecafa.

Michezo

Jumatano Oktoba 2, 2019

Nipashe



Pogba tatizo ni utoto United – Schmeichel UKURASA 30

TABU SANA...



Beki wa Manchester United, Ashley Young, akipata upinzani mkali kutoka kwa winga kinda wa Arsenal, Bukayo Saka, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Guardiola: Mashabiki wanataka taji la Uefa

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini Manchester City inatakiwa kuwapa raha zaidi mashabiki wake kwa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.



HABARI UK 28

## Emery amtetea Xhaka sare Utd

**MANCHESTER,** England

UNAI Emery amemtetea nahodha wa Arsenal, Granit Xhaka, akimsifia kwa majukumu yake kwenye mchezo dhidi ya Manchester United wa Ligi Kuu...



HABARI UK 29

# Zahera, Matola waliamsha

## ●●● Dimbani wote wakiugulia jeraha la Ruvu Shooting, huku donda la Yanga likitoneshwa na Zesco kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, akiwaonya wapinzani wao Ligi Kuu Tanzania Bara, kuwa wamerudi rasmi kwenye kinyang'anyiro hicho, Kocha wa Polisi Tanzania, Seleman Matola, amesema hasira zao za kupoteza mchezo wa kwanza mbele ya Ruvu Shooting anazielekeza kwa miamba hiyo.

**Yanga itaikaribisha Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara kwenye Uwanja wa Uhuru kesho, hiyo ikiwa ni mechi yao ya pili msimu huu baada ya kuanza kwa kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting.**

Hata hivyo, Yanga itaingia dimbani ikiwa na uchovu baada ya kundi la pili la wachezaji wa timu hiyo kurejea jana likitokea Zambia, ambapo walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Zesco United kufuatia kukubali kipigo cha mabao 2-1 ikiwa ni baada ya mechi ya awali jijini Dar es Salaam kulazimishwa sare ya bao 1-1.

Zahera ambaye kikosi chake sasa kimeangukia kucheza mechi ya mchujo kusaka nafasi ya kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, amesema akili na nguvu zote anazielekeza Ligi Kuu Bara, hadi atakapojua mpinzani wake katika michuano hiyo ya kimataifa.

"Tumetoka katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa tunarudi kwenye ligi ya nyumbani kupambana," alisema Zahera ambaye Jumatano ijayo watajua mpinzani watakayekutana naye kwenye mechi ya mchujo wakati Shirikisho la Soka Afrika (Caf), litakapochezesha droo.

Hata hivyo, Matola ambaye anajivunia rekodi nzuri ya kuifunga Yanga tangu akiwa na Lipuli FC ya Iringa msimu uliopita, alimwambia mwandishi wetu kwamba anatambua ugumu wa kupambana na Yanga kutokana na mabadiliko waliyoyafanya katika kikosi chao ila hesabu zake ni pointi tatu.

"Nafahamu Yanga imetolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na ina hasira ya kupoteza, ila isisahau kwamba nasi tumepoteza mchezo wetu wa kwanza mbele ya Ruvu Shooting tena kwa kujifunga wenyewe kwa bahati mbaya na tuliwadhibiti wapinzani wetu. "Tumefanya maandalizi mazuri na dozi kwa vijana inaendelea, historia yangu ya kushinda mbele ya Yanga hiyo naachana nayo kwani mpira hatuzungumzii wakati uliopita tunazungumzia dakika 90, tunachoomba ni mashabiki kutupa sapoti," alisema Matola.

Mbali na rekodi nzuri ya kuifunga Yanga wakati akiinoa Lipuli FC, pia mapema mwezi uliopita, Matola aliiongoza Polisi Tanzania kukichapa kikosi hicho cha Zahera mabao 2-0 kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Polisi Tanzania itashuka katika Uwanja wa Uhuru kuivaa Yanga ikiwa na pointi tatu ilizozipata kwa kuichapa Coastal Union kwenye Uwanja wa Ushirika katika mechi yao ya awali, huku kikosi hicho cha Zahera kikisaka alama zao za kwanza msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002